KUISHI KIKRISTO KWA VITENDO

Dr. Stephen Gibson

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Hakimiliki © 2021 Shepherds Global Classroom

Imetafsiriwa kutoka Toleo la Kwanza Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa. Isipokuwa kwa kurasa za majaribio, hakuna sehemu yeyote katika kitabu hiki itakayotengenezwa au kutawanywa kwa njia yeyote ile ya – elektroniki, mbinu za utunzi mfupi, kunakili, kurekodi au vinginevyo- bila kibali kutoka Shepherds Global Classroom (SGC). Kila toleo la mtalaa wetu wa SGC Kiswahili au Kiingereza linaponunuliwa linatusaidia kufanya tafsiri kwa lugha nyingi ili kuligawa kwa Viongozi wa Kikristo duniani kote. Ili kuwasiliana na SGC au kuchangia katika maono haya ya kuvutia sana, ingia kwenye tovuti yetu: www.shepherdsglobal.org.

Yaliyomo

Maelekezo kwa viongozi wa darasa 5
(1) Uadilifu wa Mkristo 7
(2) Mazoezi ya Utii kwa Mungu 19
(3) Kazi 27
(4) Mahusiano 35
(5) Kuongozwa na Mungu 45
(6) Mtazamo wa Biblia kuhusu Ndoa 53
(7) Utakatifu wa Ndoa 63
(8) Ikolojia ya Mkristo 73
(9) Fedha 79
(10) Uaminifu 89
(11) Thamani ya Binadamu 99
(12) Serikali 111
(13) Mwili wa Mkristo 119
Vyanzo Vinavyopendekezwa 127
Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa 129

Maelekezo kwa Viongozi wa Darasa

Maelekezo kwa kila somo yameandikwa katika somo lote kwa maandishi ya ulalo

Alama ► itakuwa kabla ya swali la mjadala. Kiongozi wa darasa atauliza swali na atawapa wanafunzi nafasi ya kujadili. Ikiwa mwanafunzi mmoja atajibu swali mara kwa mara au wengine watakaa kimya, kiongozi anapaswa kuelekeza swali kwa mwanafunzi fulani.. " Igor ni kwa jinsi gani utajibu swali hilo?"

Maandiko mengi yametumika katika somo hili. Wakati ambapo darasa limeagizwa kusoma kifungu cha maandiko pamoja, maelekezo yataonesha hivyo. Kwa mfano: mwanafunzi mmoja asome Warumi 6 kwa niaba ya kikundi. Wanafunzi wote lazima watafute kile kifungu kinachosomwa. Wakati mwingine maandiko huelezwa katika mabano. Kwa mfano: (1 Wakorintho 12:15). Nukuu hizo zinaunga mkono yalio andikwa. Sio lazima kuyasoma yale yalio katika mabano.

Kila somo lina mazoezi ya kufanya yaliyoelezewa mwishoni. Mazoezi lazima yakamilishwe baada ya somo na kiongozi wa darasa ajulishwe wakati wa somo litakalo fuata. Kama mwanafunzi hatamaaliza mazoezi anaweza kumalizia baadae. Lakini kiongozi atawahimiza wanafunzi kufuata ratiba ili wasome mambo mengi Zaidi darasani. Chati imewekwa mwishoni mwa somo ili kuweka rekodi ya mazoezi ambayo mwanafunzi amekamilisha.

Moja ya kusudi la somo hili ni ili kuwafanya wanafunzi wawe waalimu. Kiongozi wa darasa anapaswa kuwapa wanafunzi fursa ya kukuza ujuzi wao katika kufundisha. Kwa mfano kiongozi wa darasa mara kwa mara anapaswa kuwapa wanafunzi fursa ya kufundisha sehehu ndogo katika somo darasani.

Katika mwisho wa kila somo kuna sehemu ambayo inaelekeza juu ya majadiliano katika vikundi. Kiongozi wa darasa ataamua muda ambao mtatumia. Masomo mengi yatakuwa na muda mwingi wa majadiliano mnapoendelea kujifunza kitabu hiki.

Pia katika mwisho wa kila somo kuna sala fupi fupi ya kumuomba Mungu ili amuwezeshe mwanafunzi kuutendea kazi kweli katika maisha yake. Kiongozi wa darasa anaweza kumuomba mwanafunzi mmoja kusoma lile ombi kwa niaba ya darasa.

Somo la 1
Uadilifu wa Mkristo

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuelewa ni nini Biblia humaanisha inapozungumza kuhusu "dunia."

(2) Kutambua maeneo ambayo dunia na maadili yake yameathiri Maisha yake.

(3) Kueleza ni kwa jinsi gani na ni kwanini namna ya kufikiri ya mkristo ni lazima iwe tofauti na mwenye dhambi.

(4) Kuelezea inamaanisha nini mkristo kuishi maisha ya uadilifu.

(5) Kuonyesha kwamba kweli ya kikristo lazima udhihilishwe katika kila Nyanja ya maisha.

Yohana Chrysostom, Mhubiri wa Uadilifu

Yohana Chrysostom (370's),[1] alikuwa mchungaji mcha Mungu aliyejulikana kama "Mdomo wa dhahabu" kwa sababu ya mahubiri yake yenye nguvu na ya kukaririwa sana. Alipendwa na mwanadamu wa kawaida na akawa mhubiri mwenye sifa sana katika dola ya Rumi Mashariki. Alitekwa nyara mnamo 398 na akapelekwa katika mji mkuu wa Konstatinopo (kwa sasa Istanbul, Uturuki) alihudumu kama mchungaji na askofu wa kanisa la kitaifa lenye washirika 100,000.

Yohana alijulikana kwa msimamo wake thabiti. Alitumia ofisi yake kutumikia mahitaji ya mji wote, na sio tu matajiri. Alilisha maskini, akajenga hospitali, aliwasaidia wajane. Aliwaandau maaskofu katika Asia ndogo kwa sababu ya rushwa na matumizi mabaya ya fedha na alihubiri na kukemea anasa na usherati. Aliwaonya matajiri wa Kostantinopo kwamba, kuhudhuria viwanja vya maonyesho machafu kutawaharibu**.** Alilinganisha mambo hayo na virusi hatari vya kufisha, Yohana alisema,

> Ukimuona mwanamke asiye na adabu katika ukumbi wa michezo akiwa na kichwa ambacho hakijafunikwa na hisia za ushujaa, nguo zake zikiwa na rangi za dhahabu, huku akionyesa hisia zake za ngono na kuimba nyimbo zisizo na maadili, akionyesha viungo vyake akiimba na akiyatamka maneno yasio na adabu …utasema hamna kitu ambacho ni cha kawaida ya kibinadamu kimekutokea? …baada ya ukumbi kufungwa na kila mtu ameondoka, hizo picha zitakuwa bado katika nafsi yako, maneno yao, tabia zao, sura zao, kutembea kwao kukaa kwao-viungo vyao vikiwa wazi- na wewe utaenda nyumbani umefunikwa na vidonda elfu! Isitoshe hautakuwa peke yako pia

[1] Gerald L. Sittser. *Water from a Deep Well*. (Downers Grove: InterVarsity Press, 2007), 135

> yule kahaba atenda na pamoja wewe ijapokuwa sio kwa uwazi na kwa kuonekana… lakini kwa moyo wako na dhamili yako na ndani mwako atawasha tanuru ya Kibabeli ambako amani katika nyumba yako na usafi wa moyo wako na furaha ya ndoa yako itateketea.

Kwa matajiri Yohana aliwaonya,

> Ni upumbavu na ukichaa wa wazi kuwa na hazina ya mavazi na huku ukiwaacha wanadamu walioumbwa kwa sura na Mfano wa Mungu wakiwa uchi huku wakitetemeka kwa baridi kiasi kwamba hawawezi kusimau wima… Wewe ni mkubwa na mnene, unafanya karamu za unywaji pombe mpaka usiku wa manane, na unalala katika kitanda laini na chenye joto. Na wala haujafikiria jinsi utakavyo toa hesabu ya jinsi ulivyotumia vibaya zawadi kutoka kwa Mungu… kwa maana fedha setu ni za Mungu ijapokuwa tumezitafuta. Ndiposa Mungu amekuruhusu uwe na vingi, na sio ya kutumia isisvyostahili… bali kuwagiwa wale ambao wana uhitaji.

Yohana Chrysostom alipewa adhabu ya kuhamishwa kuelekea katika fukwe za mashariki mwa Bahari Nyeusi lakini alikufa akiwa safarini (A.D. 407). Maneno yake ya mwisho yalikuwa "Utukufu uwe kwa Mungu kwa mambo yote. Amina."

Mtazamo wa kimaandiko kuhusu ulimwengu.

Yohana 17 ni maombi ya Yesu kwa wanafundi wake muda mfupi kabla ya kusurubishwa. Yanaonesha kujali na upendo mkuu ambao Yesu alikuwa nao kwa wanafunzi wake. Alisema pia anawaombea wale ambao wataamini ujumbe wa mitume (mstari wa 20) kwa hivyo wakristo wa leo wamejumuishwa.

► Mwanafunzi mmoja asome Yohana 17:14-18 kwa niaba ya kikundi.

Yesu alimaanisha nini aliposema yeye sio wa ulimwengu? Tunajua yakwamba asili yake si ya hapa ulimwenguni,yeye ni mwana wa Mungu ,aliyekuja duniani kutoka mbinguni. Ijapokuwa anaposema jambo hili kwamba yeye sio wa ulimwengu hauanishi ya kwamba ametoka mahali fulani tofauti katika ulimwengu huu. Akasema pia wanafunzi sio wa ulimwengu huu pia kama vile yeye asivyo wa ulimwengu huu. Yesu alikuwa anaongea kuhusu watu waliozaliwa katika dunia hii na wazazi ambao ni wanadamu na wakakua na kuwa wananchi katika nchi zao.

Kwa hivyo Yesu alimaanisha nini aliposema wanafunzi wake sio wa ulimwengu huu? Lazima tuelewe basi maadiko yanauanisha nini wakati yanaposema kuhusu ulimwengu.

► Mwanafunzi mmoja asome Waefeso 2:1-3 kwa niaba ya kikundi.

Mistari hii inatuonyesha kwamba kuishi kama ulimwengu unavyoishi ni sawa na kuzifuata njia za shetani. Tunaona pia ya kwamba watu wa ulimwengu hufuata tamaa zao mbaya na watapata adhabu kutoka kwa Mungu. Waaminio wamepokea maisha mapya na hawaishi tena kama ulimwengu.

► Mwanafunzi mmoja asome 1 John 2:15-17 kwa niaba ya kikundi.

Ulimwengu unaonyeshwa hapa katika 1 John kama mahali paovu. Sio pa kupendwa, wala yaliomo ndani yake si ya kupendwa. Tamaa na nia mbaya ni kawaida ya ulimwengu. Tamaa mbaya huitwa tamaa ya kidunia.

Shetani anaitwa mtawala wa ulimwengu huu (John 16:11). Hii haimaanishi kwamba ulimwengu ni wake kihalali, yeye ni kiongozi wa uasi kwa Mungu na watu wa ulimwengu wanamfuata. Yeye alishahukumiwa tayari, na watu ambao wanaendelea kumfuata pia watahukumiwa.

Kuwa rafiki wa ulimwengu ni kuwa adui wa Mungu (Yakobo 4:4).

Ulimwengu una mamillioni ya watu kimwili, walioanguka, waliotengwa na Mungu na kuunganishwa na kile ambacho wanashirikiana kwa pamoja. **Kwanza wana mvuto na tamaa mbaya**. Wanapenda mambo ya ulimwengu kuliko muumba wa Dunia. 1 Yohana 2:15-17 yasema," Msiipende dunia… Kwa maana vyote vilivyo katika dunia—tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima—sio ya Baba bali ni ya dunia."

Pili, tamaa yao mbaya huwaelekeza katika tabia mbaya; maisha ambayo yanalenga kujitosheleza wenyewe,kwa kutohurumia wengine na kuwanyima haki na rehema (Amosi 5:11-15; 21-24). Wanaenda katika njia zao wenyewe, wakidai wanachohitaji na wanajiamulia kilicho sawa na kisicho kwa ajili yao wenyewe. Japokuwa wana aina nyingi za dini, wote walio wa ulimwengu hujifanya (wenye elimu ya kibinadamu, hekima ya kibinadamu, Hamu ya kibinadamu, uzuri wa kibinadamu, nguvu za kibinadamu) kuwa kitovu cha ibada yao. (Warumi 1:25). Hawaamini nguvu na uweza wa Mungu lakini wanaamini filosofia ya Maisha ambayo huhalalisha kile walichoona na kuamua kuwa ni haki wao kutenda. Hawatafuti kufahamu yaliyo haki na kuyatenda. Wanafanya kile ambacho wanataka halafu ndipo wanatafuta namna ya kueleza kwamba ni sawa.

Wanasaikolojia na washauri wa kidunia huwasaidia watu kutatua hukumu katika dhamira zao pasipo toba na msamaha wa Mungu. Wana filosofia wa kidunia hujaribu kueleza kusudi la kuishi ambalo halimshirikishi Mungu. Wanasayansi wa ulmwengu hujaribu kueleza chanzo cha kila kitu huku wakimkataa muumbaji. Wanasiasa na wafanyakazi za kijamii katika ulimwengu hujaribu kutafuta namna ya kuzuia maadhala ya kiasiria ambayo husababishwa na dhambi pasipo kuona dhambi kama chanzo cha shida zote. Wanamitindo wa mavazi wa duniani wanafanya bidii sana kutengeneza mavazi yenye kuleta hisia na yenye mvuto. Watumbuizaji wa kidunia hufanya vichekesho na mizaha ya dhambi, maadili na dini. Wachungaji wa kidunia wanamwamini mungu ambaye anavumilia dhambi na ambaye anajali sana wewe kuwa tajiri na mwenye mali, mwenye furahana mwenye kujithamini.

Wakolosai 2:8 yatuonya tusindanganywe na kuibiwa na filosofia na uongo kwa mambo ya ulimwengu. Msanii tapeli huwaibia watu kwa kuuza wazo la uongo. Kwa kushawishi watu kwa maoni potovu, dunia huwaibia wanadamu ushirika wao na Mungu, faida zao za kiroho, na Mbingu.

Filosofia na kudhibiti motisha za kidunia huonekana katika mtindo wa maisha ya watu wa ulimwengu. Kuongea kwao, mitazamo, namna ya kuvaa, burudani, na tabia za kidunia huonyesha dhambi katika mioyo yao.

Wakristo hawawezi kufuata maadili ya jamii zao. Wakristo wanatakiwa kuwa tofauti na jamii zao.

Tamaduni kutengenezwa na kitu hiki ambacho Biblia huita ulimwengu. Vizazi vya watu mahali fulani hutengeneza tamaduni. Wao hupenda mambo mengi mazuri kama vile usalau, mafanikio na familia iliyo imara, lakini huyatafuta mambo hayo kwa kutumia filosofia za ulimwengu na hudhamiria kupata pasipo kunyenyekea kwenye neno la Mungu. Hiyo inamaanisha kwamba wakristo hawawezi kufuata kila kitu katika tamaduni zao. Biblia inaushawishi katika baadhi ya tamaduni kuliko zingine,lakini hakuna tamaduni ya taifa lolote ambalo ni la kikristo kikamilifu.

► **Kulingana** na kile kulichosoma hadi sasa, ina maanisha nini kwamba wanafunzi wa Yesu' sio wa ulimwengu?

Wakristo hawafuati tamaa na matamanio ya dhambi. Zaidi ya yote wanataka kumpendeza Mungu. Mapenzi yao yamekuwa na yanazidi kubadilishwa (Wafilipi 1:9-11). Sheria ya Mungu imeandikwa mioyoni mwao. (Yeremia 31:33). Amri za Mungu sio nzito kwa wakristo bali wanazifurahia (1 John 5:1-3; Zaburi 19:7-11). Wakristo wana vipaumbele vya milele (Mathayo 6:33). Tabia zao huonyesha wanataka kushinda majaribu na kuishi maisha ya ushindi dhidi ya dhambi.

Watu wa dunia hufikiri wakristo ni wa ajabu kwa sababu hawavutiwi na vitu vya kidunia kama wao. (1 Petro 4:4). Yesu alisema ulimwengu unawachukia watu ambao ni tofauti kiroho. (John 17:14). Ulimwengu una uhasau na wale ambao sio wake. Hawaelewi, wanakasirikia haki, na wanahukumiwa na dhambi zao. Ndio maana Yesu alisema "….ulimwenguni mnayo dhiki…." (John 16:33). Mtume Paulo anasema, "Naam, na wote wapendao kuishi Maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." (2 Timotheo 3:12).

► Mwanafunzi asome 2 Wakorintho 6:14-18 kwa niaba ya kikundi.

Biblia huwaeleza wakristo wawe tofauti na dunia. Tofauti hii huanza na mtazamo wa mtu binafsi kama inavyoelezwa na Yesu katika mahubiri ya mlimani. Hapa anaelezea mtazamo wa mkristo kuwa ni mtazamo wa unyenyekevu, kuhuzunika kwa ajili ya dhambi, upole, haki, rehema, usafi wa moyo, amani na kukubali kuvumilia mateso. Mtazamo ulio wa tofauti matokeo yake ni tabia tofauti. Kwa mfano mkristo hawezi kushirikiana na kikundi ambacho kinafanya maovu. Mungu ameahidi kuwa Baba kwa wale wanaoamua kuwa tofauti na ulimwengu. Kumbuka tuliangalia kifungu cha Maandiko kinachosema rafiki wa ulimwengu ni adui wa Mungu. (Yakobo 4:4).

► Mwanafunzi asome Mathayo 5:13-16 kwa niaba ya kikundi.

Kuwa tofauti kwa ulimwengu hakumaanishi wakristo kujitenga na jamii na kuanzisha au kutengeneza jamii yao wenyewe. Yesu alisema haombi wanafunzi wake watolewe ulimwenguni (Yohana 17:15). Alisema pia wanafunzi wake ni taa na chumvi ya ulimwengu, hii inamaanisha kwamba lazima ulimwengu uwaone. Mkristo lazima ahusike katika mambo ya serikali na katika maeneo yake katika jamii ispokuwa wakati ambapo atatakiwa kufanya kile ambacho sio sawa.

Gerald Sittser anatuambia jinsi hii ilivyokuwa katika Ukristo wa kwanza:

> Aristides, na Athenian wanafilosofia walio… ishi katika karne ya pili waliorodhesha mambo kadhaa ambayo yalionesha tofauti ya Wakristo na halaiki ya watu wengine. Wakristo, walisema, walikuwa na uaminifu, ukweli, kutosheka, heshima kwa wazazi, upendo kwa majirani, utamaawa, uvumilivu wanapokumbana na mateso na ukarimu kwa wageni. Waliwatunza wajane na yatima. Waliwatunza watumwa kwa wema usio na kipimo. "Watumwa wa kike na wa kiume… waliwashawishi kuwa Wakristo kwa upendo waliowaonyesha. Waliofanyika Wakristo, walikuwa ndugu pasipo ubaguzi."[2]

Imani Halisi

Barua ya Yakobo inasisitiza kwamba imani ya kweli ya Kikristo hudhihirishwa katika maisha. Yakobo anasema mtu anayesikia neno la Mungu na asilifanye anajidanganya (1:22). Watu wengine hufikiri ni wema kuliko wengine kwa sababu wanajua zaidi ukweli wa kikristo-hata kama hawatii-lakini hiyo siyo kweli.

Yakobo anasema watu wengine ni wa kidini,lakini dini yao haina manufaa. Mungu anapendezwa na dini ya mtu ambaye anakutana na mahitaji ya wengine na anajiweka safi, asichafuliwe na ulimwengu (1:27).

► Mwanafunzi asome Yakobo 2:14-26 kwa niaba ya kundi.

Kuna watu husema kwa sababu wokovu hupatikana kwa imani na sio kwa matendo, hazijalishi tabia zetu. Wanafikiri kuna uwezekano wa mtu kupata wokovu hata kama nia yake, maisha yake ni kama ya wasioamini. Kifungu hiki cha maandiko katika barua ya Yakobo inaongea kuhusu watu kama hawa.

Yakobo anasema kuamini tu hakutoshi; hata mapepo wanaamini, lakini hawana ushirika na Mungu (aya 19). Mtu amwaminiye Mungu lakini hawezi kunyenyekea ni kama mtu asikiaye injili lakini wala hatubu.

Ni muhimu kueleza mstari wa 21 na 24. Inasema ya kwamba Abrahamu alihesabiwa haki kwa matendo, na kwamba mtu anahesabiwa haki kwa matendo pamoja na imani. Maandiko haya ni kama yanakinzana na maandiko ambayo yanaweka mkazo kwamba mtu huokolewa kwa neema sio matendo.[3] Yakobo hauanishi kwamba mtu huokolewa kwa imani na matendo lakini mtu huonyesha ameokoka kwa imani na matendo. Yeye haokolewi kwa matendo,lakini

[2] Ibid, 54
[3] Waefeso 2:8-9, Wagalatia 2:16, Warumi 3:28

kama hataishi kama Mkristo, hana imani iletayo wokovu. Yakobo anasema imani ya mtu imekufa kama maisha yake hayaambatani na hiyo imani (Mstari 26).

Yakobo anasema kwamba haiwezekani mti uwe na aina mbili za matunda au kisima kiwe na aina mbili za maji, mtu hataweza kunena Baraka na laana kwa wakati mmoja (3:9-12). Tabia za mkristo kila wakati zitafanana na imani yake.

Mtazamo wa Maadili

Katika Warumi 2:21-24, Paulo aliongea na Wayahudi waliofikiri wao walikuwa ni bora zaidi kuliko watu wa mataifa kwa sababu walikuwa na maandiko, hata kama hawakuyatii. Akawauliza "wewe uhubiriye kwamba mtu asiibe, waiba mwenyewe?" Akasema, "wewe ujisifuye katika torat, wamvunjia Mungu heshimakwa kuiasi torati." Ukweli kwamba walijiinua wenyewe kama watu wa dini lakini hawakuwa na tabia nzuri na hii ilifanya mataifa kumtukana Mungu na Maandiko.

Ikiwa mtu ana uadilifu, tabia yake italingana na amini wake. Kwa mfano mtu aliye mwaminifu atajumuisha tabia na usemi wake wote. Mtu asemaye ni mwaminifu lakini anafanya kitu ambacho hakilingani na uaminifu hana maadili.

Neno maadili linaweza kutumika kwa tabia ya mtu. Katika lugha zingine linatumika kueleza mambo mengine kama vile muundo wa jengo.

► Unafikiri inamaanisha nini muundo wajengo kuwa na maadili?

Ni muhimu jengo kusimau. Ni lazima liweze kuhimili uzito wake lenyewe na uzito wa mambo yeyote ambayo hufanyika ndani yake. Ikiporomoka,watu na mali zitamaamia na thamani la jengo itapotea. Maadili ya jengo humaanisha ya kwamba kanuni za majengo thabiti lazima zitumike katika ujenzi wote.

Ni vizuri pia jengo lisimame kwa mda mrefu. Mtu ambaye hujenga nyumba hutumaini ya kwamba itasimau Imara kwa muda wote wa Maisha yake. Majengo ya serikali au kampuni hugharimu sana kwa sababu linatarajiwa kusimau kwa vizazi vingi.

Kama jengo litaanza kuinau au kuporomoka ni kwa sababu halina maadili. Wakati mwingine jengo huharibiwa na tetemeko la ardhi, ijapokuwa litakuwa limesimau lakini sio salau. Halina maadili.

Kabla jengo kuanza ni muhimu kuna ramani ya mchoro uliyo na maelezo. Maelezo ya muhimu ni kwa jinsi gani jengo hilo litakuwa na nguvu na uwezo wa kusimau. Sehemu zote za jengo hilo ni lazima kuunganishwa na kushikamanishwa kwa pamoja.

Ni ya muhimu kwa mjenzi kufuata mchoro anapojenga. Akipunguza gharau kwa kuacha sehemu muhimu za muundo, jengo hilo halitakuwa salama.

► Inamaanisha nini mtu kuwa na maadili?

Yesu anatumia mfano wa ujenzi wenye maadili. Anasema mtu anayesikia na kumtii Mungu ni kama mtu ambaye anajenga nyumba yake juu ya mwamba. Hiyo nyumba husimau wakati wa dhoruba. Mtu asiyemtii Mungu ni kama mtu anayejenga nyumba juu ya mchanga. Haitoshi kusikia tu na kujua ukweli.

► Mwanafunzi asome Yakobo 1:22-25 kwa niaba ya kundi.

Yakobo anasema mtu anajidanganya kama atasikia neno la Mungu na asilitende. anarejelea mtu anayefikiria ni mzuri kwa sababu anajua ukweli katika Biblia japokuwa hafuati wala kuishi kwa huo ukweli. Mtu huyu hana maadili.

Yakobo anasema kwamba tunaposoma neno la Mungu tusiwe kama Yule mtu ambaye hujiangalia tu kwenye kioo lakini habadiliki kutokana na kile ambacho anaona. Kweli ya Mungu hubadilisha. Tunapo angalia neno la Mungu tunaona makosa yetu, na tunastahili kumruhusu Roho wa Mungu Abadilishe mienendo na tabia ili zifanane na kweli ya Mungu.

Maadili huonyeshwa katika mtindo wa maisha. Mtu hatakiwi kutosheka anapotambua kwamba nia au tabia fulani haiendani na kweli ya Mungu.

Jaribio la Tunda

Yesu alisema kutakuwepo na manabii wengi wa uongo. Hawa ni watu ambao wanataka vyeo vya kidini au wafanye Huduma kama biashara, lakini hawana tabia za Kikristo. Alisema tutawatambua kwa matunda yao (Mathayo 7:15-18). Tunda sio mafanikio. **Tunda ni hali ya kawaida ya kuelezea tabia za mti**. Tunda la mtu ni maisha yake yakidhihirisha utu wake wa ndani. Endapo mtu hatazaa tunda la Roho (Wagalatia 5:22-23; 1 Wakorintho 13), au anaishi maisha ya dhambi, ana tabia za dhambi na yeye sio kiongozi wa kweli wa kiroho (1 Wakorintho 6:9-10; 2 Wakorintho 11:13-15).

Mtume Petro anasema waumini hawastahili kuongozwa na tamaa za awali za kale bai wanapswa wawe watakatifu kwa vyote wanavyovifanya. (1 Petro 1:14-15).

Tunda nzuri halimaanishi kwamba mtu huyo anaelewa vizuri kabisa jinsi ya kutumia kanuni zote za Kikristo katika tabia zake. Sisi sote tuko katika mchakato wa Kujifunza neno la Mungu. Mtoto akiwa anafanya kazi bustanini, kimakosa anaweza kung’oa mimea isiyostahili. Mungu hawezi kutuhukumu kwa makosa tusiyoyajua. Japokuwa, neema haituruhusu kutoomba msamaha kwa makosa tuliyoyafanya. Mtume Yohana anatuambia mtu husafishwa “anapotembea katika mwanga” kuishi sawasawa na ukweli (1 Yohana 1:7).

Maadili katika uongozi

Viongozi hufanya maamuzi ambayo wengine sio lazima kuyafanya. Wajibu na nafasi ya kiongozi hutengeneza fursa nyingi za majaribu. Uamuzi wa kiongozi ni wa muhimu kwa sababu unaathiri wengi.

Kiongozi katika huduma lazima akumbuke kwamba yeye, akiufuata mfano wa Yesu, ameitwa kumtumikia Mungu na Watu. Lengo lake lisiwe kuwa maarufu ambaye anasifiwa na kutumikiwa na wengine.

Kama kusanyiko lina watu wengi ambao hawaabudu Mungu katika kweli hubadilisha ibaada kuwa ni kuigiza. Watu hawa huheshimu vipawa kuliko kuwa na mtazamo wa kiroho. Wanapenda ibaada iongozwe kwa watumbuizaji lakini sio viongozi wa kweli wa kiroho. Wanatumbuizwa kimwili. Wako radhi kuwalipa wanamuziki ambao hawajaokoka gharau kubwa ambao wako tayari kupiga muziki katika kumbi za burudani na ambao hawajakidhi vigezo vya kushiriki katika ibaada. Mchungaji lazima alinde ibaada ya kanisa ili kuvutia na kuhudumia Waabudu wa kweli.[4]

► Kama mtu atahudhuria ibaada jumapili asubuhi na awaone wanamuziki walewale ambao aliwaona katika kumbi za burudani jumamosi usiku atafikirije kuhusu kanisa?

Kiongozi anaweza jaribiwa kujitoa katika sheria za kawaida za maadili. Baadhi ya wachungaji wengine wana mahusiano mabaya na wanaume au wanawake kanisani kama vile viongozi wa kidunia wanavyofanya. Makanisa mengine huvumilia tabia mbaya kwa wachungaji kwa sababu ya hadhi zao.

Mchungaji anaweza kujaribiwa kuamini kwamba kanisa ni lake. Endapo atafikiria hivi, ataweka watu katika nyadhifa za uongozi kwa sababu wananyenyekea chini yake, na sio kwa sababu wako tayari kufanya kazi nzuri. Aina hii ya mchungaji hupendelea ndugu zake na pia huchagua atakayerithi kanisa baada yake. Yeye hufunika dhambi na makosa ya wale wanao muunga mkono kanisani. Yeye hutumia fedha na mali za Kanisa kama zake binafsi.

Ushahidi wa Kanisa

Kanisa linaweza kuharibika endapo likikosa viwango vya uadilifu. Wakati Kanisa linashiriki katika tamaa za kidunia, wanakubali viongozi walio kama wa kidunia. Wanavumilia dhambi kwa viongozi wao wa dini. Hata Wakristo wa ukweli wanaweza kufuata viongozi waovu kwa sababu hawaelewi umuhimu wa maadili na tunda jema. Wakati haya yanafanyika, watu wa kidunia huongoza kanisa na kanisa linapoteza ushuhuda.

Petro anawaonya viongozi waongo wa kiroho ambao wanalifanya Kanisa biashara (2 Petro 2:3). Kanisa likipata umaarufu katika dunia, watu wa kidunia wanapendezwa na kutaka kupata nafasi za uongozi katika hilo kanisa. Wanajifunza mfumo wa ibaada na wanakuwa viongozi wa dini pasipo kuokoka. Kanisa lisilokuwa na mafundisho mazuri haitawatambua.[5]

Yesu anatumia mfano wa chumvi kueleza nini hufanyika wakati kanisa linapopoteza utofauti wake (Mathayo 5:13). Chumvi ikipoteza ladha haina maana ni kama tu mchanga.

[4] Kwa mtazamo mkuu ibaada ya mkristo, Shepherds Global Classroom somo *Utangulizi wa Kuabudu Kikristo*, yapatikana katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

[5] 2 Petro 2 na kitabu cha Yuda vimeandikwa kwa mada ya viongozi wa kiroho wa uongo.

Kanisa likiwa kama ulimwengu, kanisa haliwezi kuubadilisha ulimwengu.

Ulimwengu unalidhihaki kanisa pale ambapo kanisa linafuata mtindo wa dunia na halifuati kweli ya maandiko.

Kumuwakilisha Mungu

Theolojia ni mfumo wa imani yetu Wakristo*,* ikijumlisha mafundisho kumhusu Mungu, mwanadamu, dhambi, Kristo na wokovu. Imani yetu kumhusu Mungu ni msingi wa imani zingine zote.

Mungu anapoanza kujidhihirisha, kusudi la kwanza la ufunuo wake ni kuonyesha yeye ni Mungu wa aina gani. Kimsingi Mungu anajieleza kama mtakatifu. Neno la kiebrania la utakatifu (kadosh) limetumika zaidi ya mara 600 katika Agano la Kale. Kwa mfano, Isaya mara kwa mara anamtaja Mungu kama "Mtakatifu wa Israeli". Utakatifu wa Mungu ndio uliokuwa kusudi la kumuabudu (Zaburi 99:3, 5). Watu wa Mungu hawakumuabudu kwa sababu ya nguvu zake pekee, lakini kwa sababu ya utakatifu wake.

Mungu pia anajidhihirisha kama upendo. Andiko katika agano la kale ambalo laonekana kwa wingi ni wakati Mungu anajidhihirisha kwa Musa na wana wa israeli Kutoka 34:6-7. Hapo Mungu anajidhihirisha kama, "…Mungu wa huruma na neema, si mwepesi wa hasira mwingi wa upendo na ni mwaminifu, huwapenda maelfu na husamehe uasi na dhambi. Japokuwa hataacha dhambi bila kuadhibiwa…" Ni vizuri kuweka utakatifu na upendo wa Mungu pamoja. Neno ambalo hutumika kueleza utakatifu na upendo wa Mungu pamoja ni "upendo - mtakatifu". Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, anatutaka kuwa na utakatifu ndani yetu; kwa sababu Mungu ni upendo ametengeneza njia ya sisi kuwa watakatifu, kama yeye alivyo mtakatifu.

Utakatifu wa Mungu unaonyesha ya kwamba watu hawastahili kumwabudu na kumtumikia kabla kwanza ya kubadilishwa na kufanywa wapya kwa neema. Nabii Isaya aliona kwamba kuna kitu ambacho alikuwa nacho kilichofanana na wenye dhambi aliokuwa anawahubiria – alikuwa na moyo ambao haukuwa safi (Isaya 6:5). "Midomo michafu" iliwakilisha maneno na matendo machafu yaliyotokana na moyo usiosafishwa. Huku kutosafiwa kulimfanya Isaya kutofaa kuwa katika uwepo wa Mungu. Isaya hakubishana na kujifanya kuwa wa kukubalika na pia Mungu hakuidhinisha. Mungu aliitikia ungamo la nabii kwa neema; sio neema ya kuvumilia bali neema ya kutakasa na ya kubadilisha (Isaya 6:6-7).

Mungu wa Israeli alikuwa tofauti na miungu mingine ya uongo na alihitaji ibaada ya tofauti. Katika Zaburi 24 mfalme Daudi anauliza swali "ni nani atakayepanda katika mlima wa Bwana?" (mstari 3). Alikuwa anauliza "nani aubaye Mungu humkubali kama mwabudu?" halafu akatoa jibu, "Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe" (aya 4). Sio kila mtu

atakubaliwa kumwabudu Mungu. Mwabudu sio tu mtuyule ambaye anaweza kuinua mikono na kupata hisia. Mwenye dhambi hakidhi vigezo.[6]

Mungu alisema utakatifu wake ndio msingi muhimu na unaohitajika kwamba wanomuabudu wawe watakatifu. "Iweni watakatifu kwa maana mimi ni mtakatifu" (Walawi 11:44-45, 19:2, 20:26, 21:8). Mungu hakuwa kama miungu ya mashariki au miungu ya ugiriki ya kisasa au ya dini za kirumi. Simulizi kuhusiana na miungu hawa ilielezwa kuwa ni miungu fisadi, wadanganyifu na wakatili. Miungu hawa walikuwa na udhaifu wote wa kibinadamu. Kama kivuli kwenye ukuta, walikuwa ni uzidisho wa upotovu wa sura ya mwanadamu. Miungu hawa hawakuhitaji kiwango cha maadili au viwango vya mienendo, na waliokuwa wanawaabudu walikuwa wenye dhambi na wakatili.

Mungu wa Israeli sio sura ya mwanadamu iliyo inuliwa. Siyo wa kufikirika, bali amejidhihirisha mwenyewe kwa wanadamu. Yeye ni wa tofauti, na ni kwa sababu hiyo wanaomwabudu lazima wawe tofauti.

Viwango vya Mungu vimerudiwa katika agano jipya: "bali kama yeye aliyewaita ni Mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu." (1 Petro 1:15-16). *Mazungumzo* ni neno ambalo linaonyesha nia, tabia, mienendo-katika kila nyanja ya maisha. Mungu haitaji tu wanaomwabudu wawe watakatifu kwa muda au waitwe "watakatifu" wakati wao si watakatifu. Anawahitaji wanaomwabudu waishi maisha matakatifu.

Mtazamo wetu na tabia zetu zinaonesha namna tunavyofikiri kumhusu Mungu na ushirika tulio nao na yeye. Mtume Paulo alisema kwamba wayahudi ambao walijivunia kuwa na sheria za Mungu hawakumuheshimu Mungu kwa kuzivunja. Kwa sababu ya tabia zao, watu walisema mambo mabaya kumhusu Mungu wao. (Warumi 2:23-24).

Unamuwakilisha Mungu wa aina gani? Watu wanafikiri nini kumhusu Mungu wako? Kama unataka watu wajue Mungu wako ni mtakatifu na pia anasamehe na ni wa neema wanahitaji kukuona wewe ukiwa hivyo.

Makanisa yanahitaji wachungaji wao wafundishe kwa utaratibu mzuri mafundisho sahihi yenye uzima. Mchungaji asipuuze mafundisho ya msingi. Kila kizazi na wakristo wapya wanahitaji kusikia hayo. Hata wakristo waliokomaa wakumbushwe. Mahubiri ya mchungaji sio tu yawe na hisia na yale yanayofanya watu wasisimke. Ni lazima amuelezee Mungu na pia aelezee jinsi maisha ya Wakristo yanavyopaswa kuambatana na maandiko katika kila Nyanja.

Kanisa lazima libadilishe jamii na utamaduni, lakini hii itafanyika tu wakati ambapo dhana za kibiblia kumhusu Mungu itatekelezwa katika kila Nyanja ya Maisha yetu.

[6] Kwa uchunguzi kamilifu wa ibada halisi, tazau Shepherds Global Classroom somo *Utangulizi wa Kuabudu Kikristo*, inapatikana kwa https://www.shepherdsglobal.org/courses

Kushiriki kwa vikundi

► katika somo hili, ni mambo gani ni mapya kwako? Ni kwa namna gani kubadilisha mtazamo wako katika maisha ya kikristo?

► Jambo gani ambalo unafikiri linapuuzwa sana katika makanisa katika utamaduni wako? Utaeleza vipi jambo hili kwa mtu unayemjua?

Maombi

Baba wa mbinguni,

Nataka kukuheshimu kwa maisha ambayo yaambatana na tabia zako. Nataka nikuwakilishe wewe katika dunia ambayo haijanyenyekea kwako.

Fanya maisha yangu daima yalingane kweli yako. Nisaidie kukubali kubadilisha jambo lolote ambalo sio sehemu ya maisha ya mkristo

Asante kwa kunipa roho wako anitiaye nguvu na neema ibadilishayo.

Amina

Zoezi la somo la 1

(1) Andika aya moja kuhusu mtazamo wa dunia ambao umeathiri tabia yako na fikra zako hivi karibuni. Tafuta maandiko mawili ambayo yanaongea kuhusu jambo hili na uyaandike. Andika aya moja kuhusu namna ambavyo unaweza kuanza kuishi kwa kutii maandiko hayo.

(2) Soma Tito 2:11-14. Andaa uwasilishaji fupi kuhusu maadili ya mkristo kutokana na andiko hilo. Tumia andiko hilo kueleza kwa nini kweli za Kibiblia zinatakiwa kutendewa kazi katika kila Nyanja ya Maisha. Shirikisha uwasilishaji hii mwanzoni wa darasa lijalo.

Somo la 2
Mazoezi ya Utii kwa Mungu

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) kuchunguza uhusiano wa kivitendo uliopo kati ya upendo wakikristo na maisha binafsi ya mkristo.

(2) kuaangalia kwa umaakini maeneo kumi ambayo mkristo katika hali ya kuendelea ataishi maisha yake sawasawa na kanuni za maandiko.

(3) kueleza sababu mbili kwanini wakristo hutofautiana kutumia Kanuni za kimaandiko zinazohusiana na mambo ya kimaisha.

(4) Fupisha kanuni tisa(zilizotolewa katika somo) za kufanya maamuzi maishani.

Mwana Mtii

Mau wa kiafrika alienda kumtazau mtoto wake mdogo aliyekuwa akicheza chini ya mti. Alishikwa na mshangao alipoona joka kubwa lenye sumu likininginia juu ya mti karibu na kichwa chake. Lile joka lilikusudia kumuuma yule mtoto. Mau alijua ya kwamba angejaribu kumuonya mtoto wake angeangalia juu badala ya kuondoka mahali pale upesi. Badala ya kumwelezea, alimuita, "mwanangu lala chini sakafuni sasa hivi". Yule mvulana alichanganyikiwa, lakini kwa sababu alikuwa amefundishwa kutii, akafanya hivyo hivyo. Mau yake akasema tana "Tambaa pole pole huku ukija kwangu". Mara nyingine tena yule mvulana akatii na akaokolewa kwenye hatari ya lile joka.

Kwa nini mtoto alitii hata kabla hajaelewa sababu ya ile amri? Aliheshimu mau yake kwa sababu alikuwa tayari amefundishwa kutii, na tayari alikuwa amewahi kurekebishwa wakati ambapo hakutii. Pia alimuamini mau yake kwa sababu alijua mau yake anampenda. Tunatakiwa kumtii Mungu kikamilifu sio kwa sababu tunaogopa adhabu yake bali kwa sababu tunajua anatupenda.

Motisha ya Upendo

► nini kitatokea endapo mtu atampenda Mungu sana? Unaweza kuzingatia swali hili kwa kukamilisha sentensi ifuatayo: "Kama nitampenda Mungu sana nita…"

Mojawapo ya matokeo ya kumpenda Mungu sana imeelezwa kwenye kitabu cha Wafilipi 1:9-11:

> Na hii ndio dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila

kosa, mpaka siku ya Kristo; hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

Kifungu hiki cha Maandiko kinazungumza kuhusu mchakato endelevu katika maisha ya mwamini. Upendo wake uwe wa kuongezeka. Upendo wake kwa Mungu unakua, uwezo wake wa kupambanua yaliyo bora unafanywa kuwa bora na unapanuka. Wakati anapambanua kilicho bora, anayakita Maisha yake katika kuwa makini na kile kilicho bora zaidi. Lazima hii ifanyike ili mkristo awe mkamilifu pasipo dosari.

Kama ambavyo mtoto mchanga aliyezaliwa ana maisha ya kujifunza mbele yake, vivyo hivyo na sisi tunapofanywa upya katika maisha ya Kikristo, hatuwezi kuelewa kikamilifu ukweli unaotuelekeza katika maisha. Katika mistari iliyotangulia, Paulo anawandikia watu waliokuwa wakristo kwa muda sasa. Na bado Paulo anawaombea kwamba wampende Mungu zaidi na kwa kumpenda Mungu Zaidi wataelewa na kutii mapenzi ya Mungu.

Tunatarajia kubadilisha maisha kwa kadri Mungu anavyotupa ufunuo. Mungu anataka utii wetu kamili katika nyanja zote za maisha, sio tu katika mambo ya kiroho peke yake.

Tusipuuze na kudhani ya kwamba tunajua kila kitu ambacho tunahitaji kujua kuhusiana na jinsi tunavyopaswa kuishi. Tusidhani ya kwamba tumeshafanya mabadiliko yote yanayohitajika katika misha yetu.

Maeneo Ambayo Mkristo Anatakiwa Kubadilika

(1) Uangalifu Katika Ushawishi (Mithali 22:1; Mathayo 5:14-16)

Je kuna mambo ambayo unafanya na usingependa watu wengine wafanye? Je utasikitika ukiona mchungaji wako anafanya mambo ambayo wewe unafanya?

(2) Kiasi (Mithali 16:32, 25:28; Wagalatia 5:22-23)

Je wewe unatawala hisia na matamanio yako ili ufanye kile ambacho unapaswa kufanya au wakati mwingine unaruhusu hisia na tamaa zako kukuongoza kufanya kama yeye asiyeamini?

(3) Kutunza Afya (1 Wakorintho 6:19, 10:31)

Je wewe hutunza mwili wako kama silaha madhubuti iliyowekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Mungu? Kwa vile mwili wako ni wa Mungu haupaswi kuharibiwa. Hautakiwi kutunza mwili wako isivyostahili.

(4) Uchaguzi wa Burudani (Wakolosai 3:17; 1 Wakorintho 6:12)

Je burudani yako husababisha majaribu ambayo hufanya wewe upapambane na majaribu kwa kukusababishia mawazo na nia mbaya? Kuwa makini sana na mambo ambayo yanawakilisha Dhambi lakini huvutia sana na kufurahisha.

(5) Tabia (Warumi 13:9; Wakolosai 3:19; 1 Timotheo 2:8; 1 Petro 3:2)

Waheshimu wengine, kwa sababu wameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu na wana hatima ya milele. Watu huwa na tabia ya kuonyesha utuwema. Lazima ujifunze kuonesha utu wema kwa namna ambayo watu watatambua. Kuwa mtu mwema hata kama watu unaowatendea wema hawastahili.

(6) Tabia Katika Biashara (Mithali 20:23)

Je wewe ni mwaminifu katika biashara zako? Je wewe hueleza vitu kama vilivyo au humfanya mtu afikirie kwamba jambo fulani si kweli?

(7) Kuwa Makini na Muda (Kutunza Muda) (Wagalatia 5:14)

Muda ni wa muhimu sana na tunapaswa kuutumia sana kwa ajili ya Mungu. Je wewe huthamini muda wako na wa wengine kwa kufuata ratiba kila panapo hitajika?

(8) Mavazi (1 Timotheo 2:9; 1 Petro 3:3-4)

Je mavazi yako yanaonyesha maadili?

- Adabu – Je yanafunika mwili vizuri?
- Unyenyekevu – siyo ya kuleta mvuto na umakini ambao hauitajiki kutokana na ulichovaa.
- Ubadhilifu – kutonunua mavazi ya gharama ya juu kuliko unavyohitaji.

(9) Lugha (Wakolosai 4:6, Waefeso 4:29)

Je, maneno yako ni ya heshima kwa Mungu na wengine? Maneno mengi ambayo dunia hutumia kama mshangao hayatokani na Mungu.

(10) Kutumainiwa (Zaburi 61:8; Mithali 20:6, 28:20)

Je wewe hutunza ahadi? Je, watu wanaweza kutarajia ufanye kile ambacho ulisema? Je huwa unasahau ahadi zako kama siyo rahisi?

Watu wengi hawatilii maanani umuhimu wao kubadilika au kujiboresha. Wanahisi kuwajibika tu katika amri zilizo wazi katika maandiko, pasipo kujua ya kwamba amri hizi hutumika sehemu nyingi za maisha ya kila siku.

Tunahitaji kufahamu ya kwamba kuwa bora kumeshikamanishwa na kuongezeka kwa upendo wetu kwa Mungu. Tunahitaji kutafakari kwa kumaanisha maandiko tuliyoanza nayo katika somo hili.(Wafilipi 1:9-11). Kama upendo wetu unazidi kuongezeka, uwezo wetu wa kupambanua na kuchagua tabia sahihi utaongezeka.

Kushiriki katika Vikundi

► Ni mfano gani wa kubadilika ambao umeufanya katika maisha yako wakati ambapo Mungu alikuonyesha jambo fulani, mtazamo, nia, tabia au matendo ambayo siyo mazuri?

► Je, kuna kitu katika maisha yako ambacho unajua unapaswa kukibadilisha? Utakibadilisha?

► Je, unafanya jambo ambalo hauna uhakika kama linampendeza Mungu?

► Je, unakubali Mungu akuonyeshe katika maombi jambo lolote ambalo unastahili kulibadilisha?

Tujitoe kuomba wiki hii tukiwa na moyo ulio wazi ili Mungu atamaaonyeshe njia zake na badiliko lolote ambalo tunapaswa kulifanya katika maisha yetu. Je unajitoa kufanya hivyo? Juma lijalo nitakuuliza kama ulitekeleza.

Kanuni za Biblia za Kutekeleza Kibinafsi

► Je, meshawahi kutambua tofauti kati ya wakristo, na hasa katika mambo halisi ya kivitendo kwa yale ambayo wanafanya na yale ambayo hawafanyi? Kwa nini hizi tofauti zipo, na wakati wanatumia Biblia ile ile? Kwa sababu kunatofauti nyingi sana kwa wakristo, je yale tunayoyatenda ni muhimu? Kwanini?

Siyo wakristo wote wanakubaliana kwa pamoja juu ya undani wa jinsi ya kuziishi kanuni na maadili ya kibiblia. Lakini ni lazima kwa Mkristo kumaanisha na kuwa na uzito wa kuishi sawasawa na kile anachokiamini.

Tabia, maamuzi ya burudani na aina ya mavazi huonesha kitu kuhusiana na makusudio ya moyo.

Hapa kuna kanuni ambazo kila mkristo ni lazima azikumbuke anapojaribu kupambanua nini ambacho ni mtindo mzuri wa maisha.

Kanuni za Maamuzi Kuhusiana na Mtindo wa Maisha

(1) Lazima tutii amri amri zote za kibiblia kwa wakristo.

Yesu akasema Mathayo 5:19,

> Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja ya hizi zilizo ndogo, na kufundisha watu hivyo ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; lakini yeyote atakayezitenda na kufundisha ataitwa mkuu katika ufalme wa mbinguni.

Hatuwezi kuchagua tu kile ambacho tunafikiri ni muhimu zaidi. Hakuna amri katika maandiko ambayo si ya umuhimu ili yapuuzwe

(2) Amri za Mungu ni za Manufaa Kwetu.

Kumbukumbu la Torati 10:12-13,

> Na sasa Israeli, Bwana Mungu wako, anataka nini kwako, ila umche Bwana, Mungu wako na kwenda katika njia zake zote, na kumpenda na kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote. Kuzishika amri za Bwana na sheria zake nanazo kuamuru leo, upate uheri.

Zaburi 84:11,

> Kwa kuwa Bwana Mungu ni jua na ngao:Bwana atatoa neema na utukufu: Hatawanyima kitu chema hao waendao kwa ukamilifu.

Mungu hawezi kutuzuilia kile ambacho ni kizuri, au kutuamrisha kufanya kile ambacho ni hatari kwetu. Tusingekuwa sawa pasipo masharti yake. Kukataaa maelekezo yake ni kutilia shaka hekima na upendo wake. Tunadhibitisha kwamba tuna imani katika uzuri na hekima yake wakati ambapo tunatii maagizo na neno lake kuliko kufuata maoni ya watu.

(3) Uhuru wa mkristo sio uhuru wa kutomtii

Paulo anaandika haya kwa wakristo 1 Wakorintho 9:21:

> Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria,(si kwamba sina sheria mbele za Mungu bali mwenye sheria mbele za Kristo, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu.

Tunakombolewa kutokana na mfumo wa –sheria ya Musa na matakwa ya Mungu ya kimaadili kwa njia ya kuhesabiwa haki, kwa maana tunaokolewa kwa neema sio kwa kutimiza sheria za Mungu. Pia tunaokolewa kutokana na hukumu ya sheria kwa sababu dhambi tulizozifanya zimesamehewa.

Hata hivyo hatujawekwa huru kutoka katika hitaji la kumtii Mungu au jukumu la kupenda "maana mliitwa kuwa huru. Usitumie uhuru na nafasi katika mwili, lakini kwa upendo tutumikie mmoja na mwingine" (Wagalatia 5:13). Kama 1 Wakorintho 9:21 (hapo juu) inaonyesha, sisi tuko chini ya mamlaka ya Mungu. Mapenzi yake kwetu yananadhihirishwa katika Biblia.

Watu fulani huamini kimakosa kwamba ni lazima washike sheria za Mungu kama njia ya kupata msamaha wa dhambi, au kwa njia ya kukomaa kiroho. Ukweli ni kwamba tunaokolewa kwa neema kwa njia ya imani, si kwa kushika sheria (Waefeso 2:8-9).

Ingawa hatuhesabiwi haki kutokana na yale tunayofanya, tunalazimika kumtii Mungu katika mambo yote ya maisha kwa sababu tumefanywa kuwa waadilifu pamoja naye. "Kuwekwa huru kwa dhambi, unakuwa mtumwa wa haki" (Warumi 6:18).

Kwa sababu tunampenda Mungu na tunashukuru kwa neema yake, tunamtii kwa furaha (1 Yohana 5:3). Utii wa wale wanaohesabiwa haki ni ushahidi wa upendo kwake (Yohana 14:15).

(4) Kama Tunampenda Mungu Tunahitaji Tujue Mapenzi yake sio Kuyaipuuza.

1 Yohana 5:2-3 yasema

> Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.

Yeremia 31:33 yasema, "Bali agano hili ndilo litakalo fanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile,asema Bwana nitatia sheria yangu ndani yao na katika mioyo yao nitaiandika;nami nitakuwa Mungu wao,nao watakuwa watu wangu".

Mtu anayempenda Mungu hatamaaliza kwanza, "Mungu atanihukumu kwa hili?" lakini ni "Mungu atapendezwa na lipi zaidi?" au "nini ni zuri zaidi la kufanya?" (Wafilipi 1:10; Tito 3:8).

(5) Maandiko yanatupea misingi ya kujifanyia kanuni katika maisha.

Maandiko hayatoa Kanuni za ujumla tu. Maandiko kadhaa yametolewa katika Zoezi la pili ambalo linampa mkristo msingi wa kuishi Maisha makini ya kikristo. baadhi ya Maandiko yanatoa maelekezo mahususi kwa ajili ya kuishi maisha ya kikristo.

(6) Kanuni kuhusiana maelezo ya maisha sio imani yetu ya msingi.

Wafarisayo walifanya makosa ya kuweka mkazo kwa vitu vidogo. Katika Mathayo 23:23 Yesu akawaambia

> Ole wenu waandishi na mafarisayo wanafiki! kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.

Andiko hili halimaanishi kwamba kuna yale ambayo si ya msingi, lakini linamaanisha mengine ni ya muhimu zaidi. Tunahitaji kuongea kuhusu yalio ya muhimu zaidi.

(7) Kuzingatia Kanuni Haitoshi Kuthibitisha Utii au Upendo Wako kwa Mungu.

Katika mazungumzo hayo Yesu anawaambia mafarisayo (Mst 25),

> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano na ndani yake vimejaa unyaganyi, na kutokuwa na kiasi.

Mtu anaweza kuishi maisha ya kujidhibiti sana lakini bado hawampendi Mungu au pia wala hamtii Mungu kikamilifu. Kwa upande mwingine mtu anaweza kumpenda Mungu kwa moyo wake wote lakini asione umuhimu wa viwango vingine vya kanuni. Kwa hivyo haimaniishi kwamba mtu anayejidhibiti sio wa kiroho zaidi.

(8) Imani yetu katika shuhuda za wengine haitegemei mambo madogo madogo ya mitindo ya Maisha yao.

Katika Warumi 14:10 Paulo anawauliza Wakristo

> Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.

Mstari huu unatoka katika kifungu ambacho kinajadili mitazamo tofauti tofauti ya wakristo katika maisha. Kuna maoni tofauti kuhusiana na kile ambacho wakristo wanapaswa na hawapaswi kufanya.

Muumini mwingine anaweza asikubaliane na tafsiri ya kifungu ulani cha maandiko, au asione ubaya wa kitu ambacho kimekataliwa. Inawezekana kuwa Mungu anafanya kazi ndani yake katika maeneomengine, au Mungu amemuweka mahali penye utamaduni tofauti. Hii haimaanishi kwamba Mtu huyo si mkristo wa ukweli.

► Unafikiri nini kuhusu sentensi hii? "Mungu atamuonyesha ukweli kila mtu kuhusiana na jinsi atakavyoishi; kwa hivyo, wakristo wote watakuwa na matendo sawa."

Wakristo hawajakubaliana kabisa katika matendo mbali mbali katika maisha. Watu wanaompenda Mungu na wanaoishi katika maisha yanayompendeza Mungu hawakubaliani katika kila kiyu kuhusiana na tabia, Matendo na mafundisho. Ni vibaya sisi kusema wengine sio wakristo kwa sababu wanatafsiri na kutekeleza maaandiko tofauti na sisi. Tunaweza kuwakubali wao kama wakristo kamili japokuwa tunafikiri mawazo yao sio sawa. Kazi ya Roho Mtakatifu sio kufanya watu wote waishi maisha na tabia zinazo fanana.

Ni lazima pia sisi tuwe tayari kijifunza kutokana na mitazamo ya wakristo wengine. Kiburi hutufanya sisi tufikiri kwamba sisi au kanisa letu lina tafsiri sahihi ya maandiko. Mtu mnyenyekevu, anayefundishika, roho ya kukubali, hukuza umoja wa wakikristo na kuujenga mwili wa Kristo.

(9) Hali ya kuwa na mawazo tofauti haimruhusu yeyote kuishi maisha ya kutojali.

"Na kila mtu adhibitike katika akili zake mwenyewe" (Warumi 14:5b).

"Lakini aliye na shaka kama akila amehukumiwa kuwa ana hatia kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilo toka katika imani ni dhambi." (Warumi 14:23).

Kuna shida pale ambapo mtu anakiuka dhamiri yake. Mtu akiamua kufanya kitu ambacho anafikiri ni kibaya, yeye amefanya dhambi. Kuna Baraka wakati mtu anatembea katika nuru ambayo Mungu amempa. (1 Yohana 1:7).

Kushiriki kwa vikundi

Hakutakuwa na ugumu katika kuanza kujadili juu ya mada hii. Wanafunzi wengine watapendelea kwamba makanisa yanahitaji sheria na mwongozo wa tabia. Wengine watasitititiza kuvumilia tofauti.

Jaribu kuzingatia kanuni tisa ambazo tumezijadili hapo awali.

► Ni Kanuni gani kati ya hizo kanuni unafikiri watu watasahau?

► Ni Kanuni gani kati ya hizo kanuni wewe unaweza kusahau?

Maombi

Baba wa mbinguni,

Ninataka upendo wangu kwako uzidi, ningependa nielewe kikamilifu nia yako kwangu.

Nisaidie kupambanua yale ambayo yanakupendeza sana ili niishi maisha yasiyo na mawaa.

Nisaidie nione tabia na nia ambayo nahitaji kuibadilisha, ili nipate tabia na nia inayokutukuza wewe.

Nataka nizae matunda kwa ajili utukufu wako Mungu.

Amina

Zoezi la somo la 2

(1) Soma 1 Wakorintho 13. Hii sura inaeleza kuhusu mtu ambaye ana upendo ambao anapaswa kuwa nao kwa wengine. Acha Mungu akuonyeshe jinsi ambavyo angependa kukubadilisha na kufanya maisha yako yawe ya kuendelea sana katika upendo. Orodhesha mabadiliko ambayo ungependa Mungu akuwezeshe kuyafanya katika maisha yako.

(2) Soma maandiko yafuatayo ambayo yanatupatia misingi ya tabia za mkristo:

- 1 Wakorintho 6:19-20
- 1 Wakorintho 10:31
- 1 Wakorintho 11:14-15
- 1 Timotheo 2:9-10
- 1 Petro 3:3-4
- Zaburi 19:14
- Zaburi 101:3

Andika maana ya kimsingi katika kila andiko. Eleza mtindo wa maisha ambao unaamini utaishi kwa sababu ya maandiko hayo.

Somo la 3
Kazi

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Eleza kile ambacho biblia inasema kuhusu kazi.

(2) Atatekeleza tabia za Mkristo kazini.

Ndugu Lawrence, mfanya kazi wa Mungu

Ndugu Lawrence alikuwa Mtawa aliyeishi kwenye nyumba ya watawa katika miaka ya 1600. Akawa maarufu kwa kufanya kazi ya kawaida-kuchonga viazi, kuosha vyombo, nk.- kutokana na upendo wake kwa Mungu hakuacha uwepo wa Mungu ukae mbali naye. Wakati wote alimfanya Mungu kuwa katikati ya kila jambo maishani mwake,hata kazini.

The Practice of the Presence of God (Zoezi la uwepo wa Mungu) ni kitabu kidogo ambacho kimesomwa na mamilioni. Kinahusisha mahojiano na barua kutoka kwa ndugu Lawrence. Anaandika, "Utakaso wetu hauegemei kubadilisha kazi, lakini hufanya kile ambacho tunajifanyia kwa uzuri wetu kwa Mungu".

► Kazi ni nini? Je kazi ni kuajiriwa tu? – kuajiriwa ili ufanye jambo**.**

Kazi huhusisha kuajiriwa, lakini pia inahusisha kujitunza sisi wenyewe na kutunza wengine, kutunza mali tuliyo nayo, kuzalisha, kufanya biashara kwa faida na kusaidia wengine bure.

► Ni vizuri Mkristo afanye kazi? Kwa nini?

Watu wengi hufikiri ingekuwa vizuri kuwa na pesa ili wasifanye kazi. Wanafikiri maisha yangependeza kama yangekuwa maisha ya kustarehe.

Mtazamo wa Biblia kwa kazi

Fikiri jinsi ambavyo Mungu aliumba ulimwengu hapo mwanzo. Iikuwa kamilifu. Yalikuwa mazingira kamilifu kwa watu wa kwanza ambao Mungu aliwaumba. Mungu alitoa kazi ya kwanza kwa watu. Mungu angeumba dunia iwape wanadamu mahitaji yote pasipo kazi, lakini Mungu alijua maisha bora kwa watu yatahusisha kazi.

Mungu alipanga kazi yetu iwe na uhusiano. Watu lazima wajifunze kushirikiana, kutegemeana, wawe wa kutumainiwa, tutumie nguvu kuwasaidia wengine walio wadhaifu, tukumbane na changamoto pamoja, tutatue kutoelewana, turekebishe makosa, tufundishwe na tufundishe wengine.

Mungu alitupa mamlaka na majukumu ya kuweza kutawala dunia, kuiweka chini ya uongozi na kuikuza kwa utukufu wake. Kazi hii imetuelekeza katika ukulima, ufugaji, uchimbaji wa migodi na uendelevu wa teknolojia.

Mungu alituumba sisi juu ya kila kiumbe maana tuko na kitu katika maumbile yake ndani mwetu. Zaburi 8:6-8 yasema

> Umemtawaza juu ya kazi za mikono; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake. Kondoo, na ngombe wote pia; naam, na wanyama wa kondeni; ndege wa angani na samaki wa baharini; na kila kipitacho njia za baharini.

Kwa sababu ya dhambi ya kwanza dunia ilibadilika, na kazi kujumlisha ugumu na ukataji tamaa ambao haukuwa katika mpango wa kwanza wa Mungu. Hata hivyo, lazima tutambue Mungu ametuumba na tunahitaji kazi.

Kazi yetu ni sawa na kazi ya Mungu ya uumbaji. Kazi ya mwanadamu ni njia moja ya kutengeneza mazingira. Mapato sio kusudi tu la kufanya kazi. Watu wana majukumu ya kubadilisha mazingira. Wanajaribu kufanya bora nyumba zao. Wanajaribu kutupa mbali takataka. Mtu yeyote ambaye hatamani tena kufanya kazi amekata tamaa ya kubadilisha mazingira. Amekata tamaa ya kufanya kile ambacho kinamuanisha kuwa mwanadamu.

► Wewe hufikiria nini ukiona nyumba ambayo haijatunzwa?

Mwanadamu katika hali ya uumbaji, mpangilio, uzalishaji na kufanya kazi ni mojawapo ya sura ya Mungu ndani ya mwanadamu. Kwa hivyo kazi yote ni nzuri kwa mkristo. Kazi yote ni tendo la ibaada ikifanywa kwa kumtukuza Mungu (Wakolosai 3:17, 23). Yesu anasema Baba yake alifanya kazi kwa hivyo yeye pia anafanya kazi. (Yohana 5:17).

Usifikiri kazi kama jambo ambalo halipendezi lakini inahitajika, kama vile kutumia dawa ukiwa mgonjwa. Kazi sio tu jambo la maana ili wewe uishi. Ni sehemu ya maumbile ya Mungu kwa wanadamu.

2 Wathesalonike 3:10 yasema, "Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwa kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi basi asile chakula."

Tufanye nini kama kazi yetu itaonekana kau isiyo ya maana? Mahatma Gandhi alisema, “Kile ambacho unafanya kinaweza kuonekana sio cha muhimu, lakini ni muhimu sana ukifanye”. Fikiria mtu aliye ajiriwa kufagia sakafu. Ambayo inaonekana sio ya muhimu, lakini anafanya uamuzi mzuri. Wakati anaenda kazini kila siku, anaamua kufanya hiyo kazi kuliko kutumia muda wake kukaa bure, pasipo kuongeza thamani kwa yeyote. Anachagua kuwajibika kwake mwenyewe kuliko awe kupe kwa marafiki na familia. Anasaidia wale ambao wanamtegemea labda mke na watoto, kuliko kuwalazimisha wao wajitafutie msaada. Kwa kuzingatia haya yote inatusaidia kutambua ya kwamba kazi inaweza kuonekana kama haistahili lakini ni ya maana kwa sababu alichagua kuifanya.

Je kuna watu ambao hawawezi fanya kazi kwa hakika? Hapana. Hata kama mtu huyu hawezi kuajiriwa kufanya kazi ya mshahara,anaweza fanya kitu kutimiza haja ya mwingine.

Mkristo lazima afanye kazi maana ana majukumu yake na ya wengine. Mtu hastahili kutarajia wengine akutane na mahitaji yake kama hataki kufanya kile ambacho anaweza.

Mwamini ana majukumu ya familia yake kwanza. “Lakini mtu yeyote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa mwake hasa, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini”. (1 Timotheo 5:8).

Mwamini ameamriwa na maandiko afanye kazi ili akutane na mahitaji ya wengine. “Mwibaji asiibe tena, bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia muhitaji”. (Waefeso 4:28). Tambua tofauti kati ya anayeiba, na kuchukua kitu na yule ambaye anafanya kazi ili kwamba aweze kutoa. Mkristo sio mtu tu asiyeiba lakini afanyaye kazi ili atoe.

Unaweza pata kazi hata kama haujaajiriwa na mtu. Tafuta namna ya kuwa msaada kwa mtu ambaye anahitaji. Ni vizuri kuishi namna hiyo kuliko kutofanya kitu na kulalamika kuwa watu hawakusaidii.

Mwamini lazima afanye kazi ajisaidie na asaidie familia na pia wengine walio na mahitaji.

Njia za kawaida za Mungu kukutana na mahitaji yetu

► Utamwambije mtu ambaye husema hatafanya kazi kwa sababu anamtumainia Mungu akutane na mahitaji yake?

Fikiri ya kwamba msimu mmoja wa kiangazi unatembea katika bustani na upate nyanya, mahindi, maharagwe na mboga zimekua na zitakutosha kwa mda mrefu.

Hilo litakaa kama muujiza? Ilifanyika kwa maelfu ya watu wakati wa kiangazi kilichopita. Walitembea katika bustani zao na waka pata hayo yote yamefanyika na zaidi. Lakini hawakushangaa wala kushikwa na butwaa kwa sababu miezi kadhaa kabla,walikuwa wamelima mashamba yao na kupanda mbegu kwa miezi wakamwagia maji na wakapalilia. Kwa hivyo walipopata mimea ni ile tu walicho kutarajia.

Utaonaje, "Basi huo haukuwa muujiza kamwe." Lakini Mungu alifanya mamilioni ya mbegu na mwanadamu hajafanya hata moja. Zaburi 104:14 yasema, “Huyameesha majani kwa makundi na maboga kwa matumizi ya mwanadamu ili atoe chakula katika nchi” Mungu huyafanya hayo lakini mwanadamu hutayarisha shamba kwa kupanda mbegu,na kunyunyuzia maji wakati unapo hitajika.

Watu wengi hufikiri tendo la Mungu sio la kawaida, pasipo kanuni za dunia za kawaida, kama vile wakati Yesu aliponya au wakati jua lilisimama. Kwa hivyo katika mtazamo huo kukua kwa mimea sio maajabu lakini ni la kawaida.

Lakini katika kutaka muujiza pia tunapuuza njia za Mungu za kawaida za kufanya kazi. Kulikuwa na mamilioni ya watu walio tembea katika bustani zao leo na hawakupata kitu ambacho wengekula. Hawakushirikiana na njia ya Mungu ya kutokeza chakula. Njia ya kukuza chakula ni moja mfano ya kawaida kazi ya Mungu. Kwa mfano njia ya kawaida ya

Mungu ya kutupatia ni mwanadamu kufanya kazi. Mithali 14:23 yatufundisha "katika kazi yote kunayo faida…" pia Mithali 19:15 yatuonya kwamba "…Nafsi yake mvivu itaona njaa."

Kuna watu ambao wanatamani kama Mungu angewafanyia jambo lakini wana puuza nafasi za kufanyia kazi, kwa sababu nafasi hizo sio za kazi ambazo wangependa kufanya.

Na kama unapenda kufanya kazi na hupati mtu wa kukuajiri? Kuna kazi ambayo ungefanya kuwasaidia wengine,na kupitia hiyo baadhi ya mahitaji yako utakutana nayo. Kama hujaajiriwa una wakati. Kwa nini usiangalie hapo karibu na wewe na uone unaweza saidia aje mtu mwingine?

Utaonaje mtu ambaye hajaajiriwa na anatumia masaa yake yote kukaa na hafanyi chochote. Hakuna kitu kabisa cha maana cha yeye kufanya? Katika ujirani wake kuna watu ambao wanahitaji msaada. Kuna takataka ambazo zahitaji kuchukuliwa. Kuna shamba inahitaji kulimwa ili kuleta mazao. Kuna vitabu ambavyo angehitajika kusoma ili aongeze maarifa. Kuna mtu ambaye anaweza kumuombea. Mtu ambaye anakaa kitako na asifanye kitu ana mfanyakazi mmoja, yeye mwenyewe, na mfanyakazi haizalishi au akui. Yeye si mwajiri mzuri way eye mwenyewe, kwa hivyo hatapata nafasi ya kuwaaajiri wengine.

Kwa wakati mwingi na mahali watu hawaajiriwi na wengine. Wanazalisha jambo kwa kubadilisha na lingine, au wanatoa huduma kwa wengine. Hizi ndizo njia Mungu hutupatia.

Kanuni za Maandiko za kuajiri Wakristo

Kanuni ya uwajibikaji na uaminifu hutupa maadili ambayo Wakristo hutumia kazini.

► Mkristo atawezaje kutumia hizi kanuni kazini kwa muajiri wake?

Agano Jipya linatupatia mwelekeo ya wafanyakazi. Wakati ambapo vitabu katika Agano Jipya ziliandikwa wafanyakazi wengi walikuwa watumwa. Mwajiriwa leo anatofauti na mtumwa kiasi kwamba anaweza pata kazi mahali kwingine na aajiriwe. Uhuru huo unawezesha kukubali au kukataa masharti ya ajira. Lakini kama wamekubaliana kufanya kazi pamoja kwa ajili ya manufaa fulani, wanatakiwa na maandiko kuwa watenda kazi wazuri ilimradi tu wabaki na mwajiri wao.

Unaweza kuwa katika hali ambayo haikuruhusu kuchagua kazi utakayo fanya. Labda unalazimishwa kufanya kazi katika mazingira ya kugandamiza. Ni vizuri pia uwe na nia ya mkristo. Watu wengine hufanya kazi kwa upole na vibaya wanapolazimishwa kwa sababu wanataka kuonesha kwamba hawataki kufanya kazi. Mtu akifanya hivyo anaonyesha hana uhuru wa kufanya kazi. Ukitaka kufanya kazi kwa uhuru ni vizuri ufanye kwa furaha na ufanye kazi vizuri. Ukifanya kazi hivyo unafanya ukiwa huru, na hakuna mtu atakulazimisha kufanya hivyo.

Kama hakuna mtu amekuajiri, wewe unajisimamia. Je wewe umekuwa mwajiriwa wa aina gani kwako mwenyewe?

Waefeso 6:5-8 – Kanuni ya majukumu

► Mwanafunzi asome andiko hilo la waefeso 6:5-8 kwa niaba ya kikundi.

► Jadili maana ya kifungu, kisha uangalie maana iliyoorodheshwa na ujumlishe kwa yako.

Baadhi ya mambo ya kufanya katika Waefeso 6:5-8:

1. Mfanyakazi anapaswa kumtii mwajiri wake, si tu anapotazamwa, bali wakati wote. Hiyo pia inamaanisha kwamba hapaswi kupuuza maelezo ambayo labda hayatachunguzwa.
2. Mfanyakazi atahifadhi ubora na uadilifu wa kazi kana kwamba anamfanyia Mungu. ("…kama mtumishi wa Kristo akimfanya mapenzi ya Mungu…").
3. Mfanyakazi atabarikiwa na Mungu kwa uaminifu kazini ("…atapokea sawa kwa Mungu...").

Tito 2:9-10 – Kanuni ya kuwa wa ukweli

► Mwanafunzi atasoma Tito 2:9-10 kwa niaba ya kikundi.

► Jadili maana ya fungu, alafu uangalie orodha ilio hapa chini alafu ujumulishe.

Baadhi ya mambo ya kufanya katika Tito 2:9-10:

1. Mfanyi kazi lazima awe na heshima katika anapoelekezwa na mwajiri wake ("...sio kujibizana..."). Matokeo ni yapi wakati mfanya kazi ana ongea pasipo heshima kumhusu mwajiri wake?
2. Mfanya kazi asimwibie mwajiri wake, ata kau anafikiri angepewa mshara mnono kidogo ("...asiibe...").
3. Kufanya kazi kwa uaminifu ni ushuhuda kwa injili; kutokuwa mwaminifu ni chukizo kwa injili ("...ili wayapambe mafundisho ya Mungu...").

► Ni nini baadhi ya mifano ya njia watu hukosa uaminifu kazini? Eleza jinsi ambavyo Mkristo anastahili kuwa tofauti.

Maandiko katika Tito na Waefeso yanasema kuhusu jinsi ambavyo mtu anastahili kufanya kazi anapoajiriwa. Kanuni sawasawa inafanya kazi kwa mtu ambaye ameajiriwa kurekebisha au kujenga kitu fulani. Lazima afanye kazi bora na ya kupendeza kama vile ambavyo angependa mwingine amfanyie kazi. Mtu anayetengeneza bidhaa za kuuza asifiche madhara kwa mnunuzi akifikiri ili kufanya mnunuzi anunue.

Kukuza ubora unaohitajika kuajiriwa

Ni ubora upi ambao mwajiri anataka mwajiriwa awe nao? Utafiti unaonyesha ya kwamba waajiri wanataka watu ambao wana nia nzuri kwa kazi. Wanataka watu wanaoweza kutumainiwa na wako tayari kujifunza. Watu huajiriwa kwa mtazamo wa nia zao kwa kazi

zaidi ya mafunzo na talanta. Mungu pia anajali mtazamo wetu kwa kazi kama tulivyo ona katika maandiko tayari.

Kuza mbinu ambazo zitakufanya uwe mfanyakazi anaye thaminiwa. Uwe tayari kutumika, uwe mwaminifu, wa kutumainiwa na mwenye subira. Waajiriwa wengine hufikiri kile ambacho wana hitaji pekee. Mwajiri hakuajiri akusaidie, anakuajiri umsaidie. Lazima uwe mtu ambaye ana thamani kwa mwajiri wake.

Mtu anaweza sema, "Nitakuwa rafiki, wa msaada na mwaminifu kama nitalipwa kwa hiyo," lakini mwajiri hataajiri mtu ambaye hana urafiki na amlipe awe rafiki. Mwajiri hataajiri mtu asiye aminika ili amlipe awe mwaminifu. Anatafuta kwa mtu mwenye urafiki, wa msaada na mwaminifu ili wamuajiri.

Kanisani mambo ni tofauti hatuwezi subiri mtu awe na urafiki kabla ya kumsaidia. Pia Mungu anakufikia na ana kubariki kabla hujafanya chochote kizuri. Lakini kwa manufaa yako mwenyewe unatakiwa kuanza kumuelekea kwa neema. Jifunze kujitoa na kutumika na tabasamu.

Kuza ubora wako. Jifunze mbinu kwa kufanya kazi na walio na mbinu hizo. Labda unaweza toa huduma kwa wengine. Au unaweza tengeneza bidhaa za kuuza au unaweza kuza mmea fulani. Zaidi ya yote kuwa na nia ya kusaidia wengine hata kama haileti faida kwako. Mungu atabariki huduma yako.

Ina maanisha nini kutumika? Kutumika ni kutumia uwezo wako, wakati, nguvu kwa manufaa ya mtu mwingine.

Kama au haufanyi kazi ya kuajiriwa, huduma inahitaji uweke kando baadhi ya haki zako na faida. Kwa mfano kama unafanya kazi kwa wengine hautaweza kulala kama utakavyo asubuhi, Na huwezi tumia masaa ya kazi kufanya kile ambacho wewe unataka. Itabidi kuweka pembeni mambo kashaa ya maisha yako kwa sababu ya kazi ambayo umeajiriwa. Ajira huathiri hata jinsi ya kuvaa na jinsi unavyo shiriki na watu wengine.

Kuwa tayari kuhudumu kuna faida nyingi:

1. Inatengeneza uhusiano ambapo mahitaji yako hutimizwa. Mara kwa mara hiii hufanyika kwa njia isiyotarajiwa,sio tu katika hali ya kusaidia watu ukitarajia watafanya kitu kwako.
2. Inakupa hadhi katika kanisa, mwili wa Kristo.
3. Itakufanya uwe mtu ambaye mtu atatamani kukuajiri.

Na kama utakuwa na mtazamo mpya-kutafuta njia ya kuhudumia wengine? Yesu akasema, "Ni Baraka kutoa kuliko kupokea " (Matendo ya Mitume 20:35). Je unaamini hakika hilo? Unaishi kama unavyo amini?

Wafilipi 2:4 inatufundisha kanuni ya kiroho: hatupaswi kuzingatia tu mahitaji yetu wenyewe, lakini tunapaswa kuzingatia mahitaji ya wengine. Pia kuna kanuni ya vitendo.

Kumbuka, wale ambao wanaajiri watu kawaida hawafanyi hivo kusaidia watu walioajiriwa. Wanaajiri watu ambao wanaweza kutana na hitaji walio nalo. Kwa hiyo ikiwa mtu anaweza kufikiria tu kile anachotaka mtu amfanyie, huenda hafai kuajiriwa.

Mambo hufanyika wakati watu wana nia ya kufanya kazi. Faida itaonekana kama muujiza kama umefanyika usipo tarajiwa,lakini Mungu ana njia ya kwaida ya kufanya faida hii katika maisha yako.

Ni kupoteza muda unapotarajia,wazia,au pia kuomba Mungu afanye muujiza kama hauko radhi kufanya kazi ili upokee msaada kwa njia ambayo Mungu anapenda.

Kushiriki kwa vikundi

► Mtu anaweza shiriki tukio jinsi ambavyo kazi nzuri kwa mwajiri ilitoa nafasi kwa injili**.**

► Mtu anaweza shiriki tukio jinsi ambavyo kumsaidia mtu katika maeneo ya jirani ilikuwa ni onyesho zuri kwamba Wakristo hujali.

► Kikundi washiriki pamoja kuhusu nafasi zilizopo kwa mtu ambaye hajaajiriwa**.**

Maombi

Baba wa mbinguni,

Aasnte kwa nafasi ya kufanya kazi kwa ubunifu. Nisaidie nione nafasi ya kusaidia wengine. Kutana na mahitaji yangu ninapofanya kazi ili nishughulikie haja zangu na za wengine.

Nibariki mimi na rasilimali ili niweze kusaidia familia,nitoe kanisani,na nisaidie wengine kwa mahitaji yao.

Nisaidie niwe mwaminifu na wa kutumainiwa kwa majukumu yangu yote. Niandae kwa nafasi kubwa na majukumu kau hayo ni mapenzi yako. Asante kwa kuwa mwaminifu kila wakati kwangu.

Amina

Zoezi la somo la 3

(1) Soma vifungu vifuatavyo katika

- Mithali 6:6-11
- Mithali 10:4-5
- Mithali 12:11, 24, 27
- Mithali 13:4, 11
- Mithali 14:23
- Mithali 18:9
- Mithali 20:13
- Mithali 22:29
- Mithali 24:30-34
- Mithali 26:13-16

Andika kurasa ya mambo ya kufanya kuhusu kazi na uzembe kutokana na aya hizo.

(2) Fanya kazi na mwenzako na muandae uwasilishaji katika mada zinazo orodheshwa hapa chini. (Kiongozi wa darasa atapatia kila kikundi mada ya kuwasilisha.) Shiriki uwasilishaji mwanzo wa darasa lijalo.

- Kazi na sura ya Mungu katika mwanadamu.
- Kazi na majukumu kwa mtu binafsi na wengine.
- Jinsi ambavyo waajiriwa wakristo wanapaswa kufanya kazi. (Wasilisho hili lizingatie Waefeso 6:5-8 na Tito 2:9-10.)
- Jinsi ambavyo Mungu kawaida huhitimiza mahitaji ya watu
- Kazi na ushirika na wengine.

Somo la 4
Mahusiano

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutumia kanuni za upendo, amani na heshima anapohusiana na wengine.

(2) Kukumbatia sheria tisa za kimaandiko zinazowezesha mazungumzo ya mkristo yawabariki wengine na yamtukuze Mungu.

Robinson Crusoe, alishangazwa na uhusiano

Katika hadithi ya kuigiza, *Robinson Crusoe*, Mwanaume aliyenusurika kwa kuogelea mpaka kisiwani meli ilipozama. Hapo alikuwa peke yake kwa miezi. Akajenga kibanda, akatengeneza mavazi, na akajifunza jinsi ya kutafuta chakula. Siku moja alipokuwa akitembea karibu na ufukwe wa bahari alishangaa kuona alama za nyayo za mtu kwenye mchanga. Hii ili maanisha kulikuwa na mtu mwingine pale. Hakujua kama mtu huyu alikuwa rafiki au adui. Hakujua chochote kuhusu tabia, lugha, tabaka au sababu ya mtu huyu kuwa hapo. Hakujua mtu huyu angebadilishaje maisha yake katika kisiwa hiki. Na kwa sababu uhusiano huathiri sana maisha ya mtu binafsi, Robinson alikuwa na tumaini na uoga kwa wakati mmoja alipoona hizo nyayo.

Umuhimu wa mahusiano katika kukua kiroho

Katika karne ya kwanza kanisa ilifanya kazi katika migogoro mbalimbali… Wayahudi na Watu wa Mataifa… madaraja katika jamii… tamaduni… jinsia… Mtume Paulo aka waambia "waweze kupokeana…" (Warumi 15:7).

► Fikiri mtu akiwa peke yake kwenye kisiwa. Anaweza kuwa mvumilivu na yeyote? Anaweza kusamehe yeyote?

Huwezi kukua na kuonyesha subira ya mkristo pasipo kuwa na ushirika na wangine. Hauwezi kusamehe wengine au kusamehewa kama huna ushirikiano na wengine.

► Je ni mambo gani mengine ambayo ni sifa ya mkristo yanayo hitaji watu wengine?

Mambo haya hufanyika katika mahusiano na watu wengine. Tabia njema inaweza kukuzwa na kuonyeshwa katika mahusiano peke yake. Hii inamaanisha mahusiano yetu na watu yanaathiri ukuaji wetu wa kiroho.

Biblia inatupa mwelekeo katika mahusiano mbalimbali. Kuna maelekezo maalum kati ya mke na mume, wazazi kwa watoto, mwajiri na mwajiriwa, wachungaji na makanisa, wazee kwa miaka na walio vijana.

Kuna kanuni tatu katika maandiko ambayo zinahusishwa katika aina yoyote ya mahusiano ya mwanadamu: Kanuni ya amani, upendo na heshima.

Kanuni ya Amani

"Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao." (Waebrania 12:14)

Aya hii inaeleza umuhimu wa uhusiano kwa msisitizo. Utakatifu uko karibu na umeunganishwa na kutafuta amani na watu wote.

► Ni mambo gani tuyafanye ili tutafute amani na watu wote?

Kutafuta amani, angalau umpe kila mtu kile ambacho anastahili. Kwa wale wanaohitaji shukrani, heshima, au utiifu, ni lazima uwape. Kama hutawapa hauna hatia ya kusababisha mtafaruku. Ukikosa kutimiza majukumu yako, ahadi au kulipa wengine, wewe hautafuti amani. Unapotambua umeanguka kwa kutotimiza yale ambayo ilikubidi, inabidi uombe msamaha na utimize majukumu yako kadri uwezavyo.

Lakini kutafuta amani ni zaidi ya kutoa kile ambacho unadaiwa. Inahusisha kuonyesha upendo na utu wema ambao hudaiwi.

► Mwanafunzi asome Tito 3:2-3 kwa niaba ya kikundi.

Lazima tuwe na subira na msamaha, tukielewa kwamba wale ambao hawaja okolewa huwa na nia mbaya na mtazamo mbaya.

Ukitaka amani utatafuta urejesho mahali penye vurugu. Utakuwa tayari kusamehe. Hautakuwa mwepesi kupuuza ya kwamba amani inaweza kurejeshwa. Hautakubali kwa wepesi kutengana katika maisha.

Yesu akasema ni lazima uende kwa aliye kukosea na umweleze kile ambacho alifanya.[7] Kama unaona hilo jambo ni ndogo na halihitaji kukutana, usiwaambie wengine au usiwe na uchungu kwa yule aliye tenda hilo jambo.

Wakati mwingine watu hupambana na kutosawamehe wakristo wenzao waliowakosea. Tunaweza kutarajia kunyanyaswa na watu, ambao hawaja okoka lakini ni vigumu kuelewa wakati mkristo mwingine amekutendea kosa.

Yesu akasema kwamba lazima tuwe tayari kusamehe sabini mara saba.[8] Jambo ambalo hufanya watu kuacha kanisa na kuacha mambo ya kiroho ni uchungu na kuumizwa na wakristo wengine. Uchungu huja kabla ya mapungufu mengine ya kiroho.

Mtu anapokataa kusamehe, anaweka sehemu fulani katika maisha yake kukataa mamlaka ya Mungu, kwa maana Mungu anataka sisi tusamehe. Eneo hilo hufanyika Sehemu ambayo

[7] Mathayo 18:15
[8] Mathayo 18:21-22

shetani ataitumia kuathiri sehemu zingine katika maisha. Kama mtu atakataa kusamehe, hivi karibuni hataweza kushinda majaribu ambayo yanaonekana hayahusiani na hilo kabisa.

Msingi wa kila kosa la kibinafsi ni thamani yetu ya haki zetu binafsi. Kwa sababu tuna amini ya kwamba tuna haki ya kupata heshima fulani, na tunahudhika tusipoipata. Tunaamini tunastahili kilicho bora kuliko kile ambacho tumepata.

Kitu muhimu katika kusamehe wengine ni kuelewa ukombozi. Ukombozi una maanisha kununua tena. Kwa sababu Mungu ametukomboa sisi, sisi ni wake, haki zetu ni zake. Ni lazima tukabidhi haki zetu kwake kwa hiari. Unaweza kuomba, "Bwana najua ya kwamba haki zangu zote ni zako. Nataka uchukue usukani na unipe kile ambacho unaona kinanifaa na ni kizuri kwangu". Halafu, watu wanapokufanyia mazuri, unaweza kumshukuru Mungu kwamba aliwezesha hiyo nafasi kwako. Mtu anapokufanyia mabaya, kumbuka ya kwamba Mungu ndiye mwenye usukani wa haki zako, na aliona utakua vizuri bila kuwa na haki hiyo wakati huo.

Kwa kusamehe wengine, unajitoa kwa Mungu na kufanya yeye akukuze jinsi apendavyo. Kanuni hii ya kuachilia haki zako kwa Mungu inatumika katika kila uhusiano wa mwanadamu. (Nukuu zingine za msamaha zinapatikana Wakolosai 3:13, Mathayo 6:15, na Warumi 12:19.)

Kanuni ya Upendo

Mtu ambaye hatudai chochote tunapaswa kumuonyesha upendo pia. Kwa sababu tulipokea neema, tuna deni kwa Mungu. Hatuwezi kumlipa. Yeye hana mahitaji, lakini ametuagiza tuwape wengine upendo tuliopokea ambao hatukustahili.

"Msiwiwe na mtu chochote, isipokuwa kupendana" (Warumi 13:8).

Upendo ni hakikisho ya kwamba mtu ni mkristo halisi.

"Mtu akisema "Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona" (1 Yohana 4:20).

Kuna upendo maalumu kati ya Wakristo, na Yesu anachukulia kibinafsi matendo yako na nia yako kwa Wakristo wengine. Atasema siku ya hukumu, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi" (Mathayo 25:40).

Lakini upendo wa Wakristo haupaswi kuelekezwa kwa Wakristo wengine tu. Katika Mathayo 5:44-45 Yesu akasema,

> Lakini mimi ninawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.

Watu wengine hupata ugumu kuwa wema kwa wale wanaowaudhi, lakini hakuna sababu ya kuwa katili. Hatuwezi kulipiza ubaya kwa ubaya. Ni vizuri tuwapende watu na tuwe wema

hata kama hawastahili. Tukumbuke kwamba tulipokuwa watenda dhambi, hatukustahili upeno wa Mungu, lakini alitupenda.[9]

Kanuni ya Heshima

► Kama nitakupa bure noti ya dola mia moja ambayo ni chafu na imeraruka, utaichukuwa? Utaikataa kwa sababu ni chafu na imeraruka?

Utaikubali kwa sababu ina thamani ambayo haitegemei hali yake.

Kila mtu anastahili heshima kwa sababu mwanadamu ameumbwa katika sura na Mfano wa Mungu.[10] Sura ya Mungu inampa mtu thamani ambayo ni ya asili.

Hata kama mtu hana elimu, ujuzi, ufundi na kingine chochote ambacho kingemfanya afanikiwe au wa maana katika viwango vya kawaida, ana thamani kwa sababu ni mtu katika sura na Mfano wa Mungu.

Asili ya mtu na thamani yake inabaki vile vile hata kama amejishusha hadhi katika njia zingine na maamuzi ya kipuuzi. Labda aliacha shule, akaharibu afya yake, akaiga tabia mbaya, lakini ana thamani kama mwanadamu aliye na nafsi ya kuishi na sura ya Mungu.

Kwa sababu ya thamani ya Mfano na sura ya MUngu kwa mwanadamu, heshima lazima idumishwe katikati ya wanadamu. Adabu ni kiwango cha chini.

Ghiliba na udanganyifu ni makosa, kwa sababu kila mtu hufanya maamuzi yakiwa na matokeo ya milele na ni lazima ajue kiini hasa cha maamuzi. Kumsababisha mtu kufanya kitu kizuri kwa makusudio mabaya sio ufanisi, kwa sababu bado hajafanya maamuzi mazuri.

Kadri iwezekanavyo ni vizuri tuwape watu heshima hata kama tabia zao ni mbaya. Hata katika kurekebisha na kuadhibu makosa (kwa wale walio na mamlaka sahihi ya kufanya hivyo) yanafanywa kukiwa na ufahamu ya kwamba tunashughulika na viumbe visivyoweza kufa ambavyo vina kitu cha asili cha Mungu.

Kushiriki kwa vikundi

Ni vizuri kuwe na mifano mingi katika kuelezea kanuni hizi.

► Shiriki na uulize mifano ya wakati ambapo mtu alifanya bidii kutafuta amani**.**

► Shiriki na uaombe watu wajitoe ili kusamehe walio wakosea**.**

► Uliza ni katika wakati gani mtu anapaswa kuonyeshwa upendo zaidi hata kama hastahili.

► Eleza inamaanisha nini kumpa mtu heshima hata wakati tabia zake ni mbaya**.**

[9] Tito 3:2-3
[10] Mwanzo 1:17

Kanuni za Kimaandiko kuhusiana na Mazungumzo

► Kuna msemo wa kale unao sema, “kalamu ina nguvu kuliko upanga”. Inamaanisha nini?

Kuna nguvu katika wazo, katika ushawishi na katika mawasiliano. Unaweza kutimiza mengi kwa kutia watu moyo kuliko kuwalazimisha. Wazo—fikra—yaweza kusambaa na kushawishi watu wengi.

Biblia inazungumza kuhusu nguvu za maneno kufanya mazuri au mabaya (Yakobo 3). Mpango wa ukombozi unahitimishwa na nguvu zilizopo katika injili, iliyo kabidhiwa kwa wajumbe ambao ni wanadamu.

Tunawezaje kutumia maneno kutimiza mazuri na kuzuia mabaya? Biblia inatupatia kanuni.

(1) Usizungumze sana.

"Mpumbavu huongeza maneno……" (Mhubiri 10:14).

"Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu; bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili” (Mithali 10:19).

"Hata mpumbavu akinyamaza, huesabiwa hekima, akifumbua midomo yake, huhesabiwa ufahamu" (Mithali 17:28).

Kwa hivyo usizungumze sana. Azungumzae zaidi hayapimi maneno yake au ya wengine. Anayasema mambo ambayo hayamaanishi kabisa, na anadhani kuwa watu wengine wanafanya vivyo hivyo. Hutoa maoni pasipo hekima. Haustahili kutoa maoni kwa kitu ambacho haukijui; sio kila maoni yana umuhimu unaofanana.

(2) Usizungumze kabla ya kufikiria.

Usikubali hisia zako kukufanya utoe matamshi ambayo utayajutia.

“Hayo mnajua ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika” (Yakobo 1:19).

"Mpumbavu hudhihirisha hasira yake yote; bali mwenye hekima huizuia na kuituliza" (Mithali 29:11).

"Asiye mwepesi wa hasira ana fahamu nyingi; bali mwenye roho ya hamaki hutukuza upumbavu" (Mithali 14:29).

(3) Usihukumu hali katika mtazamo wa kwanza.

"Yeye ajibuye kabla hajasikia ni upumbavu na aibu kwake " (Mithali 18:13).

"Ajiteteaye kwanza huonekana kuwa ana haki; lakini jirani yake huja na kumchunguza " (Mithali 18:17).

Michafuko mengi hutokana na kutoelewa. Subira na kwa kuchunguza huleta suluhu. Kama mtu aliye na haki inayojulikana akisema jambo ambalo haliko sawa kwako usiwe mwepesi wa kuhukumu.

"Mtu apitaye na kujisumbua kwa ugomvi usio wake; ni kama mtu ashikaye mbwa kwa masikio yake" (Mithali 26:17).

(4) Kuwa mwangalifu wa mzaha.

Kwa sababu ya kile ambacho maneno yanaweza kusababisha, mazaha usio zuilika ni silaha mikononi mwa mwendawazimu.

"Kama mtu mwenye wazimu atupaye miyenge,na mishale, na mauti; ndivyo alivo amdanganyaye mwenzake, na kusema, je! Sikufanya mzaha tu?" (Mithali 26:18-19).

Usufanye watu wafanye makosa kwa sababu ya kuamini mzaha wako. Usiwaambie kwamba unamaanisha wakati haumaanishi-hawatakuamini tena. Usifanye mzaha kwa kasoro ambazo watu hawawezi kujizuia. Usifanye mzaha kwa mapungufu ya mwingine. Usifanye mzaha ambao utafanya dhambi kuwa kitu kidogo.

► Ni matumizi gani mengine mabaya ya mzaha?

(5) Usiseme kwa asiye faa.

"Mwenye kitango akisingizia ufunuo wa siri bali mwenye roho ya uaminifu husitiri mambo" (Mithali 11:13).

"Moto hufa kwa kukosa kuni; na bila mchongezi fitina hukoma " (Mithali 26:20).

Kuna mambo lazima yasemwe, lakini inawezekana sio wewe unayestahili kuyasema. Hauwezi kuyasema kwa niaba ya wale walio na mamlaka ya kuyasema.

Usieneze maneno ya makosa ya watu wengine.

Watu hawatakuamini kwa taarifa zao za kibinafsi, kama watafikiri utawaambia wengine.

"Ujitetee na mwenzako peke yake; bali usifunue siri ya mtu mwingine" (Mithali 25:9).

Mpumbavu hueleza tatizo kwa watu wasio sahihi badala ya kufuata utaratibu katika Mathayo 18:15-17.

(6) Kuwa mwangalifu Unapokosoa.

Kuna wakati unaofaa na njia sahihi ya kukosoa.

"lawama ya wazi ni heri kuliko upendo uliositirika. Jeraha utiwazo na rafiki ni amini…" (Mithali 27:5-6a).

Hakikisha ya kwamba kukosoa kwako kuna lenga kujenga sio kubomoa. Lazima uonyshe unajali na unataka kusaidia. Kawaida uhusiano bora ni muhimu kabla ya msaada wako wa kukosoa.

(7) Usidanganye.

"Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale,pamoja na matendo yake" (Wakolosai 3:9).

Udanganyifu huambatana na maisha ya dhambi, sio maisha ya Kikristo.

"Midomo ya uongo ni chukizo kwa Bwana; bali watendao uaminifu ndio furaha yake" (Mithali 12:22).

(8) Weka maneno yako safi.

"...Wala aibu wala maneno ya upuzi wala ubishi; hayo hayapendezi; bali afadhali kushukuru. " (Waefeso 5:4).

Usieleze kuhusu kashfa zilizopita au za sasa isipokuwa tu kwa wakati unaofaa kushughulikia hali fulani. Usiseme utani ambao lazima uuseme kwa siri. Watu mara kwa mara hutumia maneno ya kingono au maneno za sehemu za siri katika mshangao wao, lakini hiyo haifai kwa mkristo. Haifai kutumia maneno yanayo mwelekea Mungu au Yesu kama mshangao wakati wa shida, kama sio kumuita Mungu kwa usaidizi.

(9) Usigawanye watu kwa maneno yako.

"Mtu mshupavu huondokesha fitina na mchongezi huwafarakanisha rafiki" (Mithali 16:28).

"Kuna vitu sita anavyovichukia Bwana; Naam, vitu saba vilivyo chukizo kwake… [ya saba] Naye apandaye mbegu ya fitina kati ya ndugu ... " (Mithali 6:16, 19).

Usijaribu kujifanya kuwa bora kwa kumfanya mtu mwingine aonekane duni. Usifanye vurugu kati ya wengine. Usiharibu huduma ya mwingine kwa fitina.

Kabla ya kuongea jiulize "ni ya ukweli?" pia "kwa nini niseme? "

Hitimisho

Mkristo awe tayari kuomba msamaha anapotambua ana makosa aliyoyafanya kupitia maneno yake. Awe tayari kurekebisha yale aliyo yasema ambayo sio sawa.

Maneno ya kuudhi kutoka kwa wengine haimaanishi wewe ulipize kwa maneno ya kuudhi pia.

Kuna makosa katika misemo yako ambayo unaweza kuyarekebisha pole pole. Kwa mfano, unaweza jifunza kuwaza hilo jambo kabla hujalisema. Kuna makosa megine ambayo huonyesha shida ya moyo, kama vile kutaka kuumiza mtu kwa maneno. Kama unajihukumu

kwa shida kama hiyo ya matamshi, unapaswa kumuomba Mungu akusamehe na asafishe moyo wako kutokana na mazoea hayo.

Maneno yako huonyesha yaliyo moyoni mwako. Usiharibu ushuhuda wako kwa kuyanena yale ambayo sio sawa kwa maisha ya Mkristo.

Maneno yako yanaweza kubariki walio karibu nawe. Huduma nyingi huhusisha mawasiliano. Maana ya maneno yako huwa ya maana zaidi unapozingatia na kufuata kanuni za Biblia.

Kushiriki kwa vikundi

► Watu wengi huona makosa ya wengine katika maneno lakini sio yao wenyewe. Kiongozi lazima awe mfano wakati ambapo yeye mwenyewe ameshindwa kuwa mfano mzuri kwa kushindwa kufuata kanuni za Biblia au aeleze mojawapo ya udhaifu wake.

► Omba washiriki wachague kanuni ambazo ni wadhaifu kwazo na wamwamini Mungu atawasaidia.

Maombi

Baba wa mbinguni,

Nisaidie niishi kulingana na kanuni za kimaandiko za amani, upendo, na heshima kwa mahusiano yangu yote.

Nataka nisamehe walionikosea mimi. Nisaidie kutafuta urejesho kwa wale ambao tumekuwa na kutoelewana.

Nisaidie kuheshimu kila mtu kama kiumbe katika sura na mfano wako. Nisaidie kukumbuka matokeo ambayo mazungumzo yangu yanaweza kuwa nayo, na niwajibike kwa maneno yangu. Nataka maneno yangu yatimize mazuri sio mabaya.

Nataka ushuhuda wangu kwako uheshimiwe.

Asante kwa nafasi ya kueleza kushiriki ukweli wako.

Amina.

Zoezi la somo la 4

(1) Soma Yakobo 3. Ona uwezo mkubwa wa mazungumzo ulioelezwa hapa. Katika mstari 13-18 ona jinsi ambavyo usemi wake unavyotiririka kiasili kutoka katika hali ya kiroho ya mtu. Soma Waefeso 4:25-32. Andika aya ya ombi kutokana na andiko hili.

(2) Soma Waefeso 5:22–6:9. Orodhesha na ueleze mambo mahususi ya tabia katika mahusiano mbali mbali. Andika na ueleze jinsi ambavyo maelekezo haya yanahusiana na kanuni ya upendo,amani,na heshima kama tulivo jadili.

(3) Chukua matatu kati ya maswali yafuatayo. Andika aya huku ukijibu kila mmoja wapo:

- Ni mambo gani hasa Mungu ametuitia kuyafanya katika hali ya kutafuta amani katika mahusiano yetu?
- Kwa nini kusamehe wengine ni muhimu ili kudumisha wokovu?
- Inamaanisha nini mtu kumpa Mungu haki zake?
- Ni msukumo upi tulio nao wa upendo ambao tunastahili kuwapa wengine wasio stahili?
- Ni kwa namna gani mtu kuumbwa katika sura ya Mungu inathiri uhusiano wetu na wengine?

Somo la 5
Kuongozwa na Mungu

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuelewa jinsi ambavyo Mungu anatusaidia kufanya maamuzi.

(2) Kujua jinsi ya kuwa tayari kutambua mapenzi ya Mungu na kufanya maamuzi sahihi.

(3) Kuepuka makosa unapotafuta maelekezo.

Sunami Palu, Kosa la Mawasiliano

Mwezi wa Septemba 2018, tetemeko kubwa la ardhi chini ya kisiwa ilisababisha sunami (wimbi kubwa) kuelekea jiji la Palu, Indonesia. Mwanaume aliyekuwa juu ya jengo refu aliona wimbi likija. Kwa sauti kubwa akawaonya watu waliokuwa kwenye mitaa chini ya jengo, lakini wengi wao wakampuuza. Zaidi ya watu 4,000 walifariki, na watu 10,000 wakajeruhiwa.

Miaka kumi kabla (2008), serikali iliweka maboya 22 ya kuelea ambayo ilikuwa na teknolojia ya kielectroniki ili kuonya watu endapo sunami inakuja. Hata hivyo, baada ya miaka michache kupita maboya yale yaliharibika na hayakufanya kazi tena. Hakuna hata boya moja lililotoa tahadhari wakati wa sunami mwaka 2018.

Mawasiliano na Komanda wetu

► Ni nini ambacho huwekwa katika kila gari la jeshi?

Kila kifaru, gari, ndege n.k ina redio. Sio kwa ajili ya wanajeshi kusikiliza muziki jinsi wapendayo, lakini ni redio ya mawasiliano.

Mawasiliano ni ya muhimu ili kushinda vita. Wanajeshi akiwa vitani hawawezi kuona uwanja wote wa vita. Hawawezi kujua mahali ambapo rafiki zake wapo na mahali palipo na adui. Hawawezi kujua mwelekeo wanaopaswa kupiga risasi na hawatajua waelekee upande upi, bila mawasiliano kutoka kwa Komanda.

Kumekuwa na kesi nyingi, ambapo wanajeshi wameuliwa na wenzao katika mazoezi, wakati ambapo risasi imefyatuliwa pasipo maelekezo. Kumekuwa na wakati ambapo makombora na mabomu yameshambulia marafiki na sio maadui kwa sababu ya mawasiliano mabaya.

Katika vita vya kisasa ni bayana ya kwamba kila mmoja hujaribu kushambuli jumba la mawasiliano la maadui zake. Upande ambao utafanikiwa kuna uwezekano utashinda adui.

Tuko katika vita vya kiroho. Shetani hujaribu kutudanganya. Dunia inajaribu kutuvuta katika mitindo ya kimaisha. Watu wanao tuzunguka wakati mwingine wanatuzuia, wanatuvunja moyo sisi kuishi kwa kufuata mapenzi ya Mungu. Sisi ni kama wanajeshi walio katika nchi katili, tukiwa tu na marafiki wachache na maadui wengi.

Mungu anapenda tushinde vita vya kiroho. Maombi ndio njia ya kuwasiliana na Komanda.

Hebu fikiria askari katika vita ambaye aliamua kupuuza amri za komado na kwenda mwenyewe. Huenda akafanya madhara badala ya wema; anaweza kushindwa kuwasaidia watu wanaomtegemea; na pengine anaweza kuuawa au kutekwa.

"Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa kila jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote" (Waefeso 6:18).

Aya hii inakuja mwisho wa kifungu pale ambapo Paulo anaonyesha Wakristo silaha za kiroho kwa kilinganisha na silaha za kijeshi za wakati ule. Anasema adui zetu sio wa kimwili ni wa Kiroho.

Labda kama redio zingekuwapo wakati wa Paulo, angezitumia kuonyesha silaha nyingine katika vita vya Kiroho kwa jeshi la kiroho-maombi. Baada ya kueleza silaha Paulo akasema kwamba maombi yanatumiwa sambamba na silaha za Kiroho.

Tunaposimama katika vita kinyume na roho chafu, lazima tuwe tunaomba, tudumu katika mawasiliano na Komanda wetu. Tumeitwa kuwa wenye ushujaa katika maombi, tuwe waangalifu na wavumilivu.

Mungu ameahidi kuongoza wale ambao watamsikiliza.

"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri Yeye naye Atanyosha mapito yako" (Mithali 3:5-6).

"Hatua za mtu zaimarishwa na Bwana" (Zaburi 37:23).

Mkristo hafanyi maamuzi sawa na jinsi ambavyo dunia hufanya. Watu wengine huongozwa na matakwa na tamaa zao. Wanasema, “Nitafanya kile ambacho ni kizuri kwangu”. Wanamaanisha kwamba lazima wazingatie mapenzi yao kuliko kuruhusu wengine wawaongoze. Wanafikiri uhuru unamaanisha ubinafsi. Mkristo ni tofauti kwa sababu anataka kumpendeza Mungu na kuwabariki wengine kwa maisha yake.

Baadhi ya watu hutushauri tusikilize ndani yetu ili kupata majibu. Wana amini kwamba hisia na akili zatosha kwa kuwaongoza kufanya maamuzi. Wanahimiza vijana kupuuza tamaduni na mahusia ya wazee. Wanapuuza utamaawa wa dini. Aina hii ya ushauri ni maarufu sana katika burudani ya Hollywood ya kisasa. Wanaonyesha au kuelezea vijana wanaofanikiwa kutokana na kuasi amri na tamaduni na kufuata ndoto zao binafsi. Hawaonyeshi ukweli kwamba maamuzi hayo huelekeza kwenye huzuni na janga kuu.

Katika tamaduni zingine, uamuzi wa mtu binafsi hidhibitiwa na ukoo au kabila. Mtu binafsi haruhusiwi kuondoka mkoani kwake, kubadilisha kazi, kuendelea na masomo au kuoa kabla hajathibitishwa na kikundi. Jambo gumu kabida katika mazingira haya ni kubadilisha dini. Endapo mtu atakuwa Mkristo na anaongozwa na kanuni ambazo watu wake hawazielewi anaweza kuteswa na kuumia. Mkristo katika hali hiyo lazima aombe ili kupata hekima na maongozi ya kimungu.

Tunahitaji kuongozwa na Mungu wakati wote, na anatuongoza kwa njia ambazo wakati mwingine hatuzijui. Yeye hawezi kutusahau kamwe, hata wakati ambapo hatumfikirii. Lakini kuna wakati ambao tunapaswa kutafuta njia zake na kuelekezwa na yeye na tumuombe atusaidie kuona chaguzi jinsi zilivyo. Mungu angetaka kubadilisha mwelekeo wetu kwa njia ambayo hatutarajii.

► Ni nyakati zipi ambazo tunahitaji mwelekeo maalumu kutoka kwa Mungu?

Tunastahili kutafuta mwongozo kutoka kwa Mungu…

1. **Wakati tunafanya maamuzi yatakayo badilisha maisha:** Ndoa, kazi, elimu, majukumu ya Kanisa**.**
2. **Wakati wa maamuzi mahususi**: Nafasi ya kazi, mahali pa kuishi, manunuzi ya hali ya juu.
3. **Wakati unapanga kufanya huduma**:[11] Mwito wa mtu binafsi, wapi na utahudumia nani, jambo la kuhubiri na kufundisha.
4. **Wakati tunaoshiriki katika maisha ya kanisa:**[12] Jinsi ya kuabudu, nini ya kujifunza, utatoa nini, jinsi ya kuwa sehemu ya mwili wa Kristo duniani.

Jinsi unavyo tambua vizuri uongozi wa Mungu

(1) Mkaribie Mungu kwa maombi. Kama muda mwingi wa maisha yako utatenganishwa na mawasiliano na Mungu, wewe unafuata akili zako na mawazo yako mwenyewe.

(2) Usitumaini akili yako kuliko kweli kweli iliyo katika maandiko. Kama vile maandiko yanavyosema hapo juu,"...Usitumainie akili zako mwenyewe " (Mithali 3:5).

(3) Wakati wote tii kile ambacho unajua ukweli kuwa ni mapenzi ya Mungu. Hiyo itaboresha mtazamo wako. Mtu ambaye hatii neno la Mungu maana yake hataki mapenzi ya Mungu kwa sababu Mungu anaeleza mapenzi yake katika maandiko. Ukitii tu sehemu ya neno la Mungu utachanganyikiwa sana-na mwangaza utabadilika kuwa giza (Luka 11:35).

[11] Matendo Ya Mitume 16:6-9 yaeleza jinsi ambavyo ushauri spesheli ambao Roho mtakatifu alimpa Paulo na Sila katika safari yao ya misionari ..

[12] Kanisa la kale walikuwa nyeti kwa Roho mtakatifu alipoelekeza ibada, kulinda Imani yao, walivyoongozwa kutatua shida, na pia kupa nguvu ujumbe wao. Ona Matendo Ya Mitume 15:28, 5:3-5, na 6:10.

Tunajua ya kwamba ni mapenzi ya Mungu sisi:

- Kujitwika msalaba wetu kila siku na kumfuata Yesu. (Luka 9:23).
- Kufanya haki na Kusema ukweli kutoka moyoni. (Zaburi 15:2).
- Kuheshimu viongozi waaminifu wa Kiroho. (1 Wathesalonike 5:12-13).
- Kufurahi kila wakati. (1 Wathesalonike 5:16).
- Kuomba bila kukoma. (1 Wathesalonike 5:17).
- Kushukuru katika hali zote. (1 Wathesalonike 5:18).
- Kutomhuzunisha Roho. (1 Wathesalonike 5:19).
- Kutopuuza unabii. (1 Wathesalonike 5:20).
- Kujaribu mambo yote. (1 Wathesalonike 5:21).
- Kushika sana kilicho kizuri. (1 Wathesalonike 5:21).
- Kukimbia maovu. (1 Wathesalonike 5:22).
- Kutakaswa kweli kweli. (1 Wathesalonike 5:23).

Na kuna amri zingine ambazo zimefupishwa kwa neno moja: Upendo! (Warumi 13:8-10). Tunapofanya yale ambayo tunajua ni mapenzi ya Mungu, mengi ya maamuzi ya maisha yasiyo na uzito yatafanya kazi tu.

(4) Kuwa na subira. Itakubidi usubiri kwa muda wakati Mungu anafungua milango na kuandaa Mazingira kwa ajili yako. Usifanye maamuzi kwa haraka kwa sababu ya kukosa subira. "Ukae kimya mbele za Bwana nawe umngojee kwa saburi" (Zaburi 37:7). Usifanye kitu unachojua ni kibaya kwa sababu ya dharura.

(5) Sikiliza ushauri mzuri "Maana kwa mashauri ya akili utafanya vita na kwa wingi wa washauri huja wokovu" (Mithali 24:6). Wakati Mungu anakutaka kufanya uamuzi mkubwa, ataonyesha hilo kwa watu wengine katika maisha yako. Kama kuna watu wa Mungu, watu wazima ambao wanampenda Mungu na wanakupenda, usiwe mwepesi wa kufanya kitu ambacho watafikiri ni makosa.

Kushiriki kwa vikundi

► Shiriki mfano wa jambo ambao unajua aliongozwa na Mungu. Mungu alikueleza kwa namna gani kwamba ni maamuzi sahihi?

► Itakuwa vyema pia ukishirikisha mfano wa maamuzi mabaya. Ulikosa kufuata mmojawapo ya kanuni nne ya jinsi ya kuongozwa na mungu?

Ruhusu wendine washiriki pia.

► Labda kuna mmoja ambaye anajaribu kufanya uamuzi ambaye angetaka kushirikisha**.**

Makosa ya kuepuka unapotafuta Uongozi wa Mungu

Hadithi inasimuliwa kwamba mhubiri mmoja aliyeitwa Charles Stalker alikuwa akiomba asubuhi moja wakati Mungu alipomwambia, "nataka uende China." Stalker alishangaa kwa sababu hakuwa na fedha za nauli wala mtu aliyemfahamu huko uchina. Msukumo ndani

yake ulikuwa mkubwa kiasi ya kwamba alibeba vitu vyake na akaelekea kwenye stesheni mahali ambapo safari ya namna hiyo ilikuwa ianzie. Hapo mtu ambaye hawakufahamiana akaja na kumuuliza, "wewe ni Charles Stalker?" naye akaendelea akasema , "nilitumwa hapa na tiketi yako ya kwenda China."

► Je ni namna hii ambayo tunatarajia Mungu atuonyeshe mapenzi yake? Je kutakuwa na shida kwa mtu atakaye mtarajia Mungu aoneshe mapenzi yake kwa namna hii?

Watu wengine hungoja miujiza na ufunuo ili wajue mapenzi ya Mungu katika kila hatua wanayoichukua katika maisha. Wanapuuza kufikiri na mazingira, kwasababu wanafikiri mapenzi ya Mungu yanaweza kuwa kinyume na mawazo yote na mazingira.

Ni makosa kusititiza kwamba Mungu lazima afanye muujiza kwa maamuzi yetu kwa sababu mara kwa mara hataonyesha mapenzi yake kwa njia hizo. Endapo mtu atapuuza kufikiria na mazingira anaweza kufikiri anapata maongozi kutoka kwa Mungu na kumbe anafuata hisia zake.

Wakati ambapo jambo au kitu kimekubaliwa au kukataliwa na maandiko, tunajua mapenzi ya Mungu. Lakini, kuna maamuzi mengi ambayo tuna njia mbadala ambazo hazijakubaliwa wala kukataliwa na Mungu. Mtu atajuaje mahali atakapoishi, atafanya kazi aina gani, na atatumia fedha kwa njia gani?

► Bila ufunuo maalumu, mtu atajuaje mapenzi ya Mungu kwa maamuzi ambayo hayajaelekezwa haswa kwa maandiko?

Watu wengine kwa sababu ya kuamini ya kwamba maelekezo ya Mungu lazima yawe na miujiza pasipo kufikiria na kuzingatia mazingira, wanapata njia ambazo sio za kimantiki na hufikiri Mungu atatumia hizo njia kuwapa mwelekeo. Wanaweza kumwambia Mungu awape hakikisho fulani ili kuthibitisha atafanya jambo fulani na kwamba huo ni mwongozo wake. Au wanaweza fungua Biblia kurasa yoyote na kutumia mstari fulani kusuluhisha jambo fulani.

Mashauri zaidi ya kufanya maamuzi mazuri

John Wesley anazungumza mambo mahususi ya jinsi ya kujua mapenzi ya Mungu. Alisema kwamba tunajua mapenzi ya jumla ya Mungu, kama yalivyo katika Biblia ni kwamba tuwe watakatifu na tutimize yale mazuri. **Kwa hivyo ili kufanya uamuzi fulani ni lazima tuzingatie ni uchaguzi upi utafanya tuwe watakatifu na tukamilishe yalio bora zaidi.**

Tunajifunza katika uzoefu ambapo tunatofautisha ni hali gani ni ya msaada kiroho na ipi hatari. Hali zingine ni hatari kiroho kwa wote, na zingine ni hatari kwa wachache na sio wote. Kwa kadiri iwezekanavyo tujiweke katika hali ambazo zitatukuza kiroho na tuepuke zile ambayo zitatuelekeza majaribuni (1 Wakorintho 10:12-13).

Kwa fikira na uzoefu, na kwa mashauri kutoka kwa wengine, tunaweza kupambanua ni uamuzi upi utaturuhusu kukamilisha mengi mazuri.

Sio kila Mungu wakati atajionyesha kwa miujiza. **Anatarajia sisi tuweze kutumia kanuni za kimaandiko huku tukifikiri na kuangalia kwa maakini mazingira**. Roho mtakatifu atatuongoza hata wakati mwingine pasipo hata sisi kufahamu. Kwa maamuzi mengi tusitarajie ufunuo lakini tuombe hekima na uelewa.

Watu ambao hudai mwongozo maalumu kutoka kwa Mungu, wakati mwingine hawawezi kuwasikiliza watu. (Mithali 12:15). Wanaweza kukasirika wakati watu wanapowauliza maswali kuhusu uamuzi wao. Wanaonyesha kiburi na usumbufu badala ya unyenyekevu.

► Mwanafunzi asome 1 Petro 5:5-6 kwa niaba ya kikundi.

Isipokuwa katika hali chache, ni vizuri mtu asiseme Mungu amemwambia hasa la kufanya. Mtu akisema hivyo, ni vigumu kwa mtu yeyote kumpamahusia na ushauri. Itakuwa afadhali aseme anajaribu kufanya uamuzi wa busara na kwa msaada wa Mungu.

Kando na kanuni za Wesley alizotoa, unapopeana maoni yako zingatia

1. **Je iko sambamba na amri zilizo wazi za kimaandiko?** Mungu hataki ukose kutii Neno lake.
2. **Je iko sambamba na vipaumbele katika maandiko?** Biblia inaonyesha mambo ambayo ni muhimu kwa Mungu. Je maamuzi yako yanazingatia hayo?
3. **Je inaambatana na mtazamo halisi wa mazingira?** Unatakiwa kuona jinsi ambavyo Mungu amekuwa akikuandaa katika Mazingira hayo na uamuzi huo**.**
4. **Linaleta maana?** Wakati mwingine Mungu atakuelekeza kufanya jambo ambalo ni kama halina maana, lakini atafanya mapenzi yake kuwa wazi. Usikatae kamwe sababu kama njia ya kukusaidia kutambua mapenzi ya Mungu.
5. **Je ni tabia ya kikristo?** Usifikiri kuwa jambo kila hali si ya kawaida sana kiasi kwamba unaweza kufanya jambo ambalo halitampendeza Mungu**.**
6. **Inaambatana na kuwapenda wengine kama unavyojipenda?** Nia ya ubinafsi itaharibu kupambanua kwako**.**
7. **Je itakuwa na ushawishi mzuri?** Na wengine wakifanya jinsi ambavyo unafanya? Je, itakuwa vizuri kweli?
8. **Je imethibitishwa na washauri wa kimungu?** Sisi wote twajua jinsi ya kutafuta mafiki ambao watakubaliana nasi lakini watu ambao ni wa kiroho watasemaje kulingana na maamuzi yako?

Wakati mapenzi ya Mungu yanapokuwa sio ya kawaida, atafanya uelewe bila mashaka yoyote. Malaika, maono, au kichaka kiwakacho moto kiliwapa watu wa zamani uhakika ya kwamba ni Mungu. Mungu anaweza pia kukupa hakikisho la ndani ya moyo ambalo halina mashaka. Lakini wakati hakuna ujumbe wazi kutoka kwa Mungu ni vizuri ufuate kanuni zinazo tumainiwa ili ufanye uamuzi mzuri. Usitarajie kupata ufunuo maalum kwa kila jambo.

Endapo utatumia utashi waho vizuri katika maombi na unyoofu na kuwa na vipaumbele sahihi, Mungu atakuwa mwaminifu kuongoza maamuzi wako.

Katika Warumi 12:1-2 Paulo aliandika,

> Basi ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu yakumpendeza Mungu, ndiyo ibaada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema,ya kumpendeza, na ukamilifu.

Aya hii inaonyesha hali ya mtu ya Kiroho inavyo athirika katika maamuzi. Ili kupata mapenzi ya Mungu, lazima mtu ajitoe kikamilifu kwa Mungu. Maamuzi ya Mkristo ni tofauti na maamuzi ya dunia, kwa sababu hajafuatisha namna ya dunia hii lakini amefanywa upya nia yake. Anafanya maamuzi kwa nia mpya.

Nia ni kiungo cha maana sana katika kutambua Uongozi wa Mungu. Mtu atafutaye mapenzi ya Mungu ili tu aamue nini afanye au asifanye hakika atachanganyikiwa. Kama mtu atatafuta mapenzi ya Mungu kulingana na maandiko na pia kwa kufikiri, na kwa moyo wake wote ameamua kufanya, hakika hatakosa mapenzi ya Mungu.

Kushiriki kwa vikundi

► Jadili baadhi ya matumizi ya kanuni za Wesley's. Mifano mingine inaweza kuwa ni kuchagua marafiki ambao wewe utatumia muda wako pamoja nao, kuchagua ajira, kuamua mwenzi wa ndoa. Chagua, *"ni hali ipi ambayo itanisaidia kuendelea kuwa mtakatifu na kutimiza yaliyo mazuri zaidi?"*

► Watu wengine huonekana kwamba hawawezi kudumisha Ukristo wao wanapokuwa na watu fulani, au mahali fulani. Fikiria mifano.

► Uwezekano wa mjadala zaidi ni:

- Jukumu la motisha katika kufanya uamuzi.
- Kosa la kungojea ishara.
- Hatari iliyopo kwa kutegemea hisia sana.

Maombi

Baba wa mbinguni,

Asante kwa kunipangia mambo mazuri. Najua ya kwamba unaongoza hatua zangu zaidi ya nionavyo.

Nisaidie kukukaribia kwa maombi. Nisaidie kuwa makini na kweli ambayo unanionyesha.

Nataka niwe mtakatifu na nifanikishe mengi iwezekanavyo kwa utukufu wako.

Fanya nia yangu iwe safi ili kwamba isinielekeze mbali na mapenzi yako. Niongoze kwa kuwatumia washauri wenye hekima ambao umeweka maishani mwangu.

Nataka nikuamini katika kila uamuzi wangu. Nataka nikufuate kwa moyo wote na kwa kukutii.

Asante kwa kunitakia mema.

Amina.

Zoezi la Somo la 5

(1) Soma Mithali 3:1-12. Andika kuhusu vipaumbele, nia ,mtazamo na tabia ambazo zimeelezwa hapa. Eleza jinsi ambavyo wewe binafsi unaweza kukuza tabia hizi. (majibu yote yaandikwe karika kurasa 1-2.)

(2) Chunguza Yakobo 4:13-17. Tambua ukuu wa Mungu dhidi ya hali. Ni uovu upi - usiopendeza ambao unaoneshwa katika mstari wa 16. Andika aya ukieleza kuhusu unavyo pangilia maisha yako yajayo.

(3) Andika aya mbili ukieleza uhusiano uliopo katika maombi na kufanya maamuzi. Jibu maswali yafuatayo

- Ni kwa namna gani maombi yanaathiri maamuzi yetu?
- Makosa gani uyazuie ambayo yanahusiana na maombi na kufanya maamuzi?

Somo la 6
Mtazamo wa Biblia kuhusu Ndoa

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kukumbatia ubunifu na kusudi la Mungu katika ndoa.

(2) Kuelewa thamani ya wanawake kwa mtazamo wa Mungu.

(3) Kujitoa binafsi kwa kanuni za Mungu katika ndoa ya kikristo.

Hernando Cortes: Mtu aliye jikita kikamilifu

Hernando Cortes sio mfano mzuri ambao tunaweza kuuiga katika tabia na makusudio. Hata hivyo tendo lake moja linaonesha kujikita kikamilifu kwa malengo yake. Wakati wamjira ya baridi ya mwaka 1519, Hernando Cortes aliongoza kundi ili kuuteka nyara mji ambao sasa unaitwa Mexico. Serikali ya Uhispania ilifadhili misheni hiyo kwa kuwapa meli kumi na moja na wanaume mia saba. Baada ya miezi kadhaa katika bahari Cortes na wanaume wake walifika katika fukwe za Mexico. Changamoto iliyo fuata ilikuwa ni kuvuka miji hadi jiji kuu. Cortes alijua kwamba kutembea katika nchi kavu ilikuwa ngumu na hatari. Alitaka wanaume wake wajue ya kwamba kurudi nyuma isingewezekana kamwe kwa hivyo akachoma moto meli zote. Akafanya njia ya kurudi Uhispania kutowezekana na wakati huo huo akawapa wale wanaume hamasa kubwa ya kufaulu. Vivyo hivyo, kila mtu anayeingia katika ndoa lazima ajue ya kwamba hakuna kurudi nyuma.

Utangulizi

Ndoa ya kimaandiko ni nzuri sana.[13] Lakini wapendanao wakitaka kupata uzuri na kufurahia wema wake lazima wayachunguze maandiko jinsi yanavyosema kuhusu ndoa,na kufuata na kutii walichojifunza. Ndoa ambayo yatosheleza yahitaji kujitoa na bidiii kubwa.

Ili uweze kuielewa ndoa tunatakiwa kurudi mwanzo katika hadithi ya uumbaji. Habari ya uumbaji itatufundisha kuhusiana na ndoa.

► Je kuna mtu anaweza kutushirikisha kuhusiana na jinsi ambavo aliingia katika ndoa akitarajia faida bila kujua ya kwamba kujitoa ni kwa muhimu?

[13] Somo liliandikwa na Tim Keep.

Ndoa ya Kibiblia

(1) Ndoa ya Kibiblia ni kwa ajili ya Ushirika.

"Bwana Mungu aksema si vyema mtu huyu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye" (Mwanzo 2:18).

Kama jins ambavyo Mungu ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu walivyo katika ushirika, Mungu alituumba sisi tuwe wa ushirika. Tuliumbwa tuwasiliane. Tuliumbwa kwa ajili ya urafiki wa karibu na ushirika. Mungu akasaema kuwa pekee sio nzuri!

Kila sehemu ya mwanzo inaonyesha kwamba Mungu aliipa heshima ndoa. Mungu alichukua ubavu kutoka kwa mwanaume na akamfanyia mwenzake mrembo, na "akaletwa kwa heshima kwa mwanaume kama kazi iliyo bora zaidi ya mwisho ya Muumbaji. Kila hatua na kiwango katika maelezo inakusudia kuwezesha ndoa."[14] "Neno ("akamletea") linaonesha kukabidhiwa kwake katika vifungo vya agano la ndoa, ambalo linaitwa agano la Mungu (Mithali 2:17)."[15]

Ndoa inapaswa kuwa ya umoja ulio na furaha.

Wakati Adamu aliposema, "Huyu sasa ni mfupa katika mifupa yangu…" (2:23) alikuwa anaonyesha heshima na furaha. Adamu hakusema "mwishowe, nimepata mtumwa! Nimepata mtu wa kunifulia, kunipikia chakula, kunikanda mgongo na kufanya kazi zanguza nyumbani!". Hapana, Adamu alisema "hatimaye nimepata anaye fanana na mimi!"

Ndoa inapaswa kuwa ya Umoja wa Usawa.

"...Msaidizi wa kufanana nami (mwenzangu mkamilifu)" (2:18).

Matthew Henry anatukumbusha sisi, "Mwanamke aliumbwa kutokana na ubavu wa Adamu; siyo kutoka kichwani amtawale, siyo kutoka miguuni, ili amkanyage, bali kutoka ubavuni mwake ili awe sawa na yeye, chini ya mkono wake kulindwa, na karibu na moyo wake kupendwa."[16] Mwanamke hakuwa duni wala bora kuliko mwanamume, lakini alilinganishwa naye.

Ndoa ni umoja wa Agano.

"Kwa hivyo mwanaume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja" (2:24). Ndoa zilizo simama imara hazitegemei hisia za mapenzi au mahaba, (hisia za mapenzi huja na huondoka) au raha (ijapokuwa ndoa iliyo na afya huleta furaha), au kutosheka kwa mtu (ingawa ndoa zenye nguvu zinztosheleza). Faida zilizozopo katika ndoa hazisababishi ndoa kuwa imara; bali zinatokana na ndoa

[14] *Ellicot's Commentary for English Readers* (Maelezo juu ya Mwanzo 2:22). Kimetolewa kutoka https://biblehub.com/genesis/2-22.htm Mnamo Decemba 29, 2020.
[15] *Pulpit Commentary* (Maelezo juu ya Mwanzo 2:22). Kimetolewa kutoka https://biblehub.com/genesis/2-22.htm Mnamo Decemba 29, 2020.
[16] *Matthew Henry's Commentary on the Whole Bible*

Imara. Ndoa hujengwa katika msingi wa maagano ya mwanaume na mwanamke mmoja kila mmoja akijitolea kwa kipekee kwa mwenzake Maisha yao yote.

Ndoa inapaswa kuwa ya uwazi, kuaminiana, na uhusiano wa kukubaliana – "nao walikuwa uchi wote wawili, Adam na mkewe, wala hawakuona haya" (2:25). Kwa sababu dhambi ilikuwa bado haijaharibu hali ya kutokuwa na hatia ya wanandoa wa kwanza, basi ndoa yao bila hukumu, bila aibu wala uwoga. Agano jipya linatueleza, "Ndoa na iheshimiwe na watu wote na malazi yawe safi…" (Waebrania 13:4).

Ndoa iliyo imara haiwezi kupatikana mahali ambapo hapana usalama, kutoaminiana, kushuku mwenzako, au uwoga; mahali ambapo wanandoa hawana uhakika wa kujitoa kwa kila mmoja wao kwa kwenye ndoa. Ndoa iliyo imara yahitaji nadhiri, "Hadi kifo kitakapotutenganisha!" (Tazama Warumi 7:1-2).

Dhumuni ya Mungu ni kwamba ndoa iwe agano la maisha kati ya mwanaume mmoja na mwanamke mmoja (Mathayo 19:3-6). Paulo alisema kwamba waumini hawako chini ya utumwa wakati wenzi wao wasioamini wanapotengana nao (1 Wakorintho 7:15), lakini muumini hapaswi kutafuta kutengana na mwenzi asiyeamini (1 Wakorintho 7:12-14, 16). Paulo alikuwa ameandika hapo awali kwamba Bwana alisema vivyo hivyo: waumini hawapaswi kuchagua kuacha/kutengana na wenzi wao, lakini wakifanya hivyo, hawapaswi kuoa mtu mwingine (1 Wakorintho 7:10-11, Mathayo 5:31-32, Mathayo 19:9).

Upendo wa Agano ni wa kujitoa, heshima na wa kupendeza hata wakati uhusiano ni mgumu (1 Wakorintho 13). Kujitoa kuliko dhaifu husababisha kutengana kihisia, kutengana na majaribu.

Mume anayeishi kulingana na upendo wa agano hawezi kukata tamaa kwa mke wake hata wakati ambapo mke wake hana heshima, hajiotoi, au mgonjwa. Mke ataishi kulingana na upendo wa agano anapochagua kumheshimu na kumtii mume wake kwa sababu ya Kristo hata wakati mume wake hampendi.

Upendo wake husababisha kupata heshima toka kwake. Na heshima yake husababisha kupata upendo kutoka kwake na wanazidi kukua!

► Kuna shida gani wakati ambapo watu wataoana na kutarajia kwamba watabadilisha maamuzi yao baadaye kama hawatafurahia ndoa? Kuna tofauti gani wakati ambapo wana ndoa wamejitoa na kuamini ya kwamba ndoa yao ni ya milele?

(2) Ndoa ya Kibiblia ni mahali pa uumbaji: Uzazi

"Tazama wana ndio urithi wa Bwana uzao wa tumbo ni thawabu" (Zaburi 127:3).

Watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu, na kwa upande mwingine watoto ni zawadi kwa Mungu kutoka kwa wazazi. "Au je kuna mtu mmoja atafutaye mzao mwenye kumcha Mungu? Kwa hiyo jihadharini roho zenu, mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana" (Malaki 2:15).

Wengine hupendelea maisha pasipo watoto, lakini maandiko yanasema kwamba Mungu anapendezwa na wazazi walio na watoto wacha Mungu.

Ni muhimu tujue ya kwamba sio tu kuongeza kizazi ndicho ambacho Mungu anataka lakini watoto wacha Mungu. Wazazi wameitwa na Mungu kuwafundisha watoto wao kumfuata Kristo.

(3) Ndoa yaKibiblia ni ya Kristo.

Katika Waefeso 5:30-32, Roho mtakatifu anatoa maana na umuhimu wa ndani wa ndoa, ambao umefichika hadi kuja kwake Kristo. Ndoa ni picha ya ulimwengu —picha inayoonyesha—uhusiano uliopo kati ya Yesu Kristo na kanisa.

Paulo anaanza kwa kuwahimiza wakristo "wajazwe na Roho mtakatifu" (Waefeso 5:18). Ni katika muktadha huo anatoa maagizo yafuatayo kuhusu ndoa:

Mke aliyejazwa na Roho *ataonesha utii* kwa mume wake (kichwa" chake"), "katika Bwana," kama ambavyo wakristo wanamtii Yesu (Waefeso 5:24, 32; ona pia 1 Petro 3:1), na hivyo kuonyesha heshima kwa Yesu na mumewe.

Ni muhimu kila mke awe na "Bwana" katika akili yake anapotii. Ni kwake na kwa ajili yake ndio ananyenyekea na si kwa ajili ya mumewe tu. Macho yake yapo kwa yesu asiye na dhambi. Mke aliye tayari kumtii mume wake ni tendo la kumwabudu Yesu.

Kutii kimaandiko, kama upendo, hakulazimishwi. Kutii kimaandiko ni *zawadi* ambayo wake huwatolea waume kwa sababu ya kumcha *Kristo*. (Waefeso 5:33). Kutii kwa "kila kitu" (isipokuwa kile kinachotishia afya yake au kuhatarisha uhusiano wake na Yesu), ni tendo la kumwabudu Yesu.

Utii wa mke kwa mumewe ni tendo la heshima (mstari 33) kwake, kama sehemu ya maisha yaliyojaa Roho (5:18-21). Heshima hii itokayo kwa roho ya upole na wema ni ya thamani sana mbele za mungu (1 Petero 3:4).

Mume aliyejazwa na Roho. Atapenda mke wake kama vile Yesu alivyolipenda kanisa (Waefeso 5:25). Mume anastahili kumpenda mke kama vile aupendavyo mwili wake (Mstari 28-29). Lazima adhihirishe maisha yaliojazwa Roho na kujitoa kama vile Yesu alivyodhihilisha kwa kanisa "alipojitoa mwenyewe kwa ajili yake." Hili ni tendo la "unyenyekevu" (Waefeso 5:21). Mtoa maoni mmoja aliiweka namna hii :

> Kama yeye (Yesu) alivyojitoa kuteseka msalabani ili kuliokoa kanisa, vivyo tunastahili kujitoa wenyewe na kuchukua mateso na majaribio, ili kukuza furaha ya mke. Ni jukumu la mume kujukumika kwa mahitaji ya mke; ajinyime mapumziko kama inawezekana na kumshugulikia anapougua; kumlinda dhidi ya hatari; kumtetea akiwa katika hatari; kumvumilia wakati amekasirika; kushikamana naye hata wakati ambapo hamtaki; kuomba naye wakati yupo katika shida ya kiroho; na awe tayari kufa kwa ajili yake. Mbona hii isiwe hivyo? Kama meli imeharibika na wanazama majini na kuna kipande kimoja tu cha mbao ambacho juu ya hicho tu ndio kuna

> usalama, Je, haipasi yeye kumpa nafasi ya kwanza kuokolewa bila kujali hatari zinazomkabili mwenyewe? Lakini kuna zaidi …. Mume anastahili kuhisi ya kwamba ni jukumu lake kubwa kuona ya kwamba mke wake ameokoka. Anahitajika kumtimizia mahitaji yake yote atakayohitaji kiroho… na awe mfano; kumshauri anapohitaji ushauri; kufanya njia ya wokovu kwake iwe rahisi iwezekanavyo. Endapo mume ana Roho na moyo wa kujitoa kama Kristo, ataona kwamba hakuna gharama kubwa ya kulipa endapo ataweza kukuza wokovu wa familia yake.[17]

Mume anatakiwa kutafuta usafi wa kiroho wa mke wake kama vile Kristo ambavyo humsafisha bibi harusi wake ambaye ni kanisa, ".. ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno …(na) apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" (Waefeso 5:26-27).

Nyakati za kale wake wa kifalme walioshwa mwili na mafuta ya urembo ya thamani kubwa- "miezi sita kwa mafuta au manemane, na miezi sita kwa manukato yapendezayo , na kwa vitu vingine vya kusafisha wanawake (angalia Esta 2:12 na kuendelea). Kwa njia hii bikira aliandaliwa kwa mumewe.

Katika mtazamo wa kiroho, mume anastahili kujitoa kwa kila njia inayohitajika kwa ajili ya kunawiri kwa mke wake – uaminifu, upendo usio na masharti, maelewano, maombi, ushauri, mafundisho na utu wema.

Wakati mume anamtendea mkewe upendo wa aina hii , atalipwa furaha. Paulo anasema, "ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe" (Waefeso 5:28). Waume wapendao wake zao kwa hii njia ya kujitola watalipwa zaidi na Mungu, na zaidi ya hayo kwa heshima, upendo na uaminifu kutoka kwa mke wake.

► Ni mambo gani haswa ambayo mume anastahili kufanya ili ampe usaidizi wa kiroho mkewe**?**

Jinsi ambavyo wanandoa wanaweza kuboresha ndoa yao

(1) Ni lazima wafurahie mpango wa Mungu wa asili na watambue majukumu yao maalum kwenye ndoa.

Waume lazima wakumbuke kwamba wake zao ni zawadi kutoka kwa Mungu na "mwenza mkamilifu," na kutoa maisha yao kwa sababu ya usalama wao na kiroho, kihisia na uzima wa mwili. Ni lazima achague kuwa na shukurani na kumpenda hata wakati ambao ni kana kwamba hastahili, akijua ya kwamba ni Mungu pekee anaweza kubadilisha kile ambacho lazima kibadilishwe ndani mwake. Mungu ataheshimu uaminifu wake na imani.

Mke ni lazima aheshimu chaguo la Mungu la mume wake kama kichwa chake kwa kumwonyesha heshima kwa kila njia iwezekanayo na aheshimu uongozi wake. Lazima achague kutii na kuheshimu hata wakati ambapo amefanya makosa na hastahili

[17] Albert Barnes, *Commentary on Ephesians*, (Sura ya tano)

kuonyeshwa unyenyekevu, huku akiomba ya kwamba Mungu kubadilisha kile ambacho kinahitaji kubadilishwa ndani yake. Mungu ataheshimu utiifu wake na imani.

(2) Wanandoa lazima wakuze uhusiano wa kweli wa kiroho na kimwili.

Lazima wazingatie kujuana kila mmoja na mwingine bila uoga, ukosoaji, kulinganisha na wengine, unyanyasaji, tamaa, kujiridhisha binafsi au kumdhalilisha mwingine. Ni lazima waishi kwa uwazi na uadilifu mbele za Mungu na mbele ya kila mmoja.

(3) Wanandoa lazima watumie mfano wa neema ya Mungu wanapopungukiwa.

Adamu na Hawa walipoanguka katika dhambi walipata aibu na majuto, Mungu alifunua uwezo wake wa kuwakomboa katika udhaifu wao. Mungu alimtoa mnyama ili kufanya mavazi kwa ajili ya Adamu na Hawa ili kufunika uchi wao (Mwanzo 3:21). Tendo hili la upendo lilikuwa ni picha ya neema na ahadi ya Mungu ya ukombozi kupitia Kristo Yesu. Kuvalishwa na Mungu kupitia Kristo Yesu kuliwawezesha na kunatuwezesha sisi kusamehewa na kurejeshwa. Kupitia Kristo wanandoa wanaweza kurudi kwenye urafiki usio na haya baada ya kufanya dhambi.

Yesu Mfano wa Heshima kwa Wanawake

Wanawake walichukuliwa kuwa duni wakilinganishwa na wanaume katika karne ya kwanza katika ulimwengu wa Kirumi na katika dini ya Kiyahudi. Pia mtazamo huo huo unaonekana katika tamaduni za kisasa duniani, pia katika jamii na katika nyumba. Wanawake hawaheshimiwi na wanatumika kama vyombo vya starehe, na wanadhulumiwa. Lakini heshima kuu kwa wanawake kutoka kwa Yesu inapaswa kutumika kama mfano wa kuigwa.

Kwa Yesu wanawake wana hadhi na heshima sawasawa na wanaume. Yesu akasema, "...yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke'" (Mathayo 19:4; Mwanzo 1:27). Wanawake wameumbwa katika sura na mfano wa Mungu kama vile wanaume, wanajitambua, wana uhuru wao, wana motisha wa maisha na wanawajibika kwa matendo yao.

Yesu aliwatambua wanawake Kama wanadamu wengine. Wafuasi wa Yesu walikuwa katika jinsia mbili, wakiume na wakike. Wale wa kike Yesu huwaona kama watu halisi, sio tu kama vyombo vinavyotumika kwa tamaa za wanaume. Anawaona kama watu ambao alikuja duniani kwa sababu yao.

James Borland, na John Piper na Wayne Grudem, wanatupa mfano ulio wazi wa jinsi Yesu alivyo wachukulia wanawake na jinsi alivyo waheshimu kama inavyoelezwa katika vitabu vinne vya injili:

(1) Yesu mara kwa mara aliwahutubia wanawake hadharani.

Haikuwa kawaida wakati wa Yesu mwanaume kuongea moja kwa moja na mwanamke hadharani (Yohana 4:27). Wanafunzi walishangaa kuona Yesu akiongea na mwanamke Msamaria kwenye kisima cha Yakobo pale Sikari (Yohana 4:7-26). Yesu aliongea kwa uhuru

na mwanamke aliyefumaniwa akizini (Yohana 8:10-11). Luka anasema Yesu aliongea hadharani na mjane wa Naini (Luke 7:12-13), na mwanamke aliyetokwa na damu miaka kumi na miwili (Luka 8:48; Mathayo 9:22; Marko 5:34), na Yule mwanamke aliyemuita katika halaiki (Luka 11:27-28). Yesu aliongea na mwanamke aliyekuwa amejipinda mgongo kwa miaka kumi na minane (Luka 13:12) na kikundi cha wanawake waliokuwa wakilekea Golgotha alikosurubiwa (Luka 23:27-31).

(2) Yesu alionyesha heshima na hadhi ya juu kwa wanawake kwa namna alivyoongea wakati alipokuwa akiongea nao.

Aliongea kwa kujali na kwa kutafakari. Mathayo, Marko, na Luka wanarekodi kuwa Yesu alimuongelesha mwanamke aliyetokwa na damu kama "binti" na pia alimwita mwanamke aliyejipinda mgongo "binti wa Ibrahimu" (Luka 13:16). Kwa kuwaita "binti za Ibrahimu" Yesu anawaweka katika kiwango cha kiroho sawa na "wana wa kiume wa Ibrahimu."

(3) Yesu anaonyesha asili na thamani ya wanawake kwa kufanya wao kuwajibika kibinafsi kwa dhambi zao.

Hii inaweza kuonekana kwa jinsi alivyokabiliana na mwanamke msamaria kisimani (Yohana 4:16-18), kwa mwanamke aliyezini (8:10-11), na mwanamke mwenye dhambi aliyetawadha miguu yake Yesu (Luka 7:44-50). Dhambi zao hazikupuuzwa lakini zilikabiliwa. Matendo yake yalionyesha kwamba kila mwanamke alikuwa na uhuru wa kibinafsi na uwajibikaji kwa maamuzi yake, na ni lazima kila mmoja kibinafsi akabiliane na dhambi, toba, na msamaha.

Jinsi ambavyo Yesu aliwathamini wamawake kunapaswa kuongoza kanisa la sasa.

Nafasi bora ya kibiblia ya wanawake katika huduma na nyumbani inajadiliwa sana katika kanisa la sasa, kama inavyostahili, japokuwa thamani na usawa wa mwanamke kuwa ameumbwa katika sura na mfano wa Mungu sio jambo la kutilia shaka. Yesu aliendeleza kuonyesha thamani na hadhi ya wanawake kama watu. Aliwatuma kama wajumbe wake wa kwanza kutangaza habari njema za kufufuka kwake (Yohana 20:17). Alithamini ushirika wao, maombi, huduma kwa wakristo, msaada wao wa kifedha, ushuhuda wao na kushikiki kwao katika injili. Yesu aliwaheshimu wanawake, akawafundisha, akawahudumia huku akiwawaza.

Heshima kwa wanawake katika agano jipya.

Mfano wa Yesu akiheshimu wanawake unaonekana katika maisha ya Roho Mtakatifu. Katika siku ya penteconte, Roho Mtakatifu alimwagwa juu ya wote "wana na binti," na "watumishi wa kiume na wa kike" (Matendo 2:17). Roho Mtakatifu hakuonyesha ubaguzi.

Katika Warumi 16, Paulo anamthibitisha mwanamke aitwae Fibi kama "mtumishi kanisani" (mstari wa 1), Pirisila na Aquila kama "wafanya kazi pamoja na yeye kwamba waliojitoa maisha yao kwa ajili yake". (mstari wa 3-4), Mariamu ni mojawapo ya "waliofanya kazi kwa

bidii” (mstari wa 6), Junia kama mmoja “aliyejulikana sana kwa mitume” (mstari wa 7), na wanawake wengine pia.

Katika 1 Wathesalonike Paulo anathibitisha kwamba ni Mungu aliyewapa upole na upendo anapoandika, “tulikuwa wapole kwenu, kama vile mlezi awatunzavyowatoto wake mwenyewe” (1 Wathesalonike 2:7). Katika Waefeso anawaamrisha wanaume kuwapenda wake zao, “kama Kristo alivyolipenda kanisa na akajitoa kwa sababu yake,” na “kama miili yao wenyewe” (Waefeso 5:25, 28). Petro anawasihi wanaume “kuishi na wao kwa akili , na kumpa mke wako heshima…” (1 Petro 3:7).

Ni wazi kwamba wanawake waliheshimiwa na wanaume walifundishwa kukaa kwa heshima na wao katika kanisa la kwanza. Ni wakati wa kila kiongozi wa kanisa popote kusimama na kuwatetea wanawake ili waheshimiwe na desturi za kuwafanya wanawake duni zikemewe. Ni wakati wetu sasa kuthamini wanawake kama watu maalumu walioumbwa na Mungu katika sura yake. Mafundisho yoyote ya majukumu ya wanaume na wanawake kanisani au nyumbani lazima yaanze katika misingi hii la sivyo mafunzo yetu yatakuwa njia na chanzo cha unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Hitimisho

Ndoa ni uumbaji wa Mungu na sio wa mwanadamu, kwa hivyo ni lazima twende kwa Mungu kwa ushauri na maelekezo sio katika dunia wala tamaduni zetu. Ni yeye pekee awezaye kufanya ndoa zetu kuwa imara, dhabiti na za furaha. Lakini hatutaweza kuwa mwanandoa ambao tunastahili kuwa pasipo Roho Mtakatifu!

Kushiriki kwa vikundi

► Eleza kanuni ambazo Kanisa lazima lifundishe ili kufanya ndoa kuwa thabiti. Ni kipi hasawa ambacho kinakosekana katika maeneo yako?

► Je tamaduni yako humchukulia vipi mwanamke akilinganishwa na mwanaume?

► Je ni jinsi gani makanisa katika nchi yako huwachukulia wanawake tofauti kwa kulinganisha na wanaume? Je kuna tofauti kati ya kanisa na tamaduni?

► Ukizingatia mfano wa Yesu ni desturi zipi lazima zibadilishwe?

Maombi

Baba wa mbinguni,

Asante kwa zawadi ya ndoa. Tusaidie tujitoe kwa mambo ambayo ni ya muhimu na ambayo yatafanya sisi kufanya ndoa iwe kama ulivyokusudia.

Tusaidie tuoneshe upendo kama ule ambao unaoneshwa na Kristo kwa Kanisa.

Tusaidie twende zaidi ya tamaduni zetu kwa kuheshimiana kila mmoja na mwingine.

Asante kwa Roho mtakatifu ambae anafanya uhusiano uwe na furaha wenye nguvu na wa kuwezekana.

Amina

Zoezi la somo la 6

(1) Eleza kwa kuandika tofauti iliopo kati ya wanaume na wanawake katika tamaduni yako. Je tofauti hizi zinawezaje kubadilishwa kwa uangalifu tukitumia ukweli ulio katika neno la Mungu?

(2) Chagua kanuni mbili ambazo zimekuwa mpya kwako katika somo hili. Andika aya moja ukizieleza kwa maneno yako mwenyewe.

(3) Andaa taarifa ya kuwasilisha kati ya mojawapo ya mada ambazo zimeorodheshwa (kiongozi wa darasa atampa kila mwanafunzi mada ya kuzingatia.) shiriki utafiti wako katika somo litakalofuata.

- Mpango wa Mungu wa muungano katika ndoa.
- Kusudi la kimaandiko katika ndoa.
- Njia za kuboresha ndoa.
- Mtazamo wa Biblia kuhusu wanawake
- Majukumu katika ndoa kama vile ambavyo Mungu ameelekeza na umuhimu wa kujazwa na Roho Mtakatifu ili kutimiza majukumu haya.

Somo la 7
Utakatifu wa Ndoa

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Aelewe mpango wa Mungu wa ndoa na sheria za ndoa ambazo zitalinda ndoa dhidi ya shida na kuleta Baraka.

(2) Kuelezea maelekezo ya maandiko kwa ajili ya familia.

Robertson McQuilkin, Mtunza ahadi

Dr. Robertson McQuilkin alitumika kama misionari katika taifa la Japani kwa miaka kumi na miwili. Baadae akawa raisi wa chuo kikuu cha Kimataifa cha Columbia. Alijulikana kama mwandishi, mnenaji na mkufunzi. Mke wake Muriel aliugua maradhi ya Alzheimer's (kupoteza kumbukumbu). Ugonjwa ulipozidi kwa kiwango ambacho alihitaji huduma ya karibu, Dr. McQuilkin alijiuzuru kutoka kwenye nafasi yake ya urais wa chuo ili amshugulikie mke wake. Alisema kwamba anazingatia maungamo yake na ahadi alizoahidi mke wake wakati alipomuoa. Aliamini kwamba kumtumikia mke wake kulikuwa kwa maana kuliko nafasi aliokuwa nayo katika chuo kama raisi.

Chuo cha Mungu cha Ndoa

Ndoa ilianzishwa na Mungu kati ya mwanamume na mwanamke wa kwanza ambao Mungu aliwaumba.

► Mwanafunzi asome Mwanzo 2:21-24 kwa niaba ya kikundi. Je, Maandiko haya yanatuambia nini kuhusu ndoa?

Ndoa imeumbwa na Mungu ili iwe hasa kile ambacho watu walihitaji. Ilitengenezwa hasa kwa asili ya mwanadamu. Katika kila kitu ambacho Mungu aliumba na kwa kila kitu anachohitaji, Mungu hutaka kutoka kwake kilicho bora zaidi kwetu sisi.[18] Mungu anajua kwamba mpango wake wa ndoa utampatia kila mwanandoa hisia nzuri, ushirika, uhusiano na afya ya kiroho.

Ndoa imeumbwa pia iwe mfano wa tabia za Mungu na uhusiano wake. Mungu Baba, Mungu Mwana Na Roho mtakatifu daima wamekuwa na watakuwa daima katika ushirika moja na mwingine. Kila mmoja ni wa kipekee katika jukumu lake, lakini Nafsi zote za Utatu ni Mmoja wa kudumu na ni wa asili moja. Katika uhusiano katika utatu tunaona umoja, urafiki wa karibu,uaminifu na upendo udumuo. Ndoa ya kibiblia inaundwa kwa kufuata kielelezo cha

[18] Kumbukumbu La Torati 6:24

uhusiano huu wa ajabu. Mpango wa Mungu kwa kila mume na mke ni kuwa na upendo halisi na uaminifu kila mmoja kwa mwingine kwa Maisha yote.

Mungu anasema katika ndoa mume na mke watawaacha wazazi wao nao wanaunganishwa pamoja. Ndoa huweka marafiki wawili pamoja katika kushirikiana kwa pamoja kuliko uhusiano mwingine wowote wa kibinadamu.

Ndoa sio tu watu wawili kukaa pamoja katika uhusiano. Maisha yao yameunganishwa ili kwamba wawe kama mtu mmoja. Hii sio kwamba hawana tabia zao za kimaumbile, bali wapo katika muumganiko maalumu.

Kudumu kwa Ndoa

Mungu aliweka ndoa iwe ya kudumu. Katika ndoa mwanaume na mwanamke huahidiana kuwa waamifu kila mmoja kwa mwingine kwa Maisha yao yote.

Biblia inaonyesha maneno ya Yesu a kuhusu ndoa, yaliyosemwa katika mazungumzo na mafarisayo.

► Mwanafunzi asome Mathayo 19:3-8 kwa niaba ya kikundi.

Yesu anasema Mungu alikusudia ndoa iwe ya kudumu. Talaka ni kwa wale ambao hawamjui Mungu.

Kuna sababu nyingi ambazo zinazoonesha Mungu aliitengeneza ndoa ili iwe ni ya kudumu, baadhi ya sababu tumeziona hapo awali katika masomo yetu. Sababu nyingine ambayo huitaka ndoa iwe ya kudumu ni kwa ajili ya watoto. Kutii mpango wa Mungu katika ndoa huleta mazingira mazuri ya kuwalea watoto. Kwa kadri wazazi wanavyomheshimu Mungu kwa kutii kanuni zake katika ndoa na familia, wataweza kulea watoto wa kimungu.[19]

Mungu aliyatengeneza maisha mtu kwa namna ambayo itamchukua mtu miaka mingi kabla hajakomaa na kuwa mtu mzima. Katika wakati huo, watoto hutegemea sana wazazi kwa ulinzi, mahitaji na mafunzo. Hii ni tofauti na wanyama ambao huchukua muda mfupi ili waweze kukomaa mwaka mmoja hadi miwili. Wanadamu wanahitaji muda mwingi ili kujenga tabia ya ukomavu. Mungu ameiweka familia ili iwe ni mahali pa kulea watoto. Matatizo mengi katika jamii hutokana na kukosa familia yenye wazazi ambao ni waaminifu.

Ndoa inahitaji watu kutoa ahadi ya kujitoa kila mmoja kwa mwenzake maisha yao yote. Kila tamaduni ina namna na sherehe ya kuonesha kwamba ndoa ni ahadi nzito. Sherehe ni njia ya hao wawili kusema hadharani kwamba wamejitolea kutunza ahadi yao ya maisha.

Serikali nyingi huweka rekodi za ndoa. Sheria kuhusu ndoa huathili umiliki wa mali, nani atakaa na watoto, na urithi.

Hapa kuna mfano wa kiapo katika ndoa ambacho imetumika katika harusi nyingi:

[19] Malaki 2:15

Nakuchukua wewe uwe mume/mke wangu wa ndoa kuwa nawe kuanzia leo na kuendelea, katika hali njema ama mbaya, katika utajri au umaskini, katika afya njema ama magonjwa, nitakupenda na kukutunza hadi pale kifo kitakapotutenganisha; kulingana na agizo takatifu la Mungu, na kwa hiyo nakupa ahadi yangu.

Hisia za mapenzi hazitakuwepo kila mara. Ndoa haiwezi kuwekwa katika ya misingi hisia za kibinadamu ambazo hubadilika. Kiapo cha ndoa humaanisha ya kwamba mume na mke wameaahidiana kuwa waaminifu kwa Maisha yao yote, na kiapo hiki hakitegemei vigezo na masharti yoyote.

Ndoa kama Ushirikiano wa kikristo.

► Mwanafunzi asome 2 wakorintho 6:14-18 kwa niaba ya kikundi.

Maandiko haya yanatuambia ya kwamba uwajibikaji wa mkristo hupata vikwazo kutokana na ushirika wa karibu na wasioamini. Kama ambavyo mkristo hawezi kuabudu na mtu anayemwabudu shetani, pia hawezi kufuata mtindo wa maisha na vipaumbele vya wasioamini. Onyo hilo linaweza kutumika katika aina mbalimbali za mahusiano, ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa kibiashara.

Ndoa ni ushirika wa karibu zaidi wa mwanadamu. Mkristo asifikirie hata kuingia kwenye ndoa na asieamini (1 Wakorintho 7:39). Mkristo aliyeoa mtu asiyeamini atakumbana na hofu na vikwazo vingi katika kulea watoto na katika kufanya maamuzi ya maisha.

Kama mume na mke wameokoka na wametoka katika makanisa tofauti ni lazima wahakikishe ya kwamba wanaelewana katika mambo kadhaa ya kiroho. Ni vizuri wapange wawe wanaabudu katika kanisa moja baada ya harusi.

► Kwa nini ndoa huanza na kiapo na sio tu maneno ya upendo**?**

Kiwango cha Maadili cha Mungu.

► Mwanafunzi asome Waebrania 13:4 kwa niaba ya kikundi.

Aya hii inatwambia ya kwamba ndoa lazima iheshimiwe. Dhambi ya kuzini ni ya kutoheshimu ndoa. Mungu atahukumu dhambi ya zinaa.

Dhambi za zinaa zinajumuisha usherati, uzinzi, mapenzi ya jinsia moja, na utumiaji wa filamu za ngono au ponografia. Usherati ni mahusiano ya kindoa kati ya wale ambao hawajaoana tayari. Uzinzi inajumuisha tendo lolote la ndoa kati ya mtu aliyefunga ndoa na mtu ambaye si mwenzi wake. Ushoga ni mahusiano ya kindoa kati ya watu wa jinsia moja. Ponografia inajumuisha maandishi, picha na video zilizoundwa kusasabisha mihemko ya kihisia ya kujamiiana kwa kuonyesha picha za uchi au shughuli za kujamiiana. Mambo haya yote ni ukiukwaji wa mahusiano ya ndoa.

► Mwanafunzi asome 1 Wakorintho 6:9-10 kwa niaba ya kikundi.

Kila jamii ya watu wana mtazamo wa kijamii kuhusu mahusiano ya mwanamke na mwanaume. Viwango vya kijamii viko chini sana kulinganishwa na vya Kimaandiko. Tamaduni nyingi zimeweka sheria tu za kufanya jamii kuishi tu Kwa umoja. Wanavumilia dhambi za zinaa kama zitafanywa pasipo maangamizi au hasara kubwa. Viwango vya maadili ya Mungu ni tofauti.

Kinachohuzunisha ni kwamba, makanisa mengine hufuata maadili ya tamaduni zao badala ya maadili ya Mungu katika Biblia. Huwaadhibu watu ambao makosa yao ni dhahiri na yasiyojali, lakini wanavumilia dhambi hiyo hiyo inapofanywa na watu kwa uangalifu.

Maandiko yanasema mambo haya hufanywa na wale ambao sio wakristo na hawataenda mbinguni. Baadhi ya wakristo katika Korintho walifanya dhambi hizo zamani lakini waliokolewa kutoka huko.

Imani yeyote inayovumilia dhambi yeyote kati ya hizi kwa mtu anayedai kuwa ni mkristo ni Imani potofu. Kama mtu yeyote atajiita mkristo na anafanya dhambi ya zinaa Maandiko yanalitaka kanisa kumtoa kanisani na wasimchukulie kama mkristo (1 Wakorintho 5:11-13).

Viongozi wa kanisa ni vizuri wawe kielelezo kwa tabia njema. Kanisa likiruhusu viongozi wa ibada kuvaa isiyopaswa au kuruhusu namna ya kucheza ambako hakuleti sifa kwa Mungu linamaanisha kwamba tamaa za mwili zinatawala . Hii inamaanisha kwamba dhambi za zinaa hazishughulikiwi ipasavyo.

Labda mivalio ya jamii itaonyesha mwanamke hajavaa vizuri kama hajavaa ili avutie huku akionyesha sehemu zingine za mwili. Washirika wa kanisa wakati mwingine huanguka katika jaribu hili mara kwa mara hasa katika sherehe. Wanafikiri hawajavaa vizuri kama hawajafuata namna ya mavazi katika jamii yao. Kanisa lazima lifundishe ya kwamba hiyo ni mbaya. Mkristo hastahili kusababisha mwingine kuanguka katika tamaa mbaya. 1 Timotheo 2:9-10 inatuambia kwamba mkristo anapaswa avae na aenende kwa namna ambayo wengine wakimuona watajua ya kwamba anaishi maisha ya kujichunga na hakusudii kutenda dhambi wala kufanya mwingine kufanya dhambi. Wanawake wakristo wanapaswa "...kuvaa mavazi ya kusitiri pamoja na adabu mzuri na moyo wa kiasi"

Msaada kwa Mwenye Dhambi

Wagalatia 6:1 inasema kwamba kanisa lina jukumu la kujaribu kumrejesha mshirika ambaye amefanya dhambi. Hii haimaanishi ya kwamba mtu huyu apewe nafasi ya uongozi au kurudishwa haraka katika nafasi ya huduma baada ya kufanya dhambi. Urejesho unamaanisha kukubaliwa tena katika ushirika na kuhudumiwa na kanisa. Mshirika akitubu kwa kumaanisha, anasamehewa na Mungu na kanisa. Kanisa linapaswa kuwajibika kiroho ili kumsaidia awajibike ili awe mshindi na awe shujaa wa kiroho.

Kama msichana ambae hajaolewa akipata mimba, kanisa halistahili kumfukuza kama hawajajaribu kumrejesha kiroho. Kama atatubu na kunyenyekea na pia kuwajibika kwa alichokifanya, atasamehewa. Dhambi yake sio mbaya kuliko ya mwanaume aliyesababisha

hilo. Wakati mwingine msichana anatendewa kwa ukali kwa sababu tu matokeo ya dhambi yake yanaonekana sana.

Kanisa ni jamii ya kiimani. Haitoshi tu kanisa kukemea dhambi. Lazima kanisa litunze watu wake. Kwa Mfano, mwamke anapata riziki kupitia njia ambazo hazifai, haitoshi tu kwa kanisa kumwambia kwamba hiyo haifai lakini pia wawe tayari kumpatia njia mbadala anapotubu.

Mfano halisi…

Wasichana kadhaa walikuwa wanahudhuria kanisa fulani kubwa na walikuwa wakiimba katika kwaya. Familia zao zilikuwa maskini. Wasichana hawa walikuwa katika uhusiano potovu na wanaume ili kupata fedha za kusaidia familia zao. Kanisa linapaswa kufanya nini katika hali kama hili?

► Kanisa lako linapswa kufanya nini ili kusaidia wanaoishi katika maisha ya dhambi?

Ponografia

Ponografia ni maadishi, picha na video ambazo zimeundwa kuamsha hisia za kimapenzi kwa kuonyesha picha za utupu na kujamiana.

Mitandao inafanya picha za utupu kupatikana kwa njia rahisi duniani. Hali ya matumizi ya teknologia inafanya picha hizi kuwa jaribu kwa mabo hawajafundishwa kukabiliana nalo kutumia kanuni za kikristo. Wachungaji wengi waliokomaa hawakukabiliana na jaribu hili kwa sababu hapakuwepo na mtandao kama sasa. Wanaweza kosa kuelewa kile ambacho jamii hii changa inakabiliana nacho.

Ponografia ni mbaya kwa sababu imetengenezwa ili kumfanya mtu afurahie kwa kuwaza mambo ya uasherati na uzinzi, na mengine mengi yaliopotoka. Inavutia mtu aliye na tamaa mbaya. Ponografia humfanya mtu kuvutiwa na tabia mbaya ambazo Mungu anachukizwa nazo.

Ponografia ni uraibu. Mtu ambae huona ponografia hupata msukumo mzito wa uhitaji wa kuziona. Hawezi kuishi pasipo kuona zile picha. Kwake maisha yanaonekana matupu na yasiyofurahisha bila mawazo anayopata kutokana na ponografia. Kama aina nyingine ya uraibu inavyofanya kazi, hamu au tamaa inaanza kumla na mwathiliwa huanza kupuuza kile ambacho ni kizuri katika maisha yake.

Ponografia ni Endelevu. Mtumiaji anahitaji zile picha ambazo zinazidi kuwa wazi na potofu. Huanza kupendezwa na mawazo ambayo mwanzoni yangemchukiza na kumtia hofu.

Ponografia Zinaharibu. Mtumizi ya ponografia huaza kusababisha kutopenda mahusiano ya kawaida. Tamaa yake inaaza kuwa isiyokuwa ya kawaida na ambayo haiwezi kutoshelezwa. Anaanza kuacha kujali wengine pasipo kujali.

Wachungaji na wazazi lazima wawaonye vijana kuhusu uraibu. Wazazi wasiwaruhusu watoto wao kuingia katika mtandao bila kudhibitiwa na kama hawana uwezo wa kuzuia

jaribu. Mtu yeyote anapambana na hali hii ni vizuri awe na mwingine ambaye anawajibika kwake. Atawajibika kwa huyu mtu mara kwa mara.

► Ni baadhi ya njia/mazoea gani unapendekeza ili kusaidia kulinda watu kutokana na uraibu wa kutazama ponografia? Ni kwa jinsi gani Kanisa linaweza kusaidia?

Ushoga na Usagaji

Jamii za kisasa ambazo zinakataa mamlaka ya Biblia pia wanakataa jinsi ambavyo Biblia inasema kuhusu ndoa. Wanasema wako huru kuchagua kuoana na hata mtu wa jinsia yake.

Biblia inakataa ushoga na usagaji (mapenzi ya jinsia moja).

► Kikundi waangalie Warumi 1:26-27, 1 Timotheo 1:10, and 1 Wakorintho 6:9 kwa pamoja.

Maandiko haya matatu yanahusisha mapenzi ya jinsia moja kama baadhi ya dhambi ambazo ni mbaya sana. Watu ambao hufuata na hufanya Dhambi hizi hukataa mamlaka ya Mungu.

Wengine husema ya kwamba wao kwa asili wana asili ya ushoga. Wanasema wasilaumiwe kwa tabia yao ya ushoga kwa sababu hawakuchagua kuwa na hisia hizo.

Mandiko yanasema ya kuwa ya kuwa kila mmoja ana asili ya dhambi (Isaya 53:6). Mungu anatutaka tuweze kutubu dhambi zetu tulizokusudia (Isaiya 55:7). Kwa sababu tumezaliwa na asili ya dhambi, tamaa zetu za asili haziwezi kuaminiwa kutuongoza. Mtu anaweza kupata hisia nzito na kuvutiwa na mwelekeo wa asili ili kufanya uasherati, au mwenye fujo au vurugu, au kuiba, lakini kuwepo kwa mvuto wa asili haimaniishi kuwa huo mvuto ni sawa.

Kanuni ya kumheshimu Mungu kwa usafi wa tabia kabla ya ndoa.

Vijana hukutana na majaribu makubwa kabla ya ndoa. Ni vizuri wakumbuke ya kwamba wanahitaji mwenza wa Maisha ambaye anaweza ni mwaminifu.[20] Wasiweze kuwakubali wale ambao wanataka kujifurahisha tu kwa muda mfupi tu pasipo ndoa. Wasipendezwe na mahusiano na yule ambae siyo mkristo. (1 Wakorintho 7:39). Waweze kuwatambua wale ambao watakuwa waaminifu na wazazi wazuri.

Kijana anayetaka ndoa nzuri lazima awe mwaminifu, mkristo mwaminifu ili avutie yule anayefaa.[21] Mtu anayeonesha tabia mzuri na anayevaa vizuri (1 Timotheo 2:9-10). Watu ambao hawana maadili na huvalia visivyo kana kwamba wanawavutia jinsia nyingine wanadokeza kwamba wako tayari kwa mahusiano yenye msingi wa tamaa mbaya.[22] Mtu anayevaa kusasabisha tamaa mbaya atavutia wale wasiofaa.[23]

Mungu amewapa vijana wazazi, wachungaji na viongozi wengine wa kiroho ili wawape ushauri katika mienendo, mivao na uchaguzi katika mahusiano. Kama vijana ni vizuri

[20] Ona Mithali 31:11-12, 1 Timotheo 3:12, Malaki 2:14-16, Mithali 2:16-17.
[21] Mithali 3:4-8
[22] 1 Wathesalonike 4:1-7
[23] Mithali 7

tunyenyekee kwa viogozi hawa na Mungu na watapata Baraka kubwa na Mungu atawalinda kutokana na majaribu na maadhara.

► Mwanafunzi asome 1 Petro 5:5 and Waebrania 13:17 kwa niaba ya kikundi.

Ni jukumu la watoto na vijana kunyenyekea katika hekima na mahusia ya wazazi na viongozi wao wa kiroho. Ni jukumu la viongozi hawa kusaidia hawa vijana ili waishi maisha ya ushindi dhidi ya majaribu.

► Someni Warumi 13:14 and 1 Wakorintho10:13 kwa pamoja.

Mungu haruhusu wakristo kuwa katika hali ya majaribu ambayo itawashinda bali ile ambayo wanaweza kuipinga na kuishinda. Vijana wana jukumu la kutoroka kwa majaribu. (2 Timotheo 2:22). Pia wazazi wanastahili kuwazuia vijana kupata majaribu yasiowafaa iwezekanavyo. Kuna angalau njia tatu ambazo wazazi wanaweza kufanya hivyo:

(1) Kwa kuwapa maelekezo sahihi ya vile Watoto wanavyopaswa kufanya, wakiwa na nani na wapi wanapaswa kwenda. (Waefeso 6:1-4).

Wazazi wasiruhusu watoto kuwa katika hali ambayo umri wao hauruhusu kuwalinda kutokana na majaribu. Kwa mfano kijana wa kiume na kijana wa kike wamekaa mahali palipojificha peke yao ni rahisi kupata majaribu ya kutenda dhambi.

(2) Kwa kuwafanya vijana kuwajibika katika maeneo ya majaribu

(3) Kwa kuwapa vijana ushauri wa kimaandiko.

Wazazi wanapaswa kuwasaidia vijana wao kujifunza kufikiria hali kwa kuzingatia kanuni za Biblia (Mithali 4:1-9; 7:1, 4-5). Waongee na vijana wao kuhusu hatari ambazo wanaziona. Ni vizuri waongee na vijana kuhusu maamuzi ambayo watahitaji kuyafanya. Wanaweza kuwasaidia vijana kufikiria jinsi ya kuepuka majaribu na kile wanachohitaji kufanya wanapokuwa na majaribu.

Kanisa lazima liwe tofauti na utamaduni wake linapotetea maadili ya kibiblia. Tamaduni nyingi hazizingatii dhambi ya zinaa kuwa ni mbaya. Wanatarajia vijana ambao hawajaolewa kuwa na uhusiano wa kindoa kabla ya ndoa. Kanisa lisikubaliane na dhambi. Kanisa halipaswi kufikiri kuwa dhambi ya zinaa miongoni mwa vijana ni jambo la kawaida. Mungu anasema wale wanaofanya uasherati sio wakristo. (Waefeso 5:3-7, Waebrania 13:4).

Wakati wa mahusiano kabla ya ndoa sio wakati wa kujamiana. Badala yake ni kipindi cha wakati ambapo mwanamume na mwanamke huhakikisha kwamba wana vipaumbele sawa vya kiroho na kibiblia. Ni wakati ambao wanakuza uelewa wa kila mmoja wao na unaowawezesha kuaminiana vya kutosha kufanya ahadi ya kudumu kwa kila mmoja. Kama hawawezi kuafikia kiwango hicho inabidi waache urafiki wao na wasifunge ndoa.

Watu wengine katika tamaduni zingine hufanya ndoa kuchelewa sana na baadae hufanya harusi kuwa ya gharama mno. Wakati mwingine pia wanaokusudia kuoana hukaa pamoja na wanapata watoto huku wakichelewesha ndoa. Kwa wengine matumizi katika sherehe ya

harusi huwa ghamarama kubwa kiasi cha kuteseka baadae kwa sababu walitumia kila kitu kwa ajili ya sherehe na ilibidi wakope fedha. Kanisa linapaswa kuwa mahali ambapo kuna muundo mbadala wa sherehe za ndoa. Ndoa ya kikristo ni kati ya mwamume na mwanamke ambao wamejitoa kila mmoja kwa mwenzake na kwa Mungu na haipaswi kuwa na matumizi mengi yenye gharama kubwa ambazo zitafanya ndoa yao kuumia hapo mbeleni.

► Ni kwa njia zipi ambazo ndoa ya mkristo inastahili kuwa tofauti na ya kitamaduni?

Watu ambao hawataoa

Ndoa ni mpango wa Mungu kwa watu wengi. Hata hivyo mtume Paulo anaeleza sababu ambazo zinaweza kufanya watu wasioe. Katika 1 Wakrintho 7:26 anataja "mateso yaliopo"—hali ngumu ya maisha ambayo inaweza kuwa pia mateso. Anasema ni vyema mtu asioe akiwa katika hali hii.

Aya hiyo pia (1 Wakorintho 7:32-35) inasema mtu asiyeoa ana faida ya kipekee. Asiyeoa anaweza kujikita katika kumfanyia Mungu kazi pasipo kujali familia maana hana. Pae ambapo mtu ameitwa na Mungu katika Huduma kabla hajaoa, anaweza kufanya huduma vizuri sana.

Kunazo sababu zaidi anbazo Mungu anaweza kumchagua mtu kubaki bila kuoa. (Mathayo 19:10-11). Tusione kwamba hili jambo sio la kawaida. Tusione ya kwamba kila mtu ambaye hajaoa lazima apate mwenzi wake. Tusifikiri kwamba raha kamili hupatikana katika ndoa pekee.[24]

Mtu ambaye hajaoa lazima awe mwangalifu ili ajiepushe na mahusiano mabaya kwa sabau ya hisia na tamaa ya mwili. Mungu humpa furaha na kutosheka, mtu ambaye amejitoa kikamilifu kwake.

Maelekezi ya kimaandiko katika ndoa

► Someni 1 Petro 3:1-7 na Waefeso 5:22-33 kwa pamoja. Kikundi wafungue maandiko ili kuichunguza wakati wa somo.

Mwanaume ameambiwa ampende mkewe kama vile Kristo anavyolipenda kanisa. Yesu alijitoa kama dhabihu kwa kanisa. Mume atajitoa kwa faida zake mwenyewe, starehe, na matamanio yake ili akutane na mahitaji ya mkewe. Aya inasema kwamba "aishi naye kwa akili," kumaanisha ya kwamba atafanya kila awezavyo ili kumuelewa. Lazima amsome vizuri ili amuelewe.

Mwanamke anaitwa "kiumbe dhaifu". Mke anastahili azingatiwe na mumewe sio tu kwa hatari za huku nje lakini pia kwa hofu na msongo wa mawazo.

[24] Zaburi 107:9

Mke anaambiwa anyenyekee kwa mumewe na amheshimu. Mwanamke anastahili kukubali uongozi wa mumewe hata kama mumewe siyo mwamini. Akifanya hivi mumewe ambaye hajaamini anaweza kuvutiwa katika wokovu.

Ni muhimu kukumbuka ya kwamba maandiko haya yanatoa amri. Mwanaume hajaambiwa alazimishe sheria kwa mke wake. Mke ameambiwa amtii mumewe lakini mwanaume hajaambiwa amlazimishe mkewe kufanya hivyo. Anaambiwa ampende mke wake na ajitolee kumtunza. Vivyo hivyo, mwanamke hajaambiwa amlazimishe mwamume kumtunza anambiwa amheshimu.

Kipaumbele cha mume si kuweza kutenda kwa mamlaka bali ni kumtunza na kumpenda mkewe. Kipaumbele cha mwanamke ni sio kumlazimisha mumewe kumtunza lakini kumheshimu.

Mtume anaonya mume ya kwamba maombi yake yanaweza kuzuiliwa kama hatamtunza mkewe vizuri. Hiyo inatuambia **tabia zetu katika ndoa inaathiri sana uhusiano wetu na Mungu**.

Mtume Yohana anasema kama mtu hatampenda ndugu yake, hawezi kusema anampenda Mungu (1 Yohana 4:20). Vivyo hivyo kwa maneno ya Paulo na Petro mwanaume asiyempenda mkewe impasavyo hampendi Mungu. Mwanamke asiye mheshimu mumewe hamheshimu Mungu kama inavyostahili.

► Mwanafunzi asome 1 Wakorinths 7:1-5 kwa niaba ya kikundi.

Maandiko haya yanatuambia ya kwamba kuna kusudi moja la ndoa nalo ni kutosheleza hisia za kimwili za kimapenzi katika tendo la ndoa. Mume na mke wamejitoa kila mmoja kwa mwingine na hakuna mwenye haki juu ya mwili wake ila mwenzake. Hii inamaanisha kwamba wanandoa hawapaswi kufanya tendo la ndoa wakati tu mmoja anahitaji lakini pia kwa kujali maslahi ya mwenzake. Aya hii haisemi kwamba moja wao anaweza kulazimisha mwenzake. Lakini mstali huo unasema kila mmoja amjali mwenzake.

Aya hii inasema wakristo wasinyimane. Wakati mchache wa kujizuia na tendo la ndoa uwe ni wakati wa saumu na maombi. Lakini isirefushwe huku ikifanya mwingine kuwa katika majaribu kwa sababu ya haja ambayo haijatimizwa. Wakati mwingine wana ndoa huamua kutengana kidogo kwa sababu ya uzazi au kwa sababu ya masomo. Kabla ya kufanya maamuzi haya ni vizuri wajiulize kama mpango huu uko katika mapenzi ya Mungu. Wanaweza kupata shida kwa sababu ya kutengana kwa muda.

Kusudi moja la ndoa ni kuwa na familia ambayo itasaidia jamii.

► Mwanafunzi asome 1 Timotheo 5:8 kwa niaba ya kikundi.

Aya hii katika Kifungu hiki inaeleza majukumu ya kanisa na washirika kushirikiana na kusaidiana. Jukumu la mtu la kwanza ni familia yake mwenyewe. Mzazi atahakikisha kwamba mahitaji ya mtoto wake yanatimizwa kama vile, malazi, chakula, mavazi na

masomo. Mzazi ni lazima ahakikishe mambo haya anayatenda na sio kuwachia wengine majukumu.

Kushiriki kwa vikundi

Mada ya somo hili italeta mjadala mkubwa.

Mwanafunzi atatakiwa kujaribu kutumia kanuni za kimaandiko katika jibu lake na katika hali yake.

► Ni ukweli upi kuhusu kuhusu ndoa ambao wengi husahau?

► Ni kwa njia gani ambayo kanisa linaweza kuwasaidia vijana wanaopambana na majaribu ya dunia?

► Ni kwa njia gani ambayo washirika kanisani wanaweza kujumuika pamoja (zaidi ya ibada za jumapili tu) ili kuwasaidia watoto kumfuata Kristo.

Maombi

Baba wa mbinguni,

Asante kwa mpango mzuri wa ndoa. Nisaidie niwe mwaminifu kwa mapenzi yako katika kila hatua ya maisha. Nisaidie kuwa mfano mzuri wa uaminifu wa kikristo. Nisaidie niwaambie wengine na niwatie moyo wafuate mapenzi yako.

Nisaidie nitumike kanisani kusaidia familia, vijana, watoto ili wawe na ushujaa katika imani na katika kukutii.

Asante kwa kutupatia nafasi tuwe katika mahusiano ambayo unayabariki.

Amina

Zoezi la somo la 7

(1) Kama hujaolewa, andika aya mbili ya jinsi ambavyo utajitoa kutii kanuni za Mungu katika hali yako na pia katika ndoa baadae. Kama umeoa au kuolewa andika aya mbili na jinsi ambavyo utatii kanuni za Mungu katika ndoa.

(2) Chagua mada moja zaidi na uandike ukurasa mmoja ukieleza jinsi ambavyo mtu anaweza kutumia kanuni za maandiko katika maeneo anakoishi.

Mfano:

- Eleza mahusiano ya wakristo mwanaume na mwanamke ambao wanatazamia kufunga ndoa katika maeneo yako.
- Eleza tabia ya mwanaume au mwanamke anyetaka kuonyesha uaminifu katika ndoa katika maeneo yako.

Somo la 8
Ikolojia ya Mkristo

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Ataelewa kwa nini Mungu aliumba vitu vyote na kwa nini mtu ni wa kipekee kati ya viumbe vyote.

(2) Ataelewa kwamba Mungu amempa mwanadamu utawala wa kutunza uumbaji.

(3) Kujua njia mbalimbali ya kutunza uumbaji wa Mungu.

George Washington Carver, mwanasayansi wa kilimo

George Washington Carver alizaliwa katika utumwa Marekani miaka ya 1860. Baada ya utumwa kupigwa marufuku alitaka sana masomo. Masomo hayakuwa rahisi kwa watoto wenye rangi nyeusi wakati huo lakini mwanamke mmoja mwenye moyo mkuu akamwambia, "ni lazima usome kwa kadri uwezayo baadae urudishe elimu yako yote kwa watu." George akaomba, "Bwana nionyeshe siri za ulimwengu," na akasema Bwana akasema, "wewe ni kijana sana kujua siri za ulimwengu." George baadae akaomba, "Basi Bwana, nionyeshe siri za karanga," na anasema Bwana akaitikia. Karanga ilikuwa ni ya maana sana kwa sababu ililimwa na watu wengi maskini. George alijua ya kwamba kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali kutokana na karanga itaongeza thamani ya karanga. George akagundua bidhaa 300 kutokana na karanga na bidhaa 100 kutokana na viazi vitamu. Akafundisha kilimo katika chuo cha Tuskegee kwa miaka 47 na akagundua njia zaidi za kilimo za kusaidia wakulima na baadae wapate mapato zaidi. George Washington Carver alikuwa Baraka kubwa kwa sababu ya imani yake ndani ya Kristo na uhakika aliokuwa nao katika uumbaji wa Mungu, ukitunzwa vizuri, unaweza kuleta manufaa mengi kwa wanadamu.

Ufafanuzi: Ekologia ni somo ambalo linaelezea jinsi ambavyo viumbe hai hutegemeana vyenyewe na pia na mazingira yao.

Mamlaka ya Mwanadamu juu ya asili

► Mwanafunzi asome Mwanzo 1:1 na 1:26-28 kwa niaba ya kikundi.

Majukumu ya mwanadamu kwa ulimwengu yamethibitishwa na ukweli ya kwamba Mungu aliumba ulimwengu kwa ajili ya utukufu wake (Zaburi 148) na akaweka wanadamu kama waangalizi. Kama watu walioumbwa katika sura na mfano wa Mungu tumeumbwa kutawala kama vile ambavyo Mungu angetawala; "atawale" kulingana na asili ya Mungu. Mzaburi anasema, "umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; umemvika taji la utukufu na heshima.

Umemtawaza juu ya kazi ya mikono yako umevitia vitu vyote chini ya miguu yake" (Zaburi 8:5-6). Wanadamu wana majukumu maalum katika dunia. Wao sio wanyama. Mungu aliwapa binadamu jukumu la utawala juu ya dunia na viumbe vyote vinavyoishi humo.

Mungu aliwaambia Adamu na Hawa waongezeke na wajaze nchi. Akawaambia waitiishe. Hali ya kuitawala nchi ingeendelezwa na watoto wao. Hali ya kuitiisha dunia inahusisha uvumbuzi , kujifunza kuishi mahali papya, kuvumbua na kutumia madini, kuwafuga wanyama, na kukuza teknologia.

Kila kitu kilikuwa kizuri wakati Mungu alipokiumba. Kazi ya mwanadamu ilikuwa ni kutunza bustani ya Eden (Mwanzo 2:15) ilikuwa kazi ya kufurahia na ya urafiki na mazingira. Baada ya dhambi kuingia, mazingira asili yaliharibiwa na laana , na kazi ya mwanadamu ikawa ngumu (Mwanzo 3:17-19). Dunia haina tena ukamilifu wa hapo mwanzo,[25] lakini bado inaonyesha utukufu wa Mungu katika muundo wake.

Baada ya gharika Mungu alisema kwamba mwanadamu wanaweza kula wanyama (Mwanzo 9:3). Mungu alimpa Musa sheriaambayo iliwakataza wanadamu kula wanyama wa aina fulani, lakini agano jipya linatuonesha ya kwamba sasa tumeruhusiwa kula yeyote ambae anayefaa kwa chakula. (Marko 7:19, 1 Timotheo 4:4). Wanyama hawana haki yeyote ambayo inawaweka katika kiwango sawa na mwanadamu.

Jukumu la mwanadamu kuwa mwangalizi wa raslimali

Japokuwa mwanadamu ana mamlaka juu ya uumbaji haimaanishi yeye ni ndio wa mwisho katika mamlaka. Mwanadamu anawajibika kwa Mungu. Dunia na vyote ni mali ya Mungu.

► Mwanafunzi asome Zaburi 24:1 and Zaburi 50:10-11 kwa niaba ya kikundi.

Nchi ni ya Mungu. Mungu aliumba dunia ili adhihilishe utukufu wake. (Zaburi 19:1), na akutane na mahitaji ya mwanadamu (Mwanzo 1:29), na dunia iwe mahali pazuri pa kuishi. Anataka tuifurahie na pia tufurahie vilivyomo. Hatuwezi kuiabudu dunia kwa sababu ni mali na kazi ya mikono ya Mungu. (Warumi 1:25). Pia dunia haipaswi kuharibiwa kutokana na mbaya.

Wakati mwingine watu hupata faida kutokana kwa ardhi na pia wakati huo huo wanaiharibu. Watu huchimba madini na wanaawacha ardhi ikiwa wazi na isiyoweza kutumika tena. Wakati mwingine watu hukata miti na huacha mchanga wazi na unabebwa na maji. Wakati mwingine watu huwawinda wanyama hadi wanaisha katika eneo husika. Watu huweka takataka kwenye mito hadi maji yanachafuka yasiweze kutumika tena.

Mungu aliiumba dunia ili izalishe. Ni makosa watu kutumia ardhi kwa njia ambayo inaiharibu. Matumizi mabaya ya ardhi hayaleti sifa na heshima kwa Mungu.

[25] Warumi 8:18-23

Mungu aliumba ulimwengu ili utumike kwa vizazi na vizazi kwa maelfu ya miaka. Lazima tufikirie kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kizazi kijacho. Mtu anayeharibu mazingira kwa faida ya haraka haonyeshi upendo kwa jirani na kizazi kijacho.

Ungependa kufikiria ya ya kwamba miaka ishirini ijayo mtu atawaibia watoto wako? Kwa hakika hapana. Na bado watu wanawaibia watoto wao kwa kuharibu mazingira ambayo watoto wao wataishi. Kama hauna watoto wako mwenyewe basi jali watoto wa wengine ambao watarithi hiyo ardhi baadae.

Watu wengi hujali sana ile ardhi wanayoimiliki lakini hawajali sana arhi ya umma. Wakristo lazima wawe kielelezo kwa kutunza mazingira, kwa sababu tunajua ni mali ya Mungu na pia tunawajali majirani na kizazi kijacho.

Wakati wengine watu hufikiri, "hii ardhi siyo yangu, kwa hivyo naweza kuacha takataka yangu hapa," au "naweza kata miti yote hapa hata miche ile midogo."

► Mwanafunzi asome Kumbukumbu la Torati 22:6 kwa niaba ya kikundi.

Katika sehemu ya dunia ambako kitabu cha kumbukumbu la Torati kiliandikiwa, kuna ndege ambao wangekamatwa kwa wepesi wakiwa kwenye viota vyao. Ikiwa watu watu watamchukua mama na mayai au Watoto hao ndege hawatendelea kuwepo. Mungu aliwaambia wawachilie wamama ili aina (spishi) hii isiharibiwe. Sheria zetu leo mahali tofauti tofauti tunakoishi mambo yanaweza kuwa tofauti, lakini andiko lasema ni vizuri tutunze rasilimali katika ya ardhi ya umma.

Kutambua Uzuri wa mazingira

Mungu alipoumba mimea, hakuumba tu mboga na matunda, aliumba maua na vitu vingine vya kupendeza, hii inamaanisha kuwa Mungu hajali tu jinsi ambavyo tunatumia ardhi lakini pia anajali uzuri wake (Luka 12:27). Mungu aliumba mazingira yawe ya kupendeza ili watu waishi ndani yake.

Milima, majangwa, mito, mahali tambalale na misitu yote yana uzuri wake asili. Wakati mwingine watu waliozaliwa mahali fulani hawaoni uzuri wa mahali walipo kwasababu ya kuzoea mazingira na pia ni ya kawaida kwao.

► Tafakali ya kwamba wewe ndiwe msanii, fikiri ya kwamba unatumia wakati mwingi kuchora michoro na kupaka rangi na kisha unampatia rafiki. Halafu, wakati mmoja umtembelee na kisha uikute ile zawadi yako chini na imeharibiwa kwa kukanyagwa. Utajisikiaje?

Kuna jamii nyingi ambazo watu hutupa takataka zao chini. Wanang'arisha viwanja vya maeneo ya kwao lakini wanatupa takataka mahali popote. Mitaa ya jirani zao imejaa takataka.

► Ni kitu gani hawa watu wanahitaji kufahamu?

Lazima tutunze maeneo ambayo sisi hushiriki kwa pamoja, kwa ajili yetu na ya wengine pia.

► Kanisa lifanye nini ili kubadilisha walio karibu nalo?

Matumizi ya Wanyama

Wanyama ni tofauti na wanadanu. Hawajaumbwa kwa sura na mfano wa Mungu. Na hawana umilele (Mhubiri 3:21) na hawana haki za wanadamu.

Mungu aliwapa wanadamu ruhusa ya kula wanyama, ambayo humaanisha mwanadamu anaweza kuwinda wanyama kwa chakula na pia awafuge wanyama nyumbani kwa sababu ya chakula.

Katika historia pana ya mwanadamu pia imekuwa kawaida kwa mwanadamu kufuga wanyama ili awafurahie au pia wamfanyie kazi.

► Je Mungu hujali jinsi ambavyo tunatunza wanyama wetu?

► Mwanafunzi asome Mithali 12:10 kwa niaba ya kikundi.

Kifungu hiki kinatueleza kuhusu tabia ya mtu mwadilifu ya kwamba hutunza Wanyama wake kwa njia iliyo bora. Ukatili ni tabia ya watu waovu.

Mtu ambaye anamiliki mnyama lazima ahakikishe kwamba yule mnyama anapata chakula, maji na mahali pa kulala. Kuna kitu abacho si sawa kwa mtu ambaye hatunzi na hajali mahitaji ya wanyama.

Kumbuka wanyama wote ni wa Mungu (Zaburi 50:10-11). Wote wameumbwa na Mungu. Aliwaumba katika maumbile tofauti. Angewafanya wachache kwa ajili ya chakula na kazi, lakini aliwafanya wengi maelfu ya aina na jamii za wanyama pamoja na wadudu na wale ambao hawaonekani kwa macho pia. Maajabu na uwezo wa Mungu unaonekana katika uumbaji wa aina tofauti za wanyama na wadudu.

Wanyama wengine wanauwezo wa kuonyesha shukrani na unyenyekevu kwa wanaowatunza. Wanapenda kutunzwa na wanadamu na wanajifunza kujibu. Wana ya kutosha kujinza mambo mengi. Ni dhahili ya kwamba Mungu aliwafanya ili waweze kwa njia moja amab nyingine wawasiliane na mwanadamu. Mungu aliwapa wanyama heshima maalumu kwa wanadamu (Genesis 9:2).

Mungu aliwaumba wanyama na maarifa na hali ya kuwasiliana na watu. Kuwanyanyasa wanyama ni kutoheshimu mpango wa Mungu. Zaidi ya hayo ni vibaya sana kwa mtu kufurahia kuumiza wanyama na kuwasababishia uchungu.

Maandiko yanatumia sana kielelezo cha mchungaji. Daudi alikuwa mchungaji kabla hajakuwa mfalme wa Israeli. Daudi aliandika Zaburi 23 akilinganisha Mungu na mchungaji mwema, Daudi aligundua ya kwamba Mungu huwatunza watu wake vile ambavyo mchungaji huwatunza kondoo wake. Katika Agano Jipya, watumishi wa Mungu

hulinganishwa na wachungaji (1 Petro 5:2 na kwingine). Kulinganishwa huku kusingeleta maana kama Mungu asingetaka tuwatunze wanyama.

Mafunzo ya Daudi kuwalea wanyama ni sehemu ya mafunzo ya kuwatunza watu. Katika njia hio pia, Mungu ametuamini kutunza ardhi na wanyama na kwa njia hiyo tunaandaliwa tuweze kuwatunza wenzetu.

Umuhimu wa kijani

Kijani kibichi ni rangi ambayo inaonekana sana katika mazingira yetu ispokuwa tu mahali ambapo hakuna maji au udongo mzuri. Ni rangi ambayo huyapa macho yetu utulivu.

Wengi ambao wanaishi katika miji hujisikia vizuri wanapotoka mijini na kwenda katika maeneo yenye kijani cha asili.

Miji mingi haina mimea. Mchanga wake umefunikwa kwa rami au simenti. Mahali pengine wameanza kutengeneza bustani na mahali penye kijani katika miji. Watu kila mahali lazima wafanye bidii kupanda miti na mimea iweze kukua. Wanapaswa kuhifadhi ukijani kwa ajili ya watu kufurahia na hasa kwa watoto kucheza. Familia pia zaweza kuwa na nafasi zenye kijani katika viwanja na nyumba zao kwa kupanda mimea.

Tofauti ya Ikolojia ya mkristo.

Mwanzo wa somo hili kuna maelezo kuhusu ikolojia.

► Kwa nini mkristo atunze ikologia?

Watu wengine hufikiria tunaweza kuokoa dunia kwa kuzuia uchafuzi wa hewa. Sisi wanadamu hatuwezi kuiokoa, japokuwa tunapaswa kufanya sehemu yetu kuihifadhi kwa kadri tuwezavyo. Wakristo wanajua ya kwamba hatuwezi kuitunza kimamilifu dunia inanyoharibika. Mungu hatimaye ataifanya upya dunia (Ufunuo wa Yohana 21:1). Kwa hivyo tunajua ya kwamba hatuwezi kuiokoa dunia.

Wengine hufikiri wanadamu siyo wa muhimu zaidi kuliko viumbe vingine, na ni lazima tuheshimu wanyama kwa sababu haki zao ni sawa na zetu. Wakristo wanajua Mungu alimpa mwanadamu uwezo na mamlaka ya kutawala dunia. Tunajua kwamba mwanadamu ni tofauti na mnyama kwa sababu tumeumbwa katika sura na mfano wa Mungu na tuna roho ya milele. Kwa hiyo, wanyama hawana haki zinazolingana na haki za binadamu.

Wakristo wanaitunza dunia Kwa sababu

1. Ni mali ya Mungu.
2. Wanadamu amepewa wajibu wa kuitunza dunia.
3. Tunajali kizazi kijacho cha wanadamu.

► Nini ambacho ni cha kawaida ambacho kinaonesha ya kwamba wanadamu hawana hali ya kuelewa ikolojia ya mkristo?

► Kama inawezekana kuwa mjadala wa darasa zima: Pata mtu wa karibu akafunge macho yake na aeleze kile anachokiona kila wakati anapotoka kwenye uwanja wa kanisa? Mazingira hapo nje ya kanisa yako namna gani? Kuna takataka? Panaonekana kana kwamba watu wanapajali? Nani anastahili kushugulikia mahali hapo? Eleza jinsi ambavyo washirika kanisani wanaweza kushugulikia hilo jambo. Kwa nini tushugulikie eneo hilo? Utunzaji wao unaweza kuwa na ushawishi gani kwa wengine? Wanafunzi wafikirie hivyo kwa maeneo yao pale nyumbani.

Kushiriki kwa vikundi

► Unapaswa kubadilisha tabia gani?

► Kanisa lako litaleta tofauti gani katika maeneo yake katika mafunzo na kuwa mfano?

► Je jamii yako itabadilishaje mazingira kama watu katika jamii yote wangeshirikiana?

Maombi

Baba wa mbinguni,

Asante Kwa kuumba dunia inayopendeza na rasilimali. Asante kwa kutuamini na kutupa jukumu la kutunza dunia uliyoiumba.

Tusaidie tuishi kwa shukurani kwa ajili ya uumbaji wako wa kupendeza. Tusaidie kufanya kazi pamoja ili tulinde dunia na raslimali na uzuri wake.

Amina

Zoezi la somo la 8

(1) Andika ukurasa mmoja ukieleza mpango wako wa kubadilisha tabia yako kupitia ukweli ambao tumesoma katika somo hili.

(2) Andika ukurasa ukieleza mazoea au tabia mbaya katika maeneo yako. Endelea kwa kusema jinsi ambavyo unapaswa kuwa tofauti. Weka msingi wa mjadala wako katika maandiko na mtazamo wa Biblia.

Somo la 9
Fedha

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Atajitoa kutii kanuni za Mungu za utumiaji mwema wa fedha na rasilimali.

(2) Ataelewa hatari za kiroho zinazohusishwa na Imani zisizo sahihi kuhusu matumzi ya fedha na vile tunaweza kuziepuka.

John Wesley, Mtoaji wa Mkarimu

John Wesley aliishi ungereza katika miaka ya 1703-1791. Alihubiri injili kwa wale watu maskini ambao wasingekubaliwa ndani ya makanisa. Aliishi kwa uangalifu, akitafuta kumheshimu Mungu katika kila jambo la maisha yake ikiwemo matumizi ya fedha. Alifundisha ya kwamba wakristo wakipata fedha, wanapaswa kuweka akiba kwa kadiri wanavyoweza na kisha tena kutoa kwa kadri wanavyoweza. Alikuwa mfano mzuri kwenye nidhamu katika kutumia Kanuni za kifedha. Alipunguza matumizi yake ya mwaka, ili awe na fedha za ziada ambazo angezitoa kama sadaka. Mapato yake yalipoongezeka hakuongeza matumizi yake bali alitoa kila kilichokuwa ziada. Hata ingawa mapato yalikuwa paundi 30,000 katika kipindi chake cha Maisha, wakati wa kifo chake alikuwa amebaki na sarafu chache tu kama mali yake. Wesley alitambua kwamba Mungu aliwaaminia wanadamu kusimamia fedha kwa niaba yake, na Wakristo lazima wafuate kanuni za kimungu wanaposhughulika na fedha.

Utangulizi

Agano Jipya linataja fedha mara nyingi zaidi ya masomo mengine mengi, sio kwamba fedha ni ya muhimu zaidi sana kwa Mungu lakini ni kwa sababu watu wengi wamekuwa na shida na fedha.

Mungu muumba ndiye mmiliki wa watu wote na mali zao. Kama Wakristo sisi ni wa Mungu kwa njia ya kipekee kwa sababu ametukomboa. Kama wakristo tunapaswa kujichukulia kama wasimamizi wa mali ambayo inahitajika kutumika kwa utukufu wa Mungu.

Sio makosa kujifurahisha na vitu vizuri. Mungu anafurahia kutubariki kama tutapokea kila kitu kwa shukrani na unyenyekevu..

Lakini fedha ni mojawabo ya hatari za kiroho kwa watu wengi.

Maonyo ya maelekezo kwa matajiri

►Inamaanisha nini kuwa tajiri?

Kuna sababu tofauti tofauti za mtu kuweza kuchukuliwa kuwa Tajiri.

Ukiwa na fedha ya kuweza kunua zaidi ya mahitaji ya msingi wewe ni tajiri kuliko angalau nusu watu duniani. Watu wengi hufanya kazi kila siku kupata chakula cha siku; kama kitu chochote kitafanyika kuwazuia kufanya kazi, basi hawatakuwa na chakula.

Watu humchukulia mtu kuwa ni tajiri kwa sababu ana mali nyingi kuliko watu wengi katika jamii yake. Watu wanamchukulia kuwa yeye ni wa tabaka la juu la kimaisha. Anaweza kufurahia anasa ambazo watu wengi hawawezi kununua. Ana uwezo wa kushawishi watu walio na mamlaka. Watu wako tayari kumtumikia kwa sababu ya mali aliyonayo.

Biblia ina maagizo na maonyo maalum kwa watu kama hao.

Onyo kali ni sentensi ya Yesu kuwa ni vigumu sana kwa tajiri kuingia mbiguni (Mathayo 19:24).

Tunaweza kuelewa zaidi hatari za utajiri kutokana na ujumbe wa Mtume Paulo kwa matajiri.

► Mwanafunzi asome 1 Timotheo 6:17-19 kwa niaba ya kikundi.

Paulo aliwaonya matajiri kutojichukulia kuwa wenye tabaka la juu kuliko wengine. Kuna jaribu la watu matajiri kujiona kuwa hao ni wenye bora zaidi kuliko wengine. Yakobo anaonya kanisa dhidi ya kufanya kosa hilo hilo, kuheshimu watu kwa misingi ya mali au tabaka (Yakobo 2:1-4).

Mtu tajiri hapaswi kuhisi yuko salama kwa sababu ya utajiri wake bali amtegemee Mungu. Ni vigumu zaidi kwa mtu tajiri kufikiri kwamba anahitaji msaada wa Mungu na wakati ana akiba ya fedha. Kuna jaribio lakutojali mambo ya kiroho kwa sababu ya kutohisi haja ya usaidizi wa Mungu (Kumbukumbu la Torati 8:6-18).

Matajiri wanapaswa kuwa watu watoaji kwa ukarimu na watimize mambo mazuri kwa fedha zao.

Moja ya hukumu za matajiri wa kidunia katika Yakobo 5:5 ni kuwa wanaishi kwa kwa anasa wakati wengine wanateseka. Mengi mazuri yanawezwa kufanikishwa kwa kwa utoaji wa busara. Fedha haiwezi kununua furaha lakini inaweza punguza taabu nyingi. Ni makosa kupuuza mateso ya wengine huku ukiishi Maisha ya anasa.

Kupitia Amosi Mungu alidhihirisha moyo wake kwa haki ya binadamu, (rehema na huruma kwa maskini na wanao dhulumiwa) kwa haya maneno: "lakini hukumu na iteremke kama maji, na haki kama maji makuu" (5:24). Mungu alitangaza hukumu juu ya mafanikio wakati wakati ambapo mafanikio ulisababisha kubweteka, kujifurahisha na kutojali kuhusu mahitaji ya maskini. (Amosi 6:1; 3-6; 8:4-7, 11-12).

Kila mkristo anapaswa kujitoa kuwasaidia maskini na wale wanaodhulumiwa, toa fungu la kumi kusaidia kanisa lako la mahali pamoja, na kutoa ili kusaidia kazi Umisheni ili kueneza injili. John Wesley alitoa sababu tatu ambazo zilisababisha kanisa la wakati wake lisilete mabadiliko katika dunia:

1. Kukosa mafundisho yenye uzima.
2. Kukosa nidhamu na kuwajibika.
3. Kukosa kujitoa kibinafsi

Kupenda Fedha

► Mwanafunzi anapaswa kusoma 1 Timotheo 6:8-10 kwa niaba ya kikundi.

Maonyo kuhusiana na fedha hayawaendei matajiri pekee. Watu wengi masikini wanafikiri kuwa hawawezi kuwa na furaha kwa sababu wao ni maskini. Biblia inatueleza kwamba kupenda fedha ndiyo chanzo cha uovu wa kila aina. Onyo hilo inatumika kwa kila mtu.

Kupenda fedha kamwe hakutoshelezi. Mtu anayependa fedha hatatosheka na kiwango chochote (Mhubiri 5:10). Biblia inatuambia kuwa tunapaswa tuepuke tamaa ya fedha na tutosheke na mahitaji yetu ya msingi (Waebrania 13:5).

Mtu mwenye hamu ya kuwa tajiri ana majaribio mengi ya kuathiri tabia yake. Katika mchakato wa kuwa tajiri mtu anaweza kuiacha imani yake na kupata huzuni nyingi badala ya furaha aliyotarajia.

Wakati mwingine viongozi wa dini huvutia wafuasi wengi kwa kuwaahidi kupata mali. Wao husema kuwa mtu mwenye imani ni lazima awe na mali. Watu wengi katika jamii maskini wanavutiwa na hizi ahadi kwa sababu ya hali ngumu ya maisha. Hawa viongozi huongea na kuhubiri kuhusu fedha kila mara na wanajivuna kwamba wanaweza kuonyesha alama ya mafanikio kama ambavyo watu wa kidunia huonesha.

Biblia inasema kuwa utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Mtu anayetafuta mali kwa njia za kidini yuko katika hatari sawa sawa na mtu yeyote wa kidunia anayetafuta mali. Kanisa ambalo linatoa ahadi ya utajiri huwavutia watu ambao hawajaokoa kwani huvutwa kutokana na matamanio yao binafsi. Hata hivyo Makanisa haya yamejazwa na watu walio na tumaini ambapo hawatapata kitu walichoahidiwa. Watu pekee ambao hutajirika na injili ya mafanikio ni wahubiri wanokusanya sadaka kutoka watu wanaowaamini.

► Mwanafunzi anapaswa kusoma wa filipi 4:10-13 kwa niaba ya kikundi.

Paulo alikuw anashukuru kwa sababu waamini wa Filipi walikuwa wameta sadaka kwa ajili yake. Aliwaambia kuwa alikuwa amejifunza kuridhika katika hali zote, hata njaa. Sentensi hii inatuonyesha kuwa Paulo hakuwa na wingi wa fedha. Alisema kuwa kwa msada wa Mungu angefanya yote. Muktadha wa sentensi hiyo inaonyesha kuwa alimaanisha kuridhika katika hali yote na kuwa mwaminifu kwa Mungu.

Uaminifu

► Mwanafunzi anapaswa kusoma Mithali 11:1 kwa niaba ya kikundi.

Hii aya inaongea kuhusu mizani inayotumika kuuza kitu kwa kipimo cha uzito, kama matunda au mboga au nyama. Wakati mwingine watu wana mizani ambayo imebuniwa

kutoa uzani wa uongo ili kupata fedha za ziada. Aya hii inasema Mungu anachukia kutokuwa mwaminifu.

Watu wengi wamefanya vitu vya kutoaminika kwa sababu ya fedha. Somo linalofuata katika kozi hii ni kuwa mwaminifu.

Kumuamini Mungu

Mtume Paulo aliwaandikia wakristo wa Filipi akiwahidi kuwa Mungu atatimiza mahitaji yao. Hii ni ahadi ya ajabu. Tunapaswa kuangalia kifungu cha Biblia pale inapotokea ili kuelewa hali iliyokuwapo.

► Mwanafunzi asome Wafilipi 4:15-19 kwa niaba ya kikundi.

Kanisa lilimtumia Paulo msaada wa kifedha. Alisema ilikuwa ni dhabihu kwa Mungu. Aliwaahidi kuwa Mungu atakutana na mahitaji yao. Hakuwahidi ongezeko kubwa la fedha zao.

Ahadi haikuwa kwa watu ambao hawahajibiki au wabadhilifu. Ilkikuwa ni ya watu ambao walikuwa wasimamizi wa fedha zao kulingana na vipaumbele vya kiroho.

► Mwanafunzi anapaswa asome Mathayo 6:25-33 kwa niaba ya kikundi.

Yesu aliongoea kuhusu namna ambavyo Mungu anawalisha ndege wa angani na kuyavalisha maua na akaahidi kuwa atashughulikia mahitaji yetu. Anatuambia tusiwe wenye hofu kuhusu kuishi kwetu. Ametuahidi kuwa tukitanguliza ufalme wa Mungu atakutana na mahitaji yetu.

Watu wengi wana hofu sio kuhusu leo bali siku zijazo. Mungu hajaahidi kutoa kila kitu kabla ya wakati husika. Kumbuka katika Agano la Kale wakati mana ilipoanguka, ilikuja kila siku (Kutoka 16). Vivyo hivyo, Yesu akasema tuombe kwa ajili ya "mkate wetu" wa kila siku (Mathayo 6:11). Mungu anataka tumuamini kila siku.

Yakobo alisema kuwa Mungu amewafanya maskini "matajiri kwa Imani" (Yakobo 2:5). Watu maskini wana fursa nzuri ya kumtegemea Mungu kuliko watu ambao wanautoshelevu wa kifedha.

Kumuamini Mungu hakumaanishi kuwa hatuwajibiki. Mara nyingi Mungu ametupatia mahitaji yetu kupitia kazi tunazofanya. (Waefeso 4:28). Kama mtu hayuko tayari kufanya kazi, asitarajie Mungu atampa mahitaji yake, na watu wengine wasilazimike kumpa. (2 Wathesalonike 3:10).

Tusitarajie riziki toka kwa Mungu kutafanya kuwa matajiri. Mungu anawabariki watu wachache na utajiri, lakini utajiri siyo mapenzi ya Mungu kwa kila mtu. Mtu ambaye ana shauku kubwa ya utajiri atakuwa na shida za kiroho.

Rasilimali Zinazozalisha

Rasilimali zinazozalisha kazi ni vitu ambavyo watu wanavyo kwa ajili ya kuzalisha. Mfano ni ardhi, vifaa vya matumizi au kompuyta. Mtu anaweza kutumia rasilimali zinazozalisha ili kupata faida lakini lazima azitunze bila kuziuza vinginevyo uzalishaji utakoma. Biblia inataja kuhusu rasilimali zinazozalisha katika Mithali 14:4, "Zizi ni safi ambapo hapana ngo'mbe; bali nguvu za ng'ombe zaleta faida nyingi".

Mtu aliye maskini huenda asielewe dhana ya rasilimali zinazozalisha. Kwa mfano anaweza kudhania kuwa rafiki yake ana fedha nyingi kwa sababu ana vifaa vya bei ghali mno, au compyta, au gari. Anafikiri kuwa rafiki yake au mtu wa jamii yake aliye na kitu kama hicho anapaswa kumpa fedha wakati anahitaji. Hata hivyo chochote kati ya vitu hivi vinaweza kuwa baadhi ya rasilimali zinazozalisha ambazo haziwezi kubadilishwa kuwa fedha bila kumfanya mtu apoteze mapato yake.

► Ni mifano gani mingine ya rasilimali zinazozalisha ambazo zinapatikana katika eneo lako?

Mtu asipoelewa namna rasilimali zinazozalisha zinavyofanya kazi kwa wengine, anaweza asielewe kwamba rasilimali kama hiyo ingeweza kufanya kazi kwake. Hawezi kujua ni nini hasa anachohitaji auni aina gani ya usaidizi ambao anahitaji ili kubadilisha hali yake. Anaweza kuueleza msaada kama hatua ya haraka na fupi ambayo inasaidia katika harakati zake za kila siku badala ya mabadiliko halisi ya maisha.

Sababu moja ya umaskini ni ukosefu wa rasilimali zinazozalisha. Kama mtu ambaye yuko kwenye umaskini haoni haja ya kupata, kudumisha na kuweka akiba ya rasilimali zinazozalisha, hataweza kuondolewa katika hali ya kutegemea msaada.

Katika mila fulani, ni vigumu sana kwa mtu kuweka akiba na kutengeneza rasilimali za zinazozalisha kwa sababu wale wanao mzunguka wanatarajia yeye awashirikishe kila kitu. Hawaelewi kwa nini anakusanya fedha wakati mtu mwingine anahitaji fedha. Wanatarajia kugawana alichonacho hata kama wamekuwa sio wawajibikaji.

Mkristo ni lazima aheshimu matarajio ya mila zake lakini pia atumie kanuni za Biblia. Maandiko yanatueleza kuwa hatulazimishwi kumsaidia mtu ambaye hawajibiki (2 Wathesalonike 3:10). Mtu akitoa rasilimali zinazozalisha na kisha akasaidia wengine ambao hawawajibiki, wote watakuwa maskini.

Maandiko yanadokeza aina ya mafanikio ambayo Mungu hutoa ni kwamba watu wawe na rasilimali zao za zinazozalisha. Nabii Mika alisema kuwa jamii iliyobarikiwa, kila mtu atamiliki vikamilifu "mzabibu wake na mtini" (Mika 4:4). Hiyo inahusu mali ya kibnafsi inayomilikiwa na njia za uzalishaji. Sehemu zingine kilimo kinaweza kisiwe njia halisi ya uzalishaji lakini kanuni kuu ni kuwa watu waliobarikiwa wanapaswa wawe na kile wanachohitaji kuzalisha rasilimali.

Mara nyingi watu maskini ambao wanakuwa wakristo huanza kustawi zaidi, sio kwa sababu ya baraka za moja kwa moja kutoka kwa Mungu lakini kwa sababu ya mtindo wao mzuri

wa maisha. Wanaacha kuharibu fedha kwa vitu kama pombe, kucheza kamari na aina mbaya ya burudani. Wanakuwa wafanyakazi wazuri na sifa zao zinakuwa bora. Wanaposaidia Huduma, Mungu anawabariki. Mara nyingi kizazi cha pili cha familia ya kikristo wako katika hali nzuri kulio kizazi cha kwanza.

► Ni njia zipi ambazo watu katika mazingira yako wanaweza kufanya kazi na kuweka akiba ili kuboresha hali yao ya kifedha?

Kamari

Kamari ni kuhatarisha fedha katika jaribio la kupata fedha bila jasho. Mtu yeyote anayeshinda anachukua fedha kutoka kwa mwingine ambaye amepoteza, bila kutoa chochote kama malipo. Watu wengi huwa waraibu wa kucheza kamari, hupoteza fedha zao, na hushindwa kutunza familia zao. Watu wengi wametumia fedha ambayo ilikuwa ya mtu mwingine kucheza kamari wakitumaini kushinda ili waweze kulipa deni lao. Kuna watu wengi wako jela kwa kuiba ili wacheza kamari. Watu wengi ambao ni maskini hucheza kamari kwa sababu wanafikiri hawana tumaini ya kubadilisha hali yao ya maisha ila tu kupata bahati na kushinda fedha.

Kamari ni kinyume cha kanuni nyingine za kikristo:

1. Kanuni ya kupata mali kwa kufanya kazi (Waefeso 4:28)
2. Kanuni ya kuridhika (1 Timotheo 6:6)
3. Kanuni ya kupanda na kuvuna (Wagalatia 6:7).

Pia, Mungu anataka tutoe huduma au uzalishaji wa bidhaa kwa faida badala ya kuchukua fedha kutoka kwa mtu kwa bahati. Kamari inadhurukwa sababu inalevya na inaongeza visa vya uhalifu.

Kamari ni kinyume na kumtegemea Mungu. Mtu anapaswa kujiuliza, "Je namwamini Mungu kwamba ananitunza?" "Naweza kumuomba Mungu ili anipatie utoshelevu wangu?" "Je ninaamini kuwa njia ambayo Mungu ananipa utoshelevu wangu ni kwa kuhatarisha fedha kwa kucheza kamari, nikitumaini kuchukua fedha kutoka kwa mtu mwingine?" "Je ninafikiri kuwa Mungu atanizawadia nikicheza kamari kwa kunifanya nishinde fedha nyingi?" Mtu anayecheza kamari hamtumaini Mungu katika hali yake ya kifedha. Tunapomwamini Mungu kiukweli, tunatii maagizo yake yaliyo wazi kwetu, tukijua ya kwamba atatupatia mahitaji yetu kwa uaminifu tunapotii.

Deni

Mtu anapokopa fedha, yeye hudhani kuwa ataweza kulipa mkopo kutokana na fedha apatazo siku za mbeleni. Kwa hivyo kukopa ni kutumia Fedha ya siku za mbele hata ingawa mahitaji mapya yatakuwepo.

Biblia inasema kuwa mkopaji ni mtumwa wa akopeshaye (Mithali 22:7). Mkopaji anajenga wajibu ambao unapunguza uhuru wake.

Aina fulani ya kukopa ni mbaya zaidi kuliko nyingine. Mtu anapokopa fedha kwa sababu ya mahitaji ya msingi kama vile chakula, anajitia katika hali mbaya zaidi. Chakula kitatumika, na mkopo bado utabaki,na atakuwa maskini zaidi kuliko alivyokuwa awali.

Mtu anapokopa fedha kwa sababu ya kitu kisicho cha lazima, kama vile mapambo ya kibinafsi, mavazi yasiyohitajika, burudani, au mapambo ya nyumbani, anatumia fedha zake za baadaye. Anajipunguzia uhuru wake wa siku za baadaye; siku za baadaye hataweza kuchagua kununua vitu kwa sababu fedha imeshatumika.

Baadhi ya biashara hukopesha fedha kwa riba iliyo juu sana. Watu ambao wamekopeshewa muda usio mrefu hujikuta wanadaiwa fedha zaidi kuliko zile walikopshewa. Baadhi ya maduka yanauza vitu kwa mkopo kwa riba ya juu sana. Watu hatimaye hulipa kwa bei ya juu sana kwa vitu ambavyo vimenunuliwa kwa mkopo kwa sababu hawako tayari kusubiri mpaka wapate fedha za kutosha kulipa kwa bei ya kawaida.

Wakati mwingine watu hukopa kwa sababu yakutaka kuwa na harusi ya kifahari kama inavyotarijiwa na tamaduni zao. Wanaanza ndoa yao kwa deni kubwa. Kanisa kama familia ya imani inapaswa kusaidia washirika wake kujenga tamaduni mpya au kutafuta mbinu za kufanya harusi iwe ya kupendeza bila kuwa na gharama kubwa kupita kiasi.

► Mwanafunzi anapaswa kusoma Warumi 13:7-8 kwa niaba ya kikundi.

Mistari hii inateleza kuwa tulipe kile tunachodaiwa na wengine. Tunadaiwa heshima na utiifu kwa mamlaka. Tunadaiwa kodi na serikali. Sentensi ya kwanza ya aya ya 8 inafupisha sentensi katika aya ya 7. Hatupaswi kushindwa kumpa yeyote kile tunachostahili kumpa. Hii haimaanishi kwamba tusikope kamwe, kwa sababu tukilipa kama ilivyokubaliana na mkopeshaji, hatujashindwa kumpa kama inavyotakiwa.

Ni wizi kwa mtu kukopa kama hana nia ya kulipa, au kukopa na kuamua baadaye kutolipa. (Zaburi 37:21).

Sheria za Agano la kale kwa sehemu kubwa zinaelekezwa kwa taifa la Isreal kama jamii ya wakulima. Watu wengi waliishi kwa kutegemea ukulima na kuzalisha waliyohitaji nyumbani kwao. Familia zilimiliki ardhi moja kwa vizazi vingi. Kwa hivyo ilikuwa ni vigumu kwa mtu kukopa fedha kununua ardhi au kuanzisha biashara. Kama mtu alikopa fedha, ilikuwa ni kwa sababu alikuwa katika hali mbaya na alihitaji fedha kwa mahitaji ya kimsingi. Mungu alitaka Israel wawe familia ya Imani ambayo ilishughulikia washirika wake. Mungu aliwaambia wakopeshe fedha bila kutoza riba (Kutoka 22:25). Sifa moja ya mtu mwadilifu inavyoelezwa katika Zaburi 15 ni kuwa hakopeshi fedha kwa riba.[26]

Sio makosa kwa mwekezaj kuzalisha riba anapokopesha mtu fedha kumsaidia kuanza biashara.[27] Riba ni zawadi ya mwekezaji kwa kufanya biashara iwezekane.

[26] Ezekieli 18:5-9 inafanana na Zaburi 15.
[27] Mathayo 25:27

Watu wanaofanya biashara na maskini hawapaswi kufikiria tu jinsi ya kupata faida. (Mithali 22:16a). Ni makosa kuuza vifaa vyenye viwango duni au kutoza bei zisizo za haki, kwa sababu maskini hawana chaguzi. Ni makosa pia kubuni mikopo au kuuza vitu kwa mkopo kwa kusudi ya kutengeneza faida kubwa kutoka kwa watu ambao wamekopa kwa sababu ya hali ngumu. mfanyabiashara anapaswa kutafuta njia ua kuboresha hali ya wateja wake.

Nabii Ezekieli alisema kwamba dhambi ya Sodoma haikuwa tu usherati lakini pia watu walioishi kwa anasa na " walishindwa kuimarisha mkono wa maskini" (Ezekieli 16:49). Mungu anatupa wito sio tu kuwasaidia maskini, bali kusaidia kwa njia ya mikakati ya kuwafanya wawe na nguvu.

Sheria za Mungu kwa Israel ya kale zinatuonyesha vipaumbele vyake. Leo sheria za mataifa yetu sio sawa kama sheria Mungu alizowapa Israel, lakini mapenzi na kanuni zake Mungu hazijabadilika. Kanisa linapaswa kutafuta njia ya kuwapa nguvu maskini, kwanza kujali familia ya Imani, halafu kuleta tofauti katika jamii.

Bajeti

Watu wengine hutumia fedha zao zote mara tu wanapopewa. Mara nyingi wanateseka na ukosefu wa mahitaji kabla ya kupata fedha tena. Hawawezi kuwajibika kwa wengine.

Bajeti ni mpango wa kudhibiti matumizi ya kawaida. Watu wengi hupata matumizi yasiyotarajiwa nyakati za usoni, na hivyo inapaswa kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya mahitaji ya siku za mbele. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa amepanga nyumba na anaweza kuwa analipa kwa mwezi au mwaka. Anahitajika kutunza mara kwa mara sehemu ya mapato yake ili aweze kulipia kodi ya nyumba wakati unapofika. Kama kodi yake ya nyumba ni ya mwaka, atakuwa ameshikilia baadhi ya fedha kwa muda mrefu, na kuna jaribu la matumizi, lakini anapaswa ahifadhi hizo fedha na afikirie kwamba tayari zimeshatumika.

Fedha za kwanza kuhifadhiwa inapaswa iwe fungu la kumi (Methali 3:9-10). Unapaswa ujitoe kutoa asilimia 10 ya mapato yako kwa ajili ya huduma. Usisubiri kuona kama una fedha ya ziada ya fungu la kumi baada ya matumizi. Mungu atabariki uaminifu wako.[28]

Baada ya mahitaji ya msingi kushughulikiwa na mapato yaliyosalia, mtu lazima ahifadhi fedha kwa mambo ya dharura. Anapaswa kuhifadhi fedha kwa sababu ya kujiboresha, kama vile kutunza fedha kununua nyumba yake binafsi. Anapaswa pia kujaribu kuwekeza fedha katika kuongeza mapato yake. Kununua vifaa ambavyo vitamsaidia alipwe zaidi sehemu yake ya kazi ni mfano wa uwekezaji mdogo.

Mtu ambaye anarasilimali za kuzalisha (kitu kinacho saidia uzalishaji) kama vile gari au jengo ni lazima fedha ikadiriwe (bajetiwe) kwa ajili ya matengenezo ya rasilimali. Kama mtu atapata faida na gari lake lakini hatunzi fedha, hatakuwa na uwezo wa kulipia matengenezo makubwa ya gari au kunua lingine, na faida yake mwishowe itaisha.

[28] Mfano wa kina kuhusu fungu la kumi inafanywa katika kozi ya Shepherds Global Classroom *Mafundisho na Mazoezi ya Kanisa*, inapatikana kwa https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mtu asiyetengeneza bajeti kwa mara nyingi hataweza kutimiza majukumu yake. Anaweza kutegemea wengine na kushindwa kusaidia wengine. Hali yake haitaimarika kwa sababu hajawekeza kwa njia yeyote.

Yesu alisema kuhusu Msamaria Mwema aliyemsaidia mtu aliyejeruhiwa.[29] Tazama kuwa Msamaria alikuwa na fedha na punda wa kutumia kumbeba aliyejuruhiwa. Ingekuwaje kama Msamari mwema angekuwa ameuza punda wake na kutumia fedha zote? Hata kama angekuwa na shahuku ya kusaidia, angepungukiwa na uwezo wake wa kuingilia kati kwenye hiyo hali.

Kufanya bajeti kunasaidia mtu kujiandaa kwa mahitaji yake, kuwajibikia kwa wale ambao wanamtegemea, kuwekeza kwenye Maisha yake ya baadaye, kabiliana na dharura, na kusaidia huduma.

Familia ya imani

Katika siku za mwanzo za kanisa, muda mfupi baada ya Pentekoste, waumini walijitoa sana kwa familia ya Imani na wakahakikisha kuwa mahitaji ya kila mtu yalitimizwa. Walishirikiana mali zao, na hakuna yeyote aliyesema kuwa chochote kile ni chake. Wengi wao waliuza mali zao na wakatoa fedha kwa kanisa (Matendo ya Mitume 2:44-45). Hata ingawa hatutarajii kuwa Maisha katika kanisa yatakuwa sawa kama wakati huo, tunaona kuwa kanisa likiwa katika ubora wake kama kuna ukarimu na kujitolea kulinda familia.

Waamini wa Thesalonike walihakikisha kuwa washirika wote walipata chakula lakini baadhi yao hawakupenda kufanya kazi. Hao watu walikuwa wanaishi kwa anasa, wakitegemea ukarimu wa kanisa. Paulo hakuambia kanisa kuwa walifanya makosa kuwajali wanafamilia bali alisema mtu asipewe chakula kama hawakuwa tayari kufanya kazi (2 Wathesolanike 3:10). Kwa wengine, kazi inaweza isiwe ya kuajiriwa kwa mshahara, bali ni ya kusaidia waumini kama inavyohitajika. Watu wengine hawana uwezo wa kuajiriwa, lakini kila mtu anaweza kufanya kitu kusaidia.

Katika barua zingine Paulo alitoa maelekezo ya kusaidia wajane na kuwapa msaada Wachungaji (1 Timotheo 5:3-18, Wagalata 6:6).

Kila mkristo anapaswa kuwa sehemu ya familia ya ndani ya imani na anapaswa kujitolea kusaidia washirika wenye mahitaji na kusaidia huduma.

Kushiriki kwa Vikundi

► Ni kwa insi gani kanisa linaweza kuungana kwa pamoja kushughulikia mahitaji kanisani huku wakihitaji watu wawajibike?

► Ni fursa gani zipo katika mazingira yako kwa watu wakanisa kufanya kazi pamoja kujenga rasilimali za kuleta mapato?

[29] Luka 10:25-37

Maombi

Baba wa mbiguni,

Ahsante kwa ahadi yako ya kukutana na mahitaji yangu. Nisaidie niwe mwaminifu kwa majukumu yangu kwa kujikimu kwangu na wengine wanao nitegemea. Nisaidie niwe mkarimu na kile nilichonacho. Nisaidie kutosheleza mahitaji ya wengine kwa njia ya hekima.

Nakuomba baraka za kifedha, lakini zaidi ya yote nataka kuweka vipaumbele vya kiroho na nitosheke kwa sababu ya uhusiano wangu na wewe.

Amina

Zoezi la somo la 9

(1) Kwa maombi zingatia kanuni za maandiko zilizotolewa katika somo hili. Jibu kila swali lifuatalo kwa maandishi:

- Nimekumbana na majaribu gani linapokuja kwa swala la fedha na rasilimali?
- Kwa sasa napataje fedha na/au rasilimali?
- Ninatumiaje na kusimamia fedha na/au rasilimali?
- Inamaanisha nini kumuamini Mungu na fedha na/au rasilimali?
- Nina rasilimali zipi za kuleta mapato?
- Kuna rasilimali za kuleta mapato ninapaswa niwe na mpango wa kuzipata siku zijazo? Na kama ni hivyo, ni gani?
- Ni kwa njia gani nimekuwa na matumizi mabaya ya fedha na/au rasilimali?
- Nitarekebisha kwa namna gani utumiaji wowote mbaya wa fedha au/na rasilimali uliotajwahapo juu?

(2) Andika wasilisho la ukurasa mmoja wa kanuni kutoka kwenye somo hili, ukifanya matumizi mahususi katika mazingira yako. Watu katika mazingira yako wanahitaji kuelewa nini kuhusu ufahamu wa Kikristo kuhusu fedha?

(3) Kariri Mithali 3:13-17 na uandike tafakari ya aya moja juu yake. Mwanzoni wa darasa lifuatalo, andika kifungu hiki kutoka kwenye kumbukumbu na umpe kiongozi wa darasa aya hiyo.

Somo la 10
Uaminifu

Lengo la somo

Mwisho wa somo hili mwanafunzi ataweza kujitoa kuwa mwaminifu kabisa katika hali zote na wakati wowote.

Abraham Lincoln, Mtu Mwaminifu

Abraham alifanya kazi katika duka. Siku moja alitambuwa ya kuwa hakumrejeshea mteja chenji halisi. Mteja alikua ameshaondoka. Aliishi maili kadhaa nje ya mji huko vijijini, na Abraham alijua ya kwamba hatamuona tena hivi karibuni. Hata ingawa fedha ilikuwa kidogo alikuwa na wasiwasi kuwa mteja huyo anaweza kuzihitaji. Alitaka pia kuhakikisha kuwa mwanamke asije akafikiri kwamba alikuwa amechukua fedha yake kwa makusudi. Duka lilipofungwa baada ya kazi, Abraham alitembea maili kadhaa kwa ajili ya kurudisha fedha kwa yule mteja. Kwa sababu ya uangalifu wake katika hiyo hali na hata nyakati zingine, marafiki zake walimuita "mwaminifu Abe." Baadaye alikuwa mwanasheria na kisha akajihusisha na serikali. Uaminifu wake uliheshimiwa na hatimaye akahudumu kama Rais wa Marekani.

Asili Ya Mungu

Biblia inatueleza kuwa Mungu hawezi kusema uongo (Tito 1:2,Waebrania 6:18). Asili yake daima ni thabiti na haibadilki (Yakobo 1:17). Mungu hasemi tu ukweli inapo mletea faida. Hasemi uongo ili kupata matokeo mazuri. Tunaweza kuwa na Imani kuwa neno la mungu ni kweli kabisa na la kutegemewa. Ukweli wake unatupa Uhakika (Zaburi 40: 11,91:4).

► Je, mahusiano yako na Mungu yataathiriwa vipi ikiwa humwamini kwa kusema ukweli nyakati zote?

Fikiria kuhusu vile ukweli ni wa muhimu katika uhusiano wetu na mungu. Mungu anatuita tujitoe kwake kabisa. Hatuwezi kufanya hivyo ikiwa hatumwamini kabisa.

Viwango vya Mungu vya Kweli

Mungu anataka tuseme ukweli kila wakati. Mtu anayesema uongo sio mwadilifu machoni pa Mungu (Mithali 12:17).

Wakati mwingine watu husema uongo kushinda kesi mahakamani. Watu walio na fedha wanaweza kumlipa hakimu kukubali uongo ili waweze kuchukua mali kutoka kwa wengine (Yakobo 2:6). Watu wenye mali huepuka hukumu na kuwafunga watu wasio na hatia kwa kulipa hongo ili kuanzisha uongo. (Yakobo 5:1, 6).

Ni dhambi kushuhudia uongo, hata kama ukifiria sababu yako kuwa ni sawa. Biblia inashutumu mashidi wa uongo na hairuhusu ubaguzi.[30] Watu wengi wanafikiri kuwa unaweza kusema uongo kama uongo utasaidia kuleta mema bila kusasabisha madhara. Lakini Biblia haijatupa chaguo hilo. Hatujaelezwa kwenye maandiko kwamba kuna wakati tunaweza kusema uwongo.

Wakristo wanapaswa kuongea ukweli bila kujali mazingira. Ukweli ni muhimu kwa uhusiano yetu.

Waefeso 4:15 inasema kwamba kusema ukweli ni muhimu kwa ukuaji hadi ukomavu wa kiroho.

Wakolosai 3:9 inasema kwamba kusema uongo ni sehemu ya maisha ya dhambi ambayo tumetoka.

Mungu atawahukumu wale wasemao uongo. Waongo Wamejumuishwa kwenye orodha ya watenda dhambi wabaya waliohukumiwa na sheria ya Mungu (1 Timotheo 1:10, Ufunuo 22:15). Wasema uongo wote watatupwa kwenye jehanamu ya moto (Ufunuo 21:8). Waongo hawataingia katika mji wa Mungu (Ufunuo 21:27).

Kutumia Ukweli Kwenye Biashara na Mahusiano

► Mwanafunzi anapaswa kusoma Mithali 11:1 kwa niaba ya kikundi.

Mstari huu unaongea kuhusu mizani ambazo hutumika kupima uzito wa kitu, kama vile matunda au mboga au nyama. Wakati mwingine watu wana mizani ambazo zimeundwa ili kutoa uzito usio sahihi ili mfanyabiashra aweze kupata fedha za ziada. Huu Mstari unatukumbusha kuwa Mungu anachukia vitendo vyote vya kutokuwa na uaminifu.

Ni makosa kwa mtu kuuza kitu huku akisema uongo kuhusu hali ya kitu au kuficha kasoro zake. Ni makosa kusema uongo unapoeleza mtu kiasi cha fedha ulichonunulia ili kukiuuza kwa bei ya juu.

Sio vyema kutia sahihi ya jina kwa kitu ambacho sio kweli ili kuepuka kulipa fedha. Sio vyema kwa mtu kumsaidia mwajiri wake kudanganya watu kwa faida.

► Je, ni aina gani mbalimbali za ukosefu wa uamanifu umewahi kuziona?

Biblia inasema kuwa watu waovu hukopa na hawalipi (Zaburi:21,Mithali 3:28). Baadhi ya watu hukopa na wanahisi kuwa hawana jukumu la kulipa deni lao. Biblia inasema kuwa lazima tuhakikishe kuwa hatukosi kuwapa wengine kile wanachotudai (Warumi 13:7-8).

Uaminifu inamaanisha kuwa unatimiza ahadi yako na kujitoa. Zaburi 15 inaeleza mtu aliye na uhusiano mzuri na Mungu. Sifa moja ni kuwa huyo mtu anatoa ahadi na kuitimiza hata ikiwa ni gharama kwake (Zaburi 15:4).

[30] Kutoka 20:16, Mithali 6:16-19, 14:25, 19:5, 9

Ni kukosa uaminifu wakati mtu hafanyi kazi kama navyostahili kwa mtu aliyemwajiri (Waefeso 6:5-6).

Ni Makosa kwa mfanyakazi kumuibia mwajiri wake (Tito 2:9-10).

Ni makossa kutoa risiti za uongo kuonyesha kitu kina gharama ya juu kuliko ilivyokuwa. Ni makosa kwa mfanyakazi au wakala kusema uongo kuhusu bei ya kitu ili aweze kupata kiasi fulani cha fedha.

Ni makosa kwa mwajiri kuwanyima wafanyakazi mishara iliyoahadiwa (Yakobo 5:4).

Ni makossa kuchukua kitu ambacho mtu mwingine amekipoteza kwa bahati mbaya. Unapaswa kukirudisha kwa mmiliki kama inavyowezekana (Kumbukumbu la Torati 22:1).

Kama wewe ni meneja wa rasilimali za mtu mwingine (Kama vile mwajiri au huduma), ni makosa kutumia fedha au vitu vya kazi kwa sababu za kibinafsi kama haujapewa ruhusa.

Kielezo cha Changamoto za kitamaduni kwa Uaminifu

Katika baadhi ya jamii watu wanaishi chini ya uangalizi wa chifu. Watu ni waaminifu kwa chifu, na chifu anatarajia kuwasaidia kwa kila hitaji. Katika hizi jamii watu wengi hawana mali ya kibinafsi. Rasilimali muhimu kama vile ardhi ni mali ya jamii. Viongozi wanahitajika kusimamia rasilimali kwa faida ya kila mtu. Mtu anapokuwa na hitaji, anahisi kuwa ana haki kuchukuwa chochote atakacho kutoka kwenye rasilimali ya jamii.

Gerald alizaliwa Kijiji cha msituni. Familia yake na nyinginezo karibu nao walilima mazao ya chakula kwenye ardhi iliyokuwa mali ya Kijiji. Walipata rasilimali kwenye msitu. Hakuna yeyote aliyemiliki ardhi kibinafsi hata sehemu ambazo nyumba zilikuwa zimejengwa. Familia zilisaidiana kulipotokea shida. Chifu alikuwa kama baba kwa Kijiji. Watu walitarajia kuwa atatimiza mahitaji yao.

Wakati Gerald alipokuwa kijana alipata kazi na kampuni iliyokuwa inakata miti kutoka kwenye msitu. Aliondoka kijijini kuenda kuishi karibu na sehemu ya kazi. Alilipwa mshahara kila mwezi. Kuna wakati ambao hakukuwa na chakula cha kutosha kwa sababu hakukuwa na mazoea ya kupanga bajeti ya mshahara wake. Alitarajia mwajiri wake ampe chakula na alishangaa wakati mwajiri alipomuambia kuwa ni jukumu lake kama mfanyakazi kununua kila kitu kutoka kwenye mshahara wake. Wakati dada yake na Gerald alipohitaji huduma za daktari na Gerald alimuomba mwaajiri fedha kwa ajili ya dada yake. Geraald alikasirika pale mwajiri aliposhindwa kuwa wa msaada kwake. Gerald alifikiri kuwa mwajiri wake angemsaidia katika shida zake, lakini mwajiri akasema mshara ndio jukumu lake la pekee kwa Gerald. Wakati Gerald alipoacha kazi, aliiba baadhi ya vifaa vya kazi ili avipeleke kwenye Kijiji, kwa sababu alihisi kuwa mwajiri hakumsaidia vya kutosha.

Gerald baadaye alihamia mjini na mke na mtoto wake na akapata kazi kwenye duka la kuuza vitu vya chakula. Gerald alimuoma mwajiri wake kulipa karo ya shule ya mtoto wake lakini mwajiri hakufanya hivyo. Wakati fulani Gerald hakuwa na fedha za kutosha za kununua kila kitu ambacho familia yake ilikuwa inahitaji. Kwa sababu alifanya kazi kwenye

duka ambalo lilkuwa linauza chakula, alidhani kuwa anastahili kuruhusiwa kuchukuwa chakula kutoka kwenye duka kwa ajili ya familia yake. Alijua kwamba mwajiri wake hangekubali, kwa hivyo akachukua chakula kwa siri.

Kuna baadhi ya wafanyikazi hawaelewi mipaka ya ahadi ya waajiri. Wanadhani kuwa waajiri wanajukumu la mahitaji yao yote. Wanaomba misaada ya aina nyingi zaidi ya mishara ya kazi yao. Wasipopewa kile wanahitaji, wanaona kuwa wana haki kuiba kwa sababu wanahisi ana deni kwao kwa vitu wanavyohijitaji.

► Mwanfunzi asome Tito 2:9-14 kwa niaba ya kikundi.

Mistari hii inatueleza kuwa mfanyakazi hapaswi kuiba kutoka kwa mwajiri wake. Mstari wa 10 unasema kuwa mwaminifu kunafanya Mafundisho ya Kikristo yawe na maana sana. Mistari ya mbele inaeleza maisha ya mtu aliyebadilishwa kwa neema.

Kutegemewa

Uaminifu sio tu kuhusu fedha na kumiliki.

Carlos aliahidi rafiki wake kwamba atamkuta 8.00 asubuhi. Hata hivyo alilala kwa kuchelewa na ikamchukuwa muda kupata chakula cha asubuhi. Alichelewa zaidi ya saa moja. alimwambia rafiki yake kuwa dereva wake amechelewa kuja kumchukua. Rafiki yake hakushangazwa. Marafiki wa carlos walijua kuwa yeye sio mwaminifu kwa ahadi zake.

Carlos hakukuwa na uamninfu kwa njia mbili:

1. Hakuweka au kuwa muaminifu kwa ahadi zake
2. Alisema uongo kuhusiana na sababu zilizomfanya achelewe

Watu wanaweza kukuamini unaposema kuwa utafanya kazi au utakuwa sehemu fulani? Je unajiamini unaposema haya? Unapoahidi kitu, unaahidi kuwa utafanya kila uwezalo kutimiza? Ni makosa kuahidi kitu halafu ukose kufanya bidii kutimiza ahadi yako.

Unaposhindwa kutimiza ahadi, ni vyema kuomba msamaha. Usiseme uongo kuhusiana na sababu zilizofanya ushindwe kutimiza ahadi.

Ni makosa kulaumu wengine kwenye shirika au kampuni kwa sababu ya makosa yako. Watu ambao mnafanya kazi nao kwa karibu hawatakuamini wakijua ya kwamba utasema uongo kuhusu makosa yako.

Kiongozi mwaminifu hawapatii watu wazo lake kwa kuwaambia mambo ambayo si ya kweli. Steven Covey aliandika kuwa "Uongozi ni kupata matokeo kwa njia inayohusisha uamininifu."[31]

[31] Stephen M. R. Covey. *The Speed of Trust: The One Thing That Changes Everything*. (New York: Free Press, 2006).

Sababu ya Uhusiano

Watu wengi wanaamini kuwa ni makossa kusema uongo kwa marafiki au watu unaowafahamu lakini sio makosa kusema uongo kwa makundi mengine ya watu. Baadhi ya watu huiba fedha au mali nyingine kutoka kwa waajiri wao kwa sababu wanafikiri kwamba wanastahili kulibwa zaidi. Wengine wanawaibia watu matajiri hasa matajiri walio wageni. Watu wengine wanawafanyia vitendo visivyo haki watu kutoka makundi tofauti ya kikabila au tabaka la kijamii.

Yesu alisema tuwapende jirani yetu kama vile tunajipenda sisi wenyewe. Kumbuka swali ambalo mwanasheria alimuuliza Yesu? "Je, jirani yangu ni nani?"[32] Mwanasheria alitaka Yesu abainishe vikundi vya watu ambao wangependwa. Yesu alitoa hadithi ya" Msamaria Mwema." Hadithi hiyo inahusu watu wawili kutoka makabila tofauti waliokutakana kwa mara ya kwanza. Hawakuwa na uhusiano hapo awali, na kulikuwa na mzozo kati ya makabila hayo mawaili. Msamaria alimsaidia mwanaume aliyekuwa na hitaji hata ingawa hakulazimishwa na uhusiano wowote. Jambo moja Yesu alifanya kwenye hadithi ni kuwa mtu yeyote asitengwe kutoka kwenye upendo wetu.

Hatutakiwi kuamua ni nani anastahili uaminifu wetu. Hatupaswi tuwe waaminifu tu na wale wachache tunaowachagua. Hata tukijua ya kwamba mtu hataadhirika na ukosefu wa uaminifu wetu, tunataka tumfurahishe Mungu kwa kuwa waaminifu (Matendo ya Mitume 24:16).[33]

Wewe ungependa uwe mtu wa aina gani? Mungu angependa uwe mtu wa aina gani?

Mtu anaweza asistahili heshima yako, lakini Mungu anataka uwe mtu wa heshima. Mtu anaweza kuwa hastahili uaminifu wako, lakini Mungu anataka uwe mtu wa uaminifu. Mtu anaweza kuwa hastahili upendo wako, lakini Mungu alikupenda wakati haukustahili, na anataka uwe mtu wa upendo.

► Wanafunzi wasome 1 Petro 2:21-23 na 3: 8-12 kwa niaba ya kikundi.

Usiruhusu tabia au sifa ya wengine kuamua tabia au sifa yako. Mtu anaweza sema uongo kwako, lakini wewe usiwe mwenye kusema uongo. Mtu anaweza kukuibia, lakini hiyo isilkufanye uwe mwizi. Mtu anaweza kuwa mwenye kiburi kwako, lakini wewe uwe mtu wa heshima.

Vielelezo kutoka katika Maisha

Vielelezo katika sehemu hii ni visa halisi, lakini majina na maelezo yamebadilishwa. Ni baadhi ya mifano ya kuiba, kusema uongo au zote mbili.

Kwa kiongozi wa darasa: Hakikisha wanafunzi wanaelewa kile kilichofanyika katika kila kielelezo. Waulize wanafunzi kueleza kwa nini kitendo katika kielelezo ni kosa.

[32] Luka 10:29
[33] Pia Wafilipi 1:10, 2 Wakorintho 5:9

1. George alifanya kazi kwenye kiwanda. Mara kwa mara alichukua vifaa vya kusafishia nyumbani, vyombo au zana na vitu vingine vidogo kwa sababu alijua kuwa kiwanda kitanunua vitu hivyo.

2. Pedro alikuwa dereva wa lori la mizigo wa kampuni kubwa. Wakati alipokuwa anaendesha gari la kampuni angeona ishara kando ya barabara iliyosema "Tunanuna mafuta ya diesel." Kuna wakati mwingine angesimamisha gari na kuwauzia mafuta kidogo kutoka kwenye lori, akijua kwamba kampuni isingejua kuwa mafuta kiasi kidogo yalikuwa yametolewa.

3. Tamaara aliaminiwa kunua mtambo wa kompyuta kwa ajili ya ofisi ambapo alikuwa anafanya kazi. Alimpa hongo muuzaji kwenye duka ili aandike risiti inaonyesha bei ya juu ili aweze kuchukua baadhi ya fedha.

4. Kwenye bustani katika jiji kubwa, mwanamume mmoja anauza balbu za mwanga ambazo hazifanyi kazi au kuisha nguvu. Wanunuzi wanajua kwamba hazifanyi kazi. Wanazinunua ili kuzipeleka ofisini ambako wataiba balbu nzuri na kuzibadilisha na hizi za zamani.

5. Alex alikuwa mkuu wa shule. Siku mmoja baba mzazi wa mwanfunzi alikuja kwake na akitaka kijana wake apewe daraja nzuri kwenye masomo ya algebra. Alipmatia Alex fedha. Alex aliamuru mwalimu wa algebra ampe mwanafunzi alama nzuri.

6. Angelo alikuwa profesa kwenye chuo kikuu. Mshahara wake ulikuwa mdogo. Aliwaambia wanafunzi katika darasa lake kuwa mtihani utakuwa mgumu na kuwa hakuna mwanafunzi atakayefanya vizuri katika mtihani bila hao kunua kutoka kwake ukurasa wenye majibu.

7. Alex alikuwa mkuu wa shule ya serikali. Siku moja, Vanya rafiki yake Alex anayefanya kazi na shirika la kimishonari akamuuliza kama shirika la kimishonari lingekodi vyumba kwenye jengo la shule. Alex akatoa bei, na Vanya akaleta fedha kila mwisho wa mwezi . Alex aliweka hizo fedha kwa siri bila kutoa ripoti ya mapato.

8. Vanya alifanya kazi na shirika la kimishonari ambalo lilihitaji kukodi nafasi za madarasa. Vanya alienda kwa Rafiki yake Alex, mkuu wa shule. Wakukubaliana bei ya kukodi madarasa, halafu Vanya akaenda kwenye shirika lake akataja bei ya juu. Kila mwezi Vanya alimletea Alex fedha lakini alibaki na fedha za ziada.

9. Sergei alifanya kazi na huduma fulani ambayo ilihitaji jengo jipya. Hilo shirika lilimpa Sergei jukumu la kutafuta kampuni ya ujenzi kwa ajili ya kazi ya ujenzi. Sergei aliongea na kampuni mbalimbali za ujenzi. Badala ya kuchagua kampuni ambayo ingewapa bei iliyo bora zaidi, yeye alichagua ile kampuni ambayo iliahidi kumpa baadhi ya fedha ambazo wangepata kutoka kwa shirika.

10. Alberto alihitaji kulitafutia gari lake leseni. Lakini alijua ya kuwa gari lake lisingefikia viwango vya ukaguzi kwa sababu baadhi ya taa zilikuwa hazifanyi kazi. Alilipeleka

gari kwenye idara ya ukaguzi na akaona foleni ndefu ya watu ambao walikuwa wameleta magari yao yakaguliwe, Mtu moja karibu na lango akamwambia kuwa, kwa kiwango fulani cha fedha ataweza kumsaidia apate leseni kwa haraka bila ukaguzi wa gari. Alberto alilipa fedha na muda sio mrefu akapata leseni na kaondoka kwenda nyumbani.

11. Simoni alikuja kuchukua gari lake kutoka eneo la kuegesha magari. Mhudumu wa maegesho alimwambia bei ya kugesha. Simon alimpa mhudumu fedha kidogo kuliko ada ya kawaida lakini akamuruhusu kutunza tiketi ya kuegesha ambayo angeweza kumpatia mteja mwingine ili aweze kuitumia na mhudumu angebaki na fedha ambazo amelipwa na Simoni.

12. Anna hakujianda vya kutosha kwa ajili ya mtihani. Alipokuja darasani alikaa karibu na mwanafunsi aliyekuwa mwanafunzi bora ili aweze kunakili majibu ya mtihani kutoka kwa rafiki yake.

13. Igor aliendesha trekta iliyokuwa ikivuta majembe ya kulima kwenye shamba kubwa la serikali. Alitaka kumaliza kazi mapema. Aliinua jembe ili lisiwe chini sana na kumfanya aendeshe trekta kwa haraka. Shamba lilionekana kuwa tayari, lakini halikuweza kukuza mimea mizuri kwa sababu halikulimwa vizuri.

14. Mchungaji Perrie alitumwa na misheni ya kanisa kuwa mchungaji wa kanisa. Misheni ilimtumia mshahara kila mwezi. Kwa sababu mchungaji Perrie alitaka kanisa limlipe pia, aliwambia washirika wa kanisa hilo kuwa misheni haimpi msaada wowowte.

15. Mwizi alikuja kwa nyumba ya Ellah na akaiba fedha. Alipowaeleza rafiki zake kuhusu yaliyotendeka, alisema mwizi aliiba vitu vingine ingawa huo haukuwa ukweli. Rafiki zake walimuhurumia kwa kumpa fedha kununua vitu ambavyo walidhani vilikuwa vimeibiwa.

16. Gulovo alikua chifu wa Kijiji kidogo. Alikuwa kiongozi katika kanisa la Kijiji. Watu wake walikuwa wa kale, wasio na elimu na maskini ingawa Kijiji kilikuwa kilikuwa na ardhi kubwa. Wafanyabiashara kutoka mjini walitaka kununua ardhi kwa ajili ya miradi ya ukulima. Gulovo aliuza ardhi yote ya Kijiji na akatumia fedha kujijengea nyumba huko mjini.

17. Kila mwaka Kanisa la Fairfield Community huchagua mama mmoja kumtuza kama "mama wa mwaka". Walimchagua Wilma, sio kwa sababu alikuwa na sifa nzuri kama mama, lakini ni kwa sababu walijua atachangia fedha kwa kanisa. Baada ya kutuzwa, Wilna alichangia fedha kanisani kwa ajili ya kununua milango mipya kwa ajili ya mali ya kanisa. Mwaka uliofuata kanisa liliamua kumteua tena Wilma kama mama wa Mwaka hata ingawa alikuwa amehamia jiji lingine.

18. Barney alikuwa dereva katika huduma fulani. Kila jioni alichukuwa gari la kazi na kuliegesha sehemu yenye ulinzi. Wakati mwingine kabla ya kuegesha gari alikuwa analitumia kubeba abiria na mizigo kama wateja wake wakibinafsi.

Jangwa la kitaifa la Ukosefu wa Uaminifu

Hii hadithi ni ya kubuni lakini inaeleza kile kinachofanyika sehemu nyingi.

Wakristo katika jiji la Borol walitambua kuwa kulikuwa na jamii kubwa ya watu katika eneo jirani ambao walikuwa wanaishi kwa umaskini. Watu wa hilo eneo walikuwa wa kabila liitwalo Ibanese. Kwa vizazi watu wa Ibanese waliishi maisha ya kale sana katika nyumba zao bila kufikiwa na huduma za afya au masomo. Wengi hawakuwa na chakula cha kutosha na baadhi yao walikuwa na njaa.

Wakristo wa Borol walianza kutoa fedha kusaidia Waibanese. Walituma wawakilishi wao kwa makanisa kwenye maeneo mengine kuomba michango.

Wakristo wa Borol walianza kupeleka msaada wa chakula kwa Ibanese kutumia lori za mizigo. Walianza kutegemea viongozi wa kanisa la Ibanese kusambaza chakula.

Viongozi wa Ibanese walianzisha masoko ya kuuza chakula kwa watu wao. Watu wenye fedha pekee ndio walikua na uwezo wa kununua. Kwa hivyo hakuna chakula chochote kiliweza kuwafikia watu ambao walikua na njaa. Viongozi wa kanisa na marafiki zao walichukua faida. Baadhi ya chakula kilipelekwa kwenye maeneo mengine kuuzwa ambako mapato yalikuwa ya juu.

Wakristo wa Borol walisisitiza kuwa chakula lazima kipewe bure kwa wale ambao walikihitaji sana. Viongozi wa kanisa pale Ibanese walitengeneza bajeti ya kusambaza ambayo ilijumuisha kukodi lori la mizigo na madereva na kulipa watu wa kusaidia. Walipanga bei kuwa juu kuliko kawaida na kuchukua fedha za ziada. Wakristo wa Borol walipohitaji ripoti za matumizi, waibanese walitoa ripoti za uongo.

Kila wakati wakristo wa Borol walipogundua vitendo vya kukosa uaminifu, walikata tamaa na kushushwa moyo. Walipojaribu kutafuta tafuta viongozi wengine kutoka kwa jamii ya Ibanese kuwasaidia lakini walikabiliana na shida hiyo hiyo. Wakristo wengi wa Borol waliaacha kutoa. Wengine waliendelea kutoa. Muda sio mrefu wachungaji wachache wa Ibanese walikuwa na magari na nyumba nzuri kwa sababu ya msaada kutoka Borol. Wachungaji wengine wakaanza kuwaonea wivu na wakatamani mahusiano na watoaji wa Borol. Wale ambao walikuwa na njaa maeneo ya mbali hawakupata msaada wowote.

Kielelezo Cha Kuhitimisha

Warren Buffet alikuwa mkurugenzi mtendaji kwenye kampuni iitwayo Berkshire Hathaway. Alitaka kunua kampuni iitwayo McLane Distribution ambayo ilikuwa inamilikiwa na Walmart. Bei ya kununuliwa ilikuwa dollar bilioni 23. Kwa kawaida ununuzi huu ulihitaji miezi ya ukaguzi ndiyo mnunuzi aweze kuangalia na kukagua kila kitu. Buffet alikutana na viongozi wa Walmart na wakawa na makubaliano kwenye kikao kimoja. Hakutuma mtu kuhakikisha kuwa mali zilikuwa sawa. Baadaye alisema,”Tulijua kuwa kila kitu kilikuwa sawa kwa vile

Walmart walisema itakuwa na ikawa.” Huu Mpango mkubwa wa kibiashara ulimalizika kwa haraka kwa sababu viongozi waliaminiana.[34]

Sasa jaribu kufikiri kuhusu viongozi tuliowaangazia kwenye kielelezo cha awali. Hakuna mmoja wao ambaye anaweza kufanya maafikiano kama haya, kwa sababu sio wakuaminiwa. Kila kitu lazima kikaguliwa ni hiyo inachukuwa muda mrefu sana na gharama kubwa.

Kushiriki kwa vikundi

► Ni baadhi ya mazoea gani ya kukosa uaminifu ambayo ni vigumu kwa watu kuepuka katika utamaduni na mila ya kwako?

► Ni Mazoea gani unapswa kubadilisha?

Maombi

Baba wa Mbiguni,

Tunakusifu kwa kuwa Mungu wa uadilifu na ukweli. Tunakushukuru kwa kuwa wakati wote wewe ni mwenye ukwelli kwenye shughuli zako na sisi.

Tusaidie tufuate viwango vya uamnifu ambao unavyo kwa ajili yetu.Tusaidie tutumie katika Maisha yetu ya kila siku kanuni za uaminifu kwa kila tusemalo na kufanya.

Ahsante kwa kuwa kuwa Baba yetu ambaye hutoa na kutuongoza. Tunataka tukuamini kuwa utatutunza.

Amina

Zoezi la somo la 10

(1) Andika aya kuhusu kila moja ya yafuatayo:

- Eleza uhusiano kati ya sifa ya Mungu (ukweli) na viwango vya Mungu kwetu (uaminifu). Eleza kwa nini Mungu anahitaji sisi tuwe waaminifu kwa yale tunayosema na katika shughuli zetu zote.
- Kwa ufupi eleza kile ambacho Biblia inasema kuhusu uaminifu. Tumia angalau maandiko matatu kwa mafupisho yako.
- Eleza angalau njia nne za ukosefu wa uaminifu au za uaminifu huathili uhusiano wetu na wengine.

(2) Jiandae kufanya uwasilishaji wa kibiblia kuhusu uaminifu ambao unaweza kushiriki na kikundi kutoka utamaduni au mila yako.Toa msingi wa kibiblia kwa msimamo wa Mungu una kisha uonyeshe matumizi wenye mifano mahususi.

[34] Stephen M. R. Covey. *The Speed of Trust: The One Thing That Changes Everything*. (New York: Free Press, 2006), 15

Somo la 11
Thamani ya Binadamu

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuamini kuwa kila mwanadamu ni mwenye thamani na anastahili kuheshimiwa kwa sababu ameumbwa kwa mfano wa Mungu.

(2) Kuchukua jukumu la kufanya vitendo vya haki na kuwa mwenye huruma kwa wale ambao wananyanyaswa sehemu wanapoishi.

(3) Kujitolea kuwatendea watu wote kwa utu bila kujali hali.

Dale Carnaage, Mtu Aliyethamini Watu

Dale Carnegie alipata umaarufu kwa kitabu chake, *Jinsi ya Kupata Marafiki na Kushawishi Watu*. Aliamini kuwa watu wote wanastahili kuzingatiwa na kuheshimiwa kwa sababu wanathamani kama watu. Taasisi ya Dale Carnegie ilianzishwa kufundisha kanuni zake.

Kuna wakati Fulani taasisi ya Dale Carnegie ilifundisha masomo ya jioni kwa wafanyabiashara, wakifundishwa jinsi ya kuwa na urafiki na kujenga mahusiano na watu. Wanafunzi walipopewa mtihani, walishangazwa na swali moja. Swali ambalo halikutarajiwa lilikua hivi,"Je jina la mwanamke ambaye ambaye huwa anafanya usafi kwenye ukumbi unapotoka darasani anaitwa nani?" Wanafunzi mara nyingi walikuwa wakimpita wakitoka darasani kuelekea nyumbani lakini hawakulichukulia Kama ni jambo la muhimu sana kumjua, hata ingawa walikuwa wametoka kwenye darasa la mafunzo ya kuwa na urafiki na kujenga mahusiano. Walidhani kuwa watatumia ujuzi wao mpya kwa kujenga mahusiano na watu wa maana pekee yao.

Thamani ya Kikristo ya Ubinadamu

Binadamu wote ambao wanaweka Imani yao katika Kristo ni washirika wa mwili mmoja-Mwili wa Kristo:"Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa waa huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:28).

Injili ya Luka inatueleza mazungumzo wakati Yesu aliponukuu amri "….na jirani yako kama nafsi yako." Mwanasheria akamuuliza swali, "Je jirani yangu ni nani?" (Luka 10:29). Hilo swali lilikua lenye umuhimu sana kwa sababu mwanasheria alidhani kuwa hakuwa na haja ya kumpenda kila mtu. Alifikiri kuwa amri ilimuhitaji kupenda watu wa kikundi fulani.

Watu wa tamaduni na mila zote wana maadili yanayofanana. Wanajua kwamba kuiba, kuua na dhuluma ni makosa. Hata hivyo hawafikirii kuwa kila mtu anastahili kutendewa haki.

Labda hawaibi kutoka kwa rafiki, lakini wataiba kutoka kwa mgeni wasiyemjua. Labda wasimuue mtu wa taifa lao lakini wamuue mgeni. Labda wasidhulumu watu wa jamii yao, lakini wadhulumu watu wa kabila ambalo wanalidharau.

Wakristo wanaamini kuwa kila binadamu ameumbwa katika mfano wa Mungu na thamani yake haina kikomo.

Wakati wowote ambapo malaika walionekana mbele ya watu kama vila ambavyo imeandikwa katika maandiko, maneno yao ya utangulizi yalikuwa "usiogope," kwa sababu uwepo wao ulikuwa wa kushangaza na kupita kiasi. Wakati mwingine watu walianguka chini kwa heshima mbele ya malaika kwa ajili ya kuabudu.[35] Lakini mwanadamu ni wa maana zaidi kuliko malaika.[36]

Unaweza kutana na mtu ambaye ni ombaomba wa tabaka la chini, hajasoma, asiye na akili sana, wa tabia mbaya na upungufu wa ujuzi, hana ushawishi, maumbile yanayo chukiza, utu usiopendeza lakini bado anafanya maamuzi ya matokeo ya milele. Kama amekombolewa na Mungu atakuwa kiumbe mkuu kuliko yeyote tuliyemuona duniani.[37] Kwa hivyo anastahili heshima.

► Mwanafunzi asome Wagalatia 3:28 kwa niaba ya kikundi.

Aya hii inataja namna tatu ambayo watu mara nyingi wanaainishwa- kikabila, tabaka la kijamii na jinsia. Tabaka la kijamii inajumuisha viwango vya uchumi. Tunaweza kuongeza sababu zingine kama vile umri, viwango vya masomo na ujuzi. Hakuna uainishaji wowote tuliotaja unaopaswa kuathiri thamni ya Mungu kwa mtu.

► Mtu mmoja anaweza kuwa na thamani zaidi kuliko watu wengine? Eleza

Mtu aliye na akili nyingi, masomo, ujuzi, nguvu za kimwili, uzoefu wa uongozi au fedha ana thamani zaidi *kwa kuweza kukamilisha majukumu fulani ya kazi.* Hata hivyo ni makosa kuzingatia kuwa mtu ana thamani zaidi kama binadamu kwa sababu ya hizi sifa. Hizo sifa zina thamano ya vitendo, lakini asili ya muhimu ya ubinadamu iliyofanywa kwa mfano wa Mungu ina thamani isiyo na kikomo na ni ya milele.

Ubaguzi

Watu hufikiri kwamba watu wote wenye kikundi fulani cha kabila wana sifa ambazo ni sawa. Hizi sentensi mara nyingi hutolewa kwa kuangalia rangi ya Ngozi kama vile "Watu weupe wakati wote _____" au "watu weusi wote _____."

[35] Mfano mmoja wah ii ni Ufunuo 22:8-9.
[36] 1 Wakorintho 6:3
[37] 1 Wakorintho 15 inaeleza mabidiliko ya ajabu ya miili ya Kikristo ambayo yatatokea wakati wa ufufuo.

Wakati mwingine sentensi inahusu utaifa, kama vile Wahaiti au Wajerumani au Wajapani. Wakati fulani ni maalum zaidi, kama vile jina la kikabila au kabila fulani kwenye taifa.

Sentensi ambazo watu wanatoa kuhusu makundi ya watu wakati mwinginw ni za kusifu au pongeza, lakini mara nyingi ni za kushutumu au kukosoa. Sentensi hizo zaweza kusema kuwa kila mtu kwenye hicho kikundi anakosa au upungufu fulani.

Hapa kuna mfano wa sentensi za kukosoa ambazo watu husema kuhusiana na vikundi vya makabila au mataifa. Majina ya makundi mbalimbali yatawekwa kwenye nafasi zilizoachwa wazi.

- _____ ni wavivu.
- _____ wanalewa mara kwa mara.
- _____ wataiba wakipata fursa.
- _____ wanapigana mara kwa mara.
- _____ hawamalizi kazi vizuri.
- _____ hawana akili za kutosha kufanya vizuri shuleni.
- _____ wanakasirika kwa haraka.
- _____ wandanganyifu.

Ni wazi kuwa tofauti za kikabila zipo, na hizi tofauti ni zaidi ya mwonekano wa kimwili. Kundi la kikabila linaweza kufaulu katika michezo fulani au kazi kwa sababu ya uwezo wa kimwili au akili.

Kundi la watu huwa na sifa fulani za kitamaduni.. Utamaduni hufunza watu kujibu kwa njia fulani katika hali fulani. Kwa hivyo tunajifunza kutarajia vitendo fulani kutoka kwa watu wa tamaduni fulani.

Si vibaya kuona sifa za kimaumbile na kitamaduni za kikundi. Hata hivyo, ni makosa kuhukumu tabia ya mtu kwa sababu ya kabila lake au utamaduni. Mtu kutoka kwenye kikundi chochote cha kabila anaweza kuwa mcha Mungu, mwaminifu na mkarimu. Itakuwa ni makosa kumtendea kama ana tabia mbaya wakati haumjui mtu huyo kibinafsi.

Uzoefu wetu binafsi unathiri jinsi tunavyowaona watu wengine. Kama mtu anatendewa vibaya na watu wa kabila lingine, anaweza kuhisi kuwa watu wote kutoka hilo kabila wako na tabia hiyo. Hisia hiyo inaimarishwa kama mtu anatendewa vibaya mara kwa mara na mtu wa hiyo kabila au mambo mabaya yanafanyika wakati yeye ni mdogo.

Migogoro ya muda mrefu katika ya makabila mawili yanaweza kuzalisha vizazi vya watu ambao wana chuki dhidi ya kila mmoja.

Mtoto anaposikia wazazi wake na watu wengine wazima wakiongea kuhusu kuhusu kabila fulani, maoni yake kuhusu hilo kabila yanatengenezwa.

Mkristo anapaswa kuchunguza mtazamo wake kuhusu vikundi vya makabila. Na aombe Mungu amsaidie ili aweze kuonesha haki na upendo. Tukumbuke kuwa Mungu anajali kuhusu wengine kama vile anavyojali kuhusu sisi na hafurahii tunapowatendea wengine bila haki.

Ubaguzi katika Huduma

Hadithi ya agano la kale ya Yona inafundisha. Yona anatuonesha kwa nini alimtoroka Mungu:

> Akamwomba Bwana, akasema, "Nakuomba, Ee Bwana; sivyo hivyo nilivyosema, hapo nilipokuwa katika nchi yangu? Hii ndio sababu nalifanya haraka kukimbilia Tarshih; kwa maana nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa Rehema, nawe waghairi mabaya!" (Yona 4:2-3)

Yona alikimbia kutoka kwa Mungu kwa sababu ya chuki yake kubwa sana kwa Waashuru na kwa sababu alijua kwamba Mungu alimwita kufanya kazi kati ya watu wa Ninawi ilimaanisha ya kwamba kulikuwa na uwezekano mkubwa Mungu angekuwa mwema kwao.

Biblia inafundisha kwamba wanadamu wote ni jamii moja - jamii ya wanadamu: "Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakat alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makaazi yao" (Matendo ya Mitume 17:26).

Mungu analitaka kanisa kufikia kila kabila duniani na injili (Matendo ya Mitume 1:8). Thamani ya roho ya mwanadamu ni sawa bila kujali kabila lake.

Kutoheshimu makundi ya Watu

Kwa sababu watu huwa wanakubali vipaumbele vya kidunia wao hutumia njia siziso sahihi za kutambua thamani ya watu. Jamii nyingi zinawagawanya baadhi ya watu kama wasio na umuhimu sana na huwachukulia kana kwamba wao ni chini ya binadamu.

Hapa chini ni orodha ya mifano ya namna ambazo jamii mbalimbali zimewatendea baadhi ya makundi ya watu bila heshima. Baadhi ya hivi vitendo ni ya kihistoria; na vingine bado vinatendwa.

Mifano halisi ya kutoshemu makundi ya watu:

- Wazee hawana manufaa tena, kwa hivyo wanawachwa mahali pa pekee ili wafe.
- Watu wanawamiliki watu kutoka makundi fulani ya kikabila kama watumwa na wanaweza kuwauza au kuwatendea vile wanavyotaka.
- Matangazo ya biashara yanasema kuwa watu wa kabila fulani hawataajiriwa.

- Wanawake wanachuliwa kuwa mali ya waume zao na watatendewa vile waume wao wapendavyo.
- Watoto wasichana wanawachwa kufa kwa sababu familia walitaka mtoto wa kiume.
- Serikali ya kitaifa inapeleka wanajeshi katika eneo fulani la inchi kuua kila mtu wa kabila fulani.
- Watoto huachwa kwa sababu wana ulemavu wa kiakili au wa kimwili.
- Taifa lina sheria zinazokataza mwanamke kuendesha gari au kupata elimu ya chuo kikuu.
- Watu wanozungumza lugha ya kawaida ya kitaifa lakini sio lugha inayotumika kwenye shule hawaruhusiwi kujisemea katika afisi za serikali.
- Watu wanaajiriwa kwa sababu kwa sababu wana majina ya kingereza badala ya majina ya kiafrika.
- Wasichana wanawezwa kuuzwa utumwani au kwenye ukahaba na baba zao.
- Watoto wanauawa kabla ya kuzaliwa kwa sababu mama hayuko tayari kupata Watoto.

Baadhi ya filosofia na dini zinaunga mkono unyanyasaji wa makundi ya watu.

Wanaugeuzi wasio mwamini Mungu hawaamini kuwa watu wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Wanaamini kwamba mwanadamu wa sasa wamekua kimaendeleo kwa kushindana na kuharibu makundi dhaifu na yasiyo na akili ya wanadamu. Waliamini kuwa "kuishi kwa walio na nguvu"- ndiyo kumetuzalisha. Kama hiyo ingekuwa ukweli basi ingekuwa vyema kwamba watu waendelee kuharibu aina dhaifu za binadamu. Lakini tunajua kuwa watu wote waliumbwa kwa mfano wa Mungu na kwa hivyo wako na uhusiano wa pekee na Mungu.

Mataifa mengi ya dunia yanaruhusu madaktari kuua Watoto kabla hawajazaliwa. Serikali zingine wamelazimisha mauji ya Watoto kwa sababu ya idadi kubwa ya watu. Katika mataifa mengi, wamama huomba madaktari kuua watoto kabla hawajazaliwa kwa sababu hawako katika hali nzuri ya kuweza kupata mtoto. Hii inapuuza thamani ya binadamu na haki za mtu ambaye hawezi kujisemea mwenyewe.

Dini kama vile Uhindi na Ubudha zinaamini kuwa watu wanateseka kwa sababu ya matendeo yao mabaya katika maisha yao ya hapo awali. Wanaamini kuwa watu waliodhulumiwa wanastahili hadhi waliyo nayo. Wanaamini kuwa mtu akiweza kustahimili vyema mateso na dhuluma, anaweza kuwa na maisha mazuri wakati mwingine. Hizo dini zinatoa sababu ndogo kumsaidia mtu aliyedhulumiwa, kwa sababu ya kufikiri kwamba mtu anapitia mchakato unaohitajika.

Falsafa na dini potovu husababisha watu kuvumilia unyanyasaji wa kutisha wa tabaka za watu. Jamii zinakubali hali za ukosefu wa haki uliokithiri katika jamii kama kitu cha kawaida.

Wakristo wako tofauti. Fundisho la ukristo la uumbaji maalum kwa sura na mfano wa Mungu hutoa msingi wa kutosha wa thamani ya binadamu.

► Ni aina gani ya kutoheshimu kundi la watu ni jambo la kawaida katika jamii yako?

Jirani Mwema

Kama ilivyo mifano mingi ya Yesu, hadithi ya Msamaria Mwema (Luka 10:29-37) iliwashangaza wasikilizaji wake. Alipowaambia namna ambavyo kuhani na mlawi walivyompita mtu aliyejeruhiwa bila kumsaidia hakuna mtu aliyeshangaaa. Makuhani na walawi walikuwa sehemu ya taasisi za kidini lakini watu walifikiri walikuwa wameharibiwa na fedha na madaraka.

Wasikilizaji walitarajia mtu wa tatu awe shujaa wa hadithi, lakini walishtuka na kukataa tamaa kwa sababu alikuwa Msamaria. Wasamaria walikuwa ni mchanganyiko wa kikabila, na walichanganyikiwa kidini. Wayahudi waliwadharau kwa sababu ya hizo sifa zote mbili.

Kumbuka, Mwanasheria Myahudi alikuwa amemuuliza Yesu swali, "je jirani yangu ni nani?" alikuwa anataka yesu afafanue watu ambao yeye angewapenda, akipunguza ili liwe kundi godola wale awapendao. Kama watu wengi wa dunia, alidhani kuwa wajibu wa kimaadili ulikuwa tu wa kikundi fulani cha watu waliochaguliwa, na kwamba hakukuwa na sababu ya kujali wengine.

Yesu alimjibu swali kwa kumuonyesha kwamba inatupasa tujali mtu yeyote tunayekutana naye. Mtu yeyoye tunayekutana naye ni jirani yetu. Lakini pia yesu alijibu swali ambalo hakuna mtu yeyote alikuwa ameuliza, "Nani jirani mwema?" Au "Mtu aina gani anaonyesha upendo kama huu?" Alionyesha kuwa mtu ambaye haheshimiwi na jamii anaweza kuwa mtu ambaye anampendeza Mungu kwa kuwa anaonyesha upendo ambao Mungu anataka kuona.

Mtume Yakobo analionya kanisa kuheshimu watu kwa viwango vya ulimwengu.

► Mwanafunzi asome Yakobo 2:1-9 kwa niaba ya kikundi. Umeona Makanisa yakifanya nini ambacho kina mahusiano na haya?

Watu ambao wanachukuliwa kuwa muhimu duniani sio watu ambao wanaheshimiwa mbele za Mungu. Watu wengi ambao wanampendeza Mungu hawaheshimiwi hapa duniani. Yesu alinena kuwa katika umilele hadhi za watu wengi zitabadilishwa(Mathayo 19:30).

Wakati ndugu wakristo wanapokuja pamoja, yule mtu maskini anapata hadhi ambayo asingeipata kule duniani, kwa sababu anaheshimiwa kama ndugu mkristo. Mtu tajiri anapoteza hadhi yake aliyonayo hapa duniani, kwa sababu fedha haimuweki juu ya wengine kanisani (Yakobo 1:9-10).

Utumwa

Utumwa ni hali ambayo mtu anamilikiwa kama mali ya mtu mwingine. Katika mataifa mengi ambayo yanakubali utumwa, mtumwa hana haki kama binadamu. Mmiliki anaweza kufanya lolote atakalo kwa mtumwa kana kwamba mtumwa ni mnyama au mashine. Matakwa

binafsi ya mtumwa yako chini ya mapenzi ya mmiliki. Mume na mke wanaweza kutenganishwa na mmiliki, na Watoto wachukuliwe kutoka kwa wazazi wao.

Katika Agano la Kale, Mungu aliweka sheria za kumiliki mtumwa kuwa finyu na akalinda haki fulani za watumwa. Kujali haki za watumwa haikuwa jambo la kawaida nyakati hizo. Katika Agano Jipya Mungu anasema kuwa yeye ndiye Bwana Mkuu wa watu wote, hapendelei mtu yeyote kwa sababu ya hadhi yake na Bwana wa watumwa ni sharti awe mwenye upendo (mkarimu) na mwenye haki (Waefeso 6:9). Kanuni ya kwamba mtumwa anapaswa kutendewa kwa kuzingatia kile anachostahili kila mwanadamu ilipelekea kukomeshwa kwa biashara ya watumwa katika mataifa mengi ambayo yanashiwishika na mandiko ya Biblia.

Utumwa bado upo sehemu nyingi duniani katika njia au namna tofauti. Kwa mfano, sehemu fulani watoto wanauzwa na wazazi ili kufanya kazi au kwa sababu za ngono. Wakati mwingine watoto wanapelekwa katika mahekalu ya kipegani ili kukombolewa kutoka kwa magonjwa na laana. Wakati mwingine wanawake wanalazimishwa kuwa makahaba kinyume cha mapenzi yao. Wakati mwingine watu wanaingizwa katika nchi nyingine kwa madhumuni ya kufanywa watumwa.

Ukandamizaji wa kiuchumi

Sehemu ambazo zinakosa uhuru wa kiuchumi, hali inaweza kufanana na utumwa. Watu hawana uhuru wa kuendesha au kufanya biashara zao. Kuna fursa ndogo kwa mtu kubadilisha kazi yake kwa kitu bora. Wanaume wengine hufanya kazi kwa ujira ambao hulisha familia zao kwa shida. Mara chache hununua chochote isipokuwa chakula cha msingi. Hawawezi kumudu huduma ya matibabu. Hata wafanye kazi namna gani hawataweza kuwa na nyumba nzuri za kuishi kwa sababu fedha walizo nazo hazitoshelezi mahitaji yao. Waajiri wao hawalipi zaidi kwa sababu wanaweza kupata wafanyakazi ambao wako tayari kulipwa mishara midogo.

Ukandamizaji wa kiuchumi ni swala ngumu na lenye changamoto na ambalo lawama sio tu ya waajiri pekee yao. Baadhi ya mataifa kuna wafanyakazi wengi ambao wanapatikana lakini kuna upungufu wa viwanda na biashara kubwa kubwa. Kama serikali ni nyenye ufisadi, inaweza kuzuia biashara za wiwango kubwa kuanza kwa kudai ushuru wa kiwango cha juu na hongo. Kama biashara nyingi zinaruhusiwa, mishara ya wanyakazi itakuwa ya kiwango cha juu kwa sababu wafanyakazi watakuwa na uhuru wa kuchagua pale ambapo wangependa kufanya kazi na watavutiwa kwenye biashara ambazo malipo ya mishahara na hali ya kazi ni nzuri. Kwa sababu biashara chache zinaruhusiwa na wafanyakazi wana chaguzi chache za kikazi, waajiri wanaweza kulipa wafanyakazi wao mishahara midogo. Wafanyakazi hawalipwi vya kutosha kutimiza mahitaji yao.

Madhumuni ya serikali ni kuwatumikia wanainchi kwa kuwalinda kutokana mashumbulizi na kulinda uhuru wao. Uhuru wa msingi wa binadamu ni: haki ya kuzungumza maoni yake, uhuru wa dini, kufanya kazi kwa faida, na kumiliki mali. Mtu ambaye haruhusiwi kufanya vitu hivi hatendewi vyema kama binadamu.

Wakati mwingine wakristo wakiwa mahali fulani hukubali hali ya ya unyanyasaji kama ni kitu cha kawaida na hawafanyi lolote kusaidia wale ambao wananyanyaswa kiuchumi.

Jamyla aliishi katika kijiji kidogo ambapo hakukuwa na ajira. Aliwawacha Watoto wake watatu chini ya uangalizi wa bibi yao na akaenda mjini kufanya kazi kama msaidizi wa nyumbani katika nyumba ya mchungaji ambapo alikuwa analipwa 50$ kwa mwezi. Ilikuwa ni nadra sana kuwaona watoto wake. Watu wengi hawaoni kama ni jambo nzuri kwa mama kutengana na watoto kwa ajili ya kazi, lakini wakristo huajiri watu kama hawa walio katika hali ya Jamyla. Wanashanga kwa nini walipe zaidi ilihali kuna mtu ambaye yuko tayari kulipwa huo mshara mdogo. Kwa nni wawe na wasiwasi kuhusu yeye kutenganishwa na watoto ikiwa yeye alifanya uamuzi wa kuwaacha Watoto na kufanya kazi?

► Je, wakristo wana wajibu wa kuingilia kati katika hali ya Jamyla? Kwa namna gani?

Kitabu cha Amos mara kadha kinazungumzia kuhusu ukandamizaji wa kiuchumi. Katika Amosi 5:11-12 nabii anaongea kuhusu rushwa ambavyo inafanya hakimu apendelee yule mtu aliye na fedha na kufanya haki isipatikane kwa wale walio maskini. Katika Amosi 8:4-6 nabii Amosi aliwashutumu watu waliotumia vipimo vyenye uwongo kuwandanga masikini. Katika Amosis 4:1 alisema kuwa wanawake pia ni wenye hatia kama wataishi kwenye anasa ambazo waume zao walipata kwa njia ya kukandamiza maskini. Nabii alisema haki inapaswa kumwagika kama mto (Amosi 5;24), ikimaanisha kuwa ni lazima iwe tele na ipatikane kwa yeyote anayehitaji.

Thamani ya Mwanadamu na Majukumu ya Mamlaka

Ukweli Kwamba kila mtu ana uthamani usio na kikomo haimaanishi kwamba Kusiwe na muundo wa mamlaka miongoni mwa watu. Thamani sawa haimaanishi mamlaka sawa. Kwa mfano, ingawa kila mtu kwenye utatu ni Mungu kikamilifu, Mwana yupo chini ya Baba (Yohana 6:38). Mungu ameamuru mke awe mtiifu mumewe; hiyo haimaanishi kuwa yeye ni duni kuliko mume (Waefeso 5:22). Mungu amewaambia Watoto watii wazazi wao; hiyo haimaanishi kwamba hao ni wa chini kuliko wazazi isipokuwa tu katika makuzi (Waefeso 6:1).

Mungu ndiyo ameweka serikali (Warumi 13:1-5). Ameweka pia mamlaka kanisani. (Waebrania 13:17).

Viongozi wote ni lazima wakumbuke kuwa hao ni watumishi (Mathayo 20:25-28). Kutumikia kwa kuongoza inamaanish kuongoza kwa faida ya wale ambao ni wafuasi. Kiongozi haongozi kwa sababu ya faida yake binafsi lakini anajitolea kibinafsi bila kuzingatia faida yeyote kwa ajili ya kuwatumikia wale ambao wanamfuata.

► Je unawezaje kueleza ukweli kwamba kimsingi baadhi ya watu watu ni mhimu zaidi kuliko wengine na kwa maana nyingine watu wote ni sawa mbele ya mungu?

Matumizi ya mafunzo haya katika Maisha ya kila siku ya wakristo

Hakikisha kuwa watu wote wanatedewa inavyostahili na familia ya kanisa.

- Wazee na watu wenye umri wanakumbukwa na kusaidiwa kama inavyohitajika?
- Watoto wanathaminiwa na kupewa mafunzo na kutiwa moyo kulingana na viwango vyao vya ukomavu?
- Watu maskini wanakaribishwa na kufanywa kujisikia vizuri na uhuru katika kanisa lako?
- Unaepuka kuwaheshimu na kuwatambua watu kanisani kwa sababu ya mali zao au hadhi katika jamii?
- Je watu wote wa kabila zote wanakaribishwa kwenye ushirika na kushiriki katika maisha na huduma ya kanisa?
- Kuna kundi lolote la kikabila ambalo linahitaji kufikiwa na injili ya Yesu Kristo?
- Kuna watu wanaonyanyaswa katika Sehemu yako unayokaa na wanahitaji mtu wa kuwatetea?

Familia ya kikristo lazima ioneshe kwa vitendo thamani ya watu wote. Mke na mume wote lazima waheshimiwe. Mahitaji yao lazima yazingatiwe. Watoto wasipuuzwe au kuchukuliwa kama hawana maana. Watoto wanapaswa kuwa na nidhamu ipasavyo. Hauna haki ya kuwa mkatili kwa watoto wako au mke zaidi sana huna haki ya kumtendea jirani yako hivyo.

Tunapaswa kusaidia maskini katika njia inayoimarisha na kujenga utu wao. Usitoe hadharani ili kujipatia heshima huku ukiwadhalilisha maskini. Ukimpa maskini kwa njia ya haki ili kupata kile anachohitaji, heshima yake inalindwa na anaweza kufanya uchaguzi, na anaweza kufanya kazi kwa ajili ya faida. Msaada mzuri ni ule ambao utampa maskini nafsi ya kubadilisha hali yake.

Manabii wa Agano la Kale walisisitiza kwamba Mungu anataka watu wake wawawekwe huru wale waliodhulumiwa na kunyanyaswa (Isaya 58:6).

Agano Jipya linasisitiza ukweli kwamba Yesu alikuja kati ya maskini. Alizaliwa mahali ambapo wanyama walihifadhiwa. Wengi wa marafiki na wafuasi wake walikuwa watu wa kazi na watu maskini. Yesu alionyesha kujali watu ambao hawakuwa wa maana katika jamii yake: maskini, wenye ukoma, wajane, wageni, na watoto. Alisema alikuja kuwaletea maskini habari njema. Alisema kwamba injili itawaweka huru waliokandamizwa.

Tangu siku za kanisa la kale, Wakristo wamekuwa watendaji katika jamii zao, Wamewachukuwa Watoto waliowachwa majumbani kwao. Kuwakomboa watumwa na kusaidia wagonjwa. Wamekuwa na moyo wa kujalia watu ambao jamii yao iliwaona kuwa hawana thamani.

Yesu alisema kwamba tunapaswa tuombe kuwa ufalme wa Mungu uje na mapenzi yake yafanyike hapa duniani kama vile mbinguni (Mathayo 6:10). Tunajua kuwa dhuluma zote zitaisha wakati ufalme wa Mungu utakapokuja kikamilifu hapa duniani. Kwa sasa hivi tuombe Mungu aingilie kati hali ya watu ambao wananyanyaswa kila mahali.

Wimbo Wa Kristmasi

Wimbo wa Krismas "Usiku Mtakatifu"[38] unaongea namna injili inaweka thamani kwa wanadamu, kuleta uhuru. Hapa chini kuna mabeti mawili ya huu wimbo.

1. Usiku mtakatifu, nyota zameremeta
   Ni usiku wa kuzaliwa mwokozi
   Dunia yote, kwa dhamnbi ilizama
   Hadi Yesu akaja na **mtu alijua thamani yake**,
   Kuna furaha kamili ya tumaini, ulimwengu uliochoka hufurahi,
   Alfajiri ya asubuhi mpya na tukufu.

2. Kweli ametufundisha sote kupendana
   Sheria yake ni upendo, na injili yake ni amani.
   Atavunja minyororo kwa sababu mtumwa ni ndugu yetu.
   Kwa mamlaka yake hakutakuwa na uonevu tena.
   Kwa shukrani tutaimba nyimbo tamu za sifa kwa upatano.
   Tumsifu kwa roho zetu zote.

Kushiriki kwa vikundi

Katika vikundi vingi, mada hii itazua mjadala mkubwa. Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuwa na hisia nzito kuhusu yale ambayo wamepitia au wameona.

► Ni kwa vipi mtazamo wako kwa vikundi vingine vya makabila utabadilika ukikumbuka kwamba kila mtu ana thamani kwa Mungu?

► Ni kitu gani ungetemani kufanya tofauti kwa sababu ya yale umejifunza sasa hivi kuhusu thamani ya mwanadamu? Himiza wanafunzi kushirikisha ahadi zao wenyewe zaidi ya kuonyesha hasira kuhusu yale ambayo wengine wamefanya.

► Jinsi gani thamani ya mwanadamu inavyopaswa kuathiri huduma ya kanisa?

[38] Maneno ya wimbo "Usiku Mtakatifu" uliandikwa kwanza kwa kifaransa na Placide Cappeau mnamo mwaka wa 1843.

Maombi

Baba wa Mbiguni,

Ahsante kwa kutufanya viumbe vya pekee katika sura na mfano wako. Nisaidie niheshimu watu wote. Nisaidie nitubie chuki zozote nilizonazo dhidi ya watu.

Naomba ya kuwa utaleta haki kwa wale ambao hapa duniani wanatendewa visivyo kwa msingi wa kabila, jinsia, umri au sifa nyingine.

Nisaidie niwatetee walioonewa na kufanya bidii kuifanya jamii yangu kuwa bora kwa wote. Saidia kanisa na kila mtu mtu mkristo binafsi aonyeshe upendo wako kwa ulimwengu kwa njia maalum.

Amina

Zoezi la somo la 11

(1) Andika kuhusu jukumu ambalo Mungu amelipa kanisa kubadilisha vile ambavyo litawatendea watu katika jamii yake?

- Kanisa linapaswa kufanya nini?
- Wakristo binafsi wanahitaji kufanya nini?
- Wewe utafanya nini?

(2) Soma kumbukumbu la Torati 24:10-22. Orodhesha amri zinaonyesha thamani ya watu. Eleza nia ya kila amri.

Somo la 12
Serikali

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Ataelewa majukumu na mipaka ambayo Mungu ameweka kwenye serikali.

(2) Atii maagizo na kanuni za biblia katika mahusiano yake na serikali.

(3) kujikita katika kuwa na ushawishi katika jamii kwa ajili ya haki.

William Wilberforce, Mtetezi wa Ubinadamu

William Wilberforce (1759-1833) alikua mbunge wa bunge la Uingereza. Yeye alikua mkristo na alipinga biashara ya utumwa, ajira ya watoto na unyanyasaji wa maskini. Ilimchukua miaka ishirini kupitisha sheria ambayo ilikomesha biasahara ya utumwa ya kuchukua mateka afrika na kupelekwa kuuzwa katika dola yote ya Uingereza. Mara nyingi alipata msongo wa mawazo kuona ya kwamba wengine hawajali kuhusiana na jambo hili. Mara alipopata wingi wa kura za wabunge kuunga mkono sheria, wapinzani walishawishi baadhi ya wabunge kutohudhuria kikao cha bunge kwa kuwapa ticketi za ukumbi wa burudani na sheria haikupitishwa. Sheria ya kumaliza biasheria ya utumwa ilipitishwa mwaka wa 1807, ingawa utumwa wenyewe haukufanywa haramu. Wilberforce aliendelea na harakati zake za kuhakikisha kuwa utumwa umekomeshwa katika dola ya Uingereza. Ilipofikia mwaka wa 1833 biashara ya utumwa ilikuwa imeisha sehemu nyingi za dola ya Uingereza. Wilberforce alifariki siku tatu baada ya kupokea habari nzuri kwamba sheria ya kuharamisha biashara ya utumwa ilikua ipitishwe.

Utangulizi

Kumekuweko na tofauti kubwa wa kimahusiano kati ya wakristo na serikali zao. Wakati fulani na mahali fulani katika historia ya Kanisa kulikuwa na kanisa la kitaifa ambalo lilikuwa na ushirika na serikali. Wakati mwingine na mahali pengine serikali iliharamisha kanisa na kulitesa. Kuna mataifa ambayo yanaruhusu uhuru wa kuabudu dini yeyote na serikali haidai kupendelea dini yeyote.

Uhusiano kati ya wakristo na serikali husababisha maswali mengi magumu. Wakati mwingine kanisa likiwa pahali hujenga uhusiano na serikali ambao hauwezi kupatikana sehemu nyingine duniani ambako serikali ni tofauti.

Hili somo halitajibu kila swala au kueleza mkristo atafanya nini katika mazingira ambayo atapitia bali tutatazama kanuni kutoka kwenye Bibilia kuhusu uhusiano wa mkristo na serikali.

► Mwanafunzi asome Warumi 13:1-7 kwa niaba ya kikundi. Ni sentensi gani kuhusu serikali unaona katika kifungu hiki?

Biblia inatueleza ya kwamba Mungu ndiye huziweka serikali za wanadamu. Mungu anataka serikali iwepo na mtu anayekataa kutii serikali ya wanadamu anamwasi Mungu (Warumi 13:2).

► Kusudi la serikali ni nini kulingana na mistari hii?

Kusudi moja la serikali ni kuadhibu tabia mbaya kwa kutekeleza sheria. (Warumi 13:4). Mtawala anamtumikia Mungu na hutimiza kusudi la Mungu anapoadhibu wavunja sheria (Warumi 13:4).

► Mwanafunzi asome I Timotheo 2:1-2 kwa niaba ya kikundi.

Tunahitaji kuombea kwa wale watu ambao wako kwenye serikali ili tuishi maisha yaliyo na utilivu na amani. Inatueleza ya kwamba serikali ikifanya kazi kama vile inavyohitajika inalinda amani ya jamii.

Ushawishi wa Kikristo

► Yesu alituambia tuwe kama chumvi na mwanga (Mathayo 5:13-16). Alimaanisha nini?

Kuna baadhi ya watu ambao wanaamini ya kwamba wakristo hawapaswi kupiga kura au kuwa na nyadhifa kwenye serikali kwa sababu serikali za dunia hazitawali kwa kufuata kanuni za ukiristo. Wengine wanaamini kuwa kanisa inapaswa lijitenge kutoka kwa jamii kwa sababu jamii imeharibka sana.

Nabii Yeremia aliwaandikia Wayahudi ambao walikua wanaishi uhamishoni kwenye jamii ya kipagani. Hawakwenda huko kwa hiari yao. Kama kulikuwa na waumini wa Mungu walikuwa na sababu za kujiepusha na ushiriki katika jamii, hakika Wayahudi hawa walifanya hivyo. Walikuwepo huko kinyume na mapenzi yao, dini ya jamii walimo ishi ilikuwa ya kipagani, serikali ilikuwa ya dhuluma na iliangamiza taifa lao, na wayahudi walikuwa wanasubiri siku ambayo watarudi kwao.

Lakini sikiza ujumbe wa Mungu aliompa nabii Yeremia kwa hawa watu:

> Kautakieni amani mji ule ambao nimewafanya mchukuliwe mateka, mkauombee kwa Bwana; kwa maana katika amani yakemji huo ninyi mtapata amani (Yeremia 29:7)

Shalom, Neno la kiebrania kwa kawaida hutafsiriwa amani, haimaanishi tu amani yenyewe bali baraka ambazo zina ambatana na amani. Linarejelea baraka za Mungu. Hawa wanao mwabudu Mungu watapata baraka za Mungu wanapojaribu kuleta hizo baraka kwenye jamii yenye dhambi na ambayo haijui lolote kuhusu Mungu na inatesa pia watu wa Mungu.

Watu ambao wanamtumikia Mungu ni lazima washawishi jamii yao kwa kuheshimu mapenzi ya Mungu ndipo jamii yao iweze kubarikiwa. Hawapaswi tu kuhubiri injili bali pia kutumia kanuni za kimungu katika kila hali na kila uamuzi.

Serikali na jamii inapaswa iboreshwe na Neno la Mungu. Kutokana na ukweli wa Mungu uliofunuliwa yanapaswa kuja maadili (kanuni na matendo sahihi), kutoka kwenye maadili tunapaswa tupate siasa (serikali ya haki na uhuru), halafu uchumi (usimamizi wa rasilimali). Kwa hivyo mpangalio sahihi wa kweli hii, maadili, siasa halafu uchumi.

1. Ukweli kutoka kwa Maandiko ya Mungu
2. Maadili
3. Siasa
4. Uchumi

Tabia ya asili ya binadamu ni kugeuza utaratibu huo. Watu hufanya uchumi wao binafso au Fedha kuwa ni kipaumbele, halafu watamaanga mkono viongozi na sharia ambazo zitawapa kile wanachotaka hata kama itamaanisha ya kwamba watapoteza haki na uhuru. Basi baaada ya kufanya hivyo wataweza kutunga maadili kuendana na ile wanataka, kisha tena watabuni dini kuidhinisha tabia yao. Kwa hivyo utaratibu wa kawaida ni uchumi, halafu siasa, halafu maadili, halafu dini.

1. Uchumi
2. Siasa
3. Maadili
4. Dini

Dini kama hiyo imeumbwa na kanuni mbaya ambazo hazina ukweli.

Kanisa ni lazima lisimame kwenye msingi wa ukweli wa bibila, sio tu kwa kukataa dhambi katika jamii bali kwa kueleza na kuonyesha kwa vitendo vile jamii inavyohitaji kuwa. Kama wakristo hawawezi kueleza na kuonyesha kwa matendo jinsi jamii inavyohitaji kufanya, tutatarajia ya kwamba watu wasio fahamu ukweli wa kibiblia watashindwa kutuumia katika Maisha yao.

Wakristo wasiikosoe tu jamii lakini lazima wawe sehemu ya jamii. Wakristo wanapaswa kushiriki kikamilifu katika jamii zao na kuwa watetezi wa haki. Wakristo pia lazima wawe wenye maadili katika ushirikiano wao wote na hivyo ndivyo watakuwa sauti ya ushawishi kwa wengine kwa haki na kweli. Ni lazima washiriki kwenye serikali na mashirika ambayo yana ushawishi katika jamii alimradi wafanye hivyo bila kukiuka kanuni za kikristo. Kama wataruhusiwa, wapige kura na wawaunge mkono wagombeaji wa nyadhiva za ofisi za siasa ambao wana sifa za kikristo.

► Ni mfano upi wa shinikizo la kijamii kwa kanisa la kufanya uamuzi kwa ajili ya ustawi wa kiuchumi badala ya kufanya uamuzi unaotegemea ukweli wa kimaandiko?

Wakristo na sheria za serikali ya wanadamu

Wakristo katika historia wametatizika kujua jinsi ya kufuata kanuni za kikristo wakati serikali yao inafuata kanuni tofauti. Wakati mwingine mzozo huwa mkali, na wakristo

wanateseka kwa ajili ya msimamo wao wa Imani kwa sababu hawawezi kufanya vitu ambavyo serikali inawahitaji wafanye.

Biblia inatueleza tulipe ushuru ambao unahitajika na serikali (Warumi 13:7, Mathayo 22:21).

Biblia inatuambia tutii sheria za taifa letu (Tito: 3:1). Hata hivyo, biblia pia inatuambia kuwa ni lazima tumtii Mungu wakati wowote ambapo amri za Mungu zinapingana na sheria za mwanadamu (Matendo ya mitume 5:29)

Serikali inaweza kuwataka watu wajiunge na jeshi kupigana vita kwa sababu isiyostahili. Serikali inaweza kutaka vifo vya watoto wachanga ili kupunguza idadi kubwa ya watu. Serikali inaweza kuwataka watu katika nchi washiriki katika utumwa wa kabila au makundi fulani ya kikabila.

Wakati mwingine masuala yanahusu ibada. Wakristo wanaweza kuteswa wasipo abudu miungu ya familia au makabila yao. Wakristo wanaweza kuteswa wakati dini fulani tofauti inapendelewa na serikali.

Kuna mataifa ambayo yana sheria ambayo inaharamisha uinjilisti na mafunzo ya Bibilia. Wakristo wanateswa wanaposhiriki katika kuhubiri injili. Mataifa mengine yanaadhibu wazazi wanaofundisha watoto kuhusu Mungu.

Tuna mifano kwenye Bibilia ya watu wa Imani ambao walikataa kutii amri kutoka kwa watawala waliokuwa na sheria zisokuwa na haki. Daniel aliendelea na maombi yake hata ingawa maombi yalikuwa yameharamishwa**.** Marafiki watatu wa Daniel walikataa kuabudu sanamu ya mfalme. Wakunga wayahudi hawakumtii Farao alipowaamuru waue watoto Wayahudi.

Katika historia, wakristo wamehubiri injili hata kama kufanya hivyo kulikua kumeharamishwa. Kwa kutotii sheria, wameweza kuchukua Biblia na kuzivusha mipaka ya kitaifa. Wakristo wameweza kukusanyika na kuabudu kisiri. Wakristo pia bila kutumia vurugu wameweza kuzuia zahanati za kutoa mimba. Wakristo wamesaidia watumwa kutoroka.

Wakristo wengi wanapendelea kuishi Maisha yao kwa amani bila ya kukabiliana na maamuzi tatanishi kama hiyo. Hata hivyo, kama mkristo atakabiliwa na tatizo la kimaadili ni lazima afanye kile ambacho ni sawa hata kama kinahitaji kuhatarisha maisha. Kama ana fursa ya kuzuia dhuluma au kushiriki injili, anafanya uamuzi mzito anapoamua kuchukua hatua au kutotenda.

► Unaweza kueleza shida ya kisheria inayoweza kutokea kwa mkristo katika nchi yako?

Rushwa

Mchungaji alikua anasafiri katika nchi ya kigeni. Alikuwa na hati sahihi, lakini mara nyingi alisimamishwa na askari ambao walimtaka awape kitu kidogo. Kama hawezi kuwapa fedha watamchelewesha safari yake na watamuweka kwenye hali ya shida.

► Mchungaji atafanya nini katika hali hii?

Hongo/rushwa ni fedha inayolipwa kwa mtu aliye na mamlaka kumshawishi aruhusu kitu fulani. Ni makossa kumuhonga mtu kufanya kitu ambacho yeye hakupaswa kufanya. Kwa mfano kama jengo au gari halihitimizi viwango vilivyowekwa, ni kosa kumuhonga mkaguzi kutia sahihi ya ubora kwa kitu ambacho sio kweli. Ni makosa pia kumuhonga hakimu au askari kutoa hukumu isio ya haki.

Wakati mwingine wale ambao wako kwenye mamlaka wanadai hongo ili kufanya ile wanalopaswa kufanya. Katika hali hiyo, mtu ambaye analipa hongo hamlipi yule anayedai hongo kufanya jambo mbaya. Ni makosa kwa afisa kudai hongo (Luka 3:4), lakini mtu anayelipa wakati mwingine hana chaguo. Kwa mfano kupata kibali cha kitu ambacho unaruhusiwa kupata au kupata uhuru wa mtu ambaye hana hatia. Wakati mwingine hongo ni kama wizi wa kutumia mabavu. Wizi wa kutumia mabavu ni makosa lakini hatuwalaumu mwathirika.

Mtazamo wa maandiko unatuonyesha ya kuwa Mungu anawashutumu wale ambao wanachukua hongo ingawa inawahurumia wale ambao wamelazimishwa kulipa(Kutoka 18:21;23:8; Kumbukumba la Torati 10:17;16:19;27:25). Wakristo hawastahili kulipa hongo kwa urahisi, lakini hawana hatia wanapolazimishwa kulipa na maafisa wafisadi.

► Ni mfano upi wa hongo au rushwa ya makosa?

Huduma za kijeshi

Wakristo wengi wanaamini ya kwamba ni makosa kutumikia kama askari jeshi wa nchi yao. Wanajenga imani yao juu ya sentensi fulani za kimaandiko . Yesu alisema tugeuze shavu lingine mtu anapotupiga shavu moja (Matayo 5:39). Yesu alisema watumishi wake wasipigane, maana ufalme wake sio wa ulimwengu huu (Yohana 18:36). Mtume Paulo alisema silaha zetu sio za kimwili (2 Wakorintho 10:4). Hawa wakristo wanaamini ya kwamba fujo yeyote dhibi ya watu wengine ni makosa. Wengi wa hawa kristo wanaishi kwenye inchi ambazo serikali hairuhusu uhuru na wakristo katika haya mataifa wamenyanyaswa.

Wakristo wengine wanaamini ya kwamba ni lazima tuwe tayari kuilinda nchi yetu kama askari jeshi. Maandiko yanasema Mungu ndiye aliyeweka serikali na serikali inaweza kutumia silaha au zana kuwaadhibu wakosaji (Warumi 13:4). Inaonekana wazi kuwa Mungu alipanga mwanaume kuilinda familia, na kwa hivyo ni jambo la asili kuwa wanaume wanahitaji kuwa na muongozo fulani wa kulinda familia kutokana na mashambulizi kwa kuwa kwenye mfumo wa jeshi. Wakati askari alipomuuliza Yohana mbatizaji namna ya

kutubu, Yohana alimwambia kuwa asikubali kupokea hongo au kufanya unyanyasaji wa kibinafsi lakini hakumwambia atoke kwenye jeshi (Luke 3:14). Yesu aliposema geuza shavu la pili, hakumaanisha ya kwamba hatuwezi kujilinda kutokana na mashambulizi, bali tusilipize kisasi sisi wenyewe kwa sababu ya vitendo vya kukera, kama vile kupigwa kofi usoni. Alisema watumishi wake hawapigani kuanzisha ufalme wa kidunia kwa niaba yake, kwa sababu hataanzisha ufalme kwa namna hiyo. Kama serikali ni jambo la Mungu, na kama serikali inastahili kulinda watu wake, hivyo basi ni vyema wakristo kuhudumia serikali yao kwa kuisaidia kutimiza malengo yake.

Kwa karne nyingi za historia ya kanisa,wakristo wengi katika mataifa mengi wamehudumu kwenye jeshi, hata kwenye mapambano, kwa sababu waliaamini kuwa ni lazima wafanye sehemu yao ya kulinda taifa lao kutoka kwa mashumbulizi mabaya.

Wakristo duniani kote hawana mafikiano kwa jambo la huduma za kijeshi. Ni vyema mtu atafakari kwa maombi maandiko na kutumia fikira zake binafsi, halafu afuate msimamo wa Imani yake kwa uaminifu.

► Makanisa katika inchi yako wanalijibu vipi hili swala la huduma jeshini?

Kushiriki kwa vikundi

Wakrsito wengi wana maoni mazito kuhusiana na haya mambo. Ni muhimu kuelewa kuwa wakristo katika wakati na sehemu tofauti hawajafikia makubaliano kuhusiana na haya masuala. Ni lazima tuepuke kupeana hukumu kuhusu motisha ya wengine kwa sababu ya moani yao.

► Tunapaswa kutathmini vipi uhusiano wa kawaida kati ya serikali na makanisa katika nchi yetu? Je, kuna kitu kinahitajika kubadilika?

Maombi

Baba aliye mbiguni,

Ahsante kwa kubuni serikali kutoa ulinzi na uhuru. Nisaidie niwe mwaminifu kwako licha ya mapungufu ya serikali za wanadamu.

Nisaidie nitimize majukumu yanguya kulinda wengine na kushawishi jumuia yangu.

Tunatarajia kuja kwa ufalme wako kwa ukamilifu.

Amina

Zoezi la somo la 12

(1) Biblia ina hadithi nyingi za Mungu akifanya kazi kupitia maafisa wa serikali kukamilisha kusudi lake katika Maisha ya watu wake. Mithali 21:1 yasema, ”roho ya mfalme iko kwenye mikono ya Mungu, kama vile mito ya maji: yeye anabadilisha anapotaka.” Chagua moja ya hizi hadithi ukazisome:

- Mwanzo 41:14-49, 42:1-3, 45:4-7
- Esta 4, 7-8
- Nehemia 1-2

Andika kuhusu uchunguzi wako:

- Ni kitu gani kilihitajika kufanyika katika Maisha ya watu wa Mungu?
- Jinsi gani Mungu alitumia watawala wasiomcha kutimiza kususdi lake?
- Jinsi gani Mungu alitumia mtu anayemcha kutimiza kusudi lake?

(2) Chagua moja ya mada hizi:

- Ushawishi wa kikristo
- Wakristo na sheria za binadamu
- Rushwa
- Huduma ya kijeshi

Angalia maandiko yanayopatikana katika somo hili kuhusiana na mada yako. Andika ukurasa mmoja ukielezea kile unachofikiri ni mbinu ya kimaandiko kwa mada hii.

Somo la 13
Mwili wa Mkristo

Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kujua vile mambo ya kimwili yanayoathiri afya ya kiroho.

(2) Kuweka wakfu mwili wake mbele ya Mungu na kujifunza tabia mpya ambayo italeta sifa njema kwa Mungu.

Martin Luther, mtumishi wa Mungu

Martin Luther alijibadilisha kuwa mtawa kwa sababu alidhani kwa kufanya hivyo anatumikia Mungu kwa njia iliyo bora zaidi. Nidhamu ya Maisha ya watawa ilijumuuisha utaratibu makini kwenye mpangalio wa chakula, kufunga, kuvaa mavazi ya kawaida, uchache wa mali na useja. Adhma ya Martin ya kuutoa sadaka mwili wake kwa mungu ilimfanya pia auadhibu mwili wake kwa kuuchapa viboko. Baada ya Martin kuelewa ya kwamba injili ya wokovu kwa neema kupitia njia ya Imani, alitambua ya kwamba asingeweza kupata neema kwa kutesa mwili wake. Alibadilisha msimamo wake kuhusu viapo ya kitawa kuwa hazima msingi kwenye Biblia. Baadaye alimuoa Katherina ambaye alikuwa mtawa wa kike na wakabarikiwa kuwa na Watoto sita kwenye ndoa yao.

Utangulizi: Kuchanganyikiwa huko Korintho

Baadhi ya watu huko Korintho hawakuamini kuwa wakristo watafufuka: Walifikiria ya kwamba mwili wa binadamu utaharibiwa baada ya kifo na ni roho tu ya wakristo ndiyo itaenda mbiguni.

Wengine walisema," kwa vile mwili utakufa na utaharibiwa, haijalishi tunafanya nini na mwili sasa hivi. kuutumia mwili kwa vitendo vya dhambi haijalishi, kwa sababu mwisho mwili hauna thamani yoyote".

Wengine waliopinga ufufuo walisema, "Mwili utatupwa kwa sababu tamaa zake ni mbaya. Mbiguni hatutakuwa na tamaa za kimwili. Kwa sababu tamaa za kimwili ni mbaya, hatuhitaji kuzifuata sasa hivi. Kwa hivyo tusile chakula kizuri, tuzivae mavazi mazuri na hata tusishughulike na kukutana kimwili katika ndoa. Tunafanye lolote tuwezalo tuutiishe mwili mpaka wakati tunauacha."

Hizi zote ni dhana potofu. Yote msingi wake ni makosa. Katika I Korintho 15, Paulo anaeleza kwa nini fundisho la ufufuo wa Kristo ni la muhimu.

Ingawa ni vyema sisi tuweze kuongea zaidi kuhusu maisha ya kiroho kuliko maisha ya kimwili, miili yetu huathiri masuala ya kiroho. Mungu alituumba siyo tu kama viumbe wa

kiroho bali wenye roho iliyo ndani ya mwili pia. Sisi siyo tu wanyama wa kawaida, lakini pia siyo viumbe tu vya kiroho ambavyo vinakaa kwenye mwili kwa muda.

Kujiweka Wakfu kwa Mungu

► Mwanafunzi asome 1 Wakorintho 6:19-20 kwa kikundi.

Mistari hii inatueleza kwamba miili yetu ni mali ya Mungu kwa sababu ametukomboa. Miili yetu ni hekalu la roho mtakatifu na hivyo isitumike kufanya dhambi.

Bibilia inatueleza kwamba mwili wa nyama lazima ukabidhiwe kikamilifu kwa Mungu.

► Mwanafunzi asome Warumi 12:1 kwa niaba ya kikundi.

Huu mstari unatueleza ya kwamba miili zetu lazima iwe mitakatifu kwa sababu ni mali ya mungu. Ibada ambayo mungu anataka kutoka kwetu ni kutii kikamilifu.

Hatuwezi kumtumikia Mungu kwa uthabiti kama bado hatuna uwezo wa kudhibiti tamaa zetu za mwili. Tabia yeyote ya dhambi ni kama uraibu (mazoea ya tabia mbaya).

Fikiri kuhusu mnyama aliye na mabwana au waajiri wawili. Mwajiri mmmoja anatoa amri, lakini mnyama hawezi kutii kwa sababu mwajiri ule mwingine amefunga mnyama kwenye mnyororo. Mwajiri mwenye mnyororo anaweza kuvuta mnyama popote atakapo. Mnyama anaweza kuwa na upendo zaidi kwa yule mwajiri mwingine, lakini hawezi kumtii. Hivyo ndivyo mazoea ya tabia mbaya yalivyo. Mtu angependa kumtumikia Mungu lakini mazoea ya tabia mbaya ni kama nyororo ambao inakuwa ni vigumu kuushinda/kuukataa.

Mazoea ya tabia mbaya na aina nyingine za dhambi uharibu mwili na akili. Kwa sababu mili zetu ni mali ya Mungu una imewekwa wakfu kumtumikia, itakuwa ni vibaya tukiiharibu. Mhustari tuliosoma kwenye kitabu cha Warumi unatueleza tutoe miili yetu kama sadaka kwa Mungu lakini hatuwezi fanya hivyo kama hatuwezi kujidhibiti wenyewe.

► Mwanafunzi asome 1 Wakorintho 9:24-27 kwa niaba kikundi.

Mwili wako ni Mtumishi wako, unapaswa kuudhibiti. Ni Mtumishi mzuri sana. Endapo utakosa udhibiti, unakuwa bwana wako, na mwili ni bwana asiye mzuri kabisa (mkorofi)**.** Paulo alisema kwamba alikataa kuruhusu tamaa za mwili kumtawala (1 Wakorintho 6:12).

► Mwanafunzi asome Warumi 6:13 kwa niaba ya kikundi.

Mwili ni kama seti ya zana ambazo unamiliki. Zana ziko chini ya mamlaka yako. Hauzitumii tena kwa kutenda dhambi lakini kwa ajili yaMungu.

Tamaa za Asili

Kuna baadhi ya watu ambao wanafikiria kwamba hatuwezi kuepuka dhambi kwa sababu ya tamaa zetu za asili. Ni kweli kwamba tumezaliwa na asili ya dhambi ambayo inatufanya tutende dhambi. Asili hiyo inajuumuisha sio tu tamaa za kimwili lakini pia tamaa za akili na utashi unaoegemea kwenye dhambi. Mtu ambaye hajazaliwa upya na Roho wa Mungu hana

uwezo wa kujizuia kufanya Dhambi, ingawa anaweza fanikiwa kwa kiwango fulani kujizuia baadhi ya dhambi. Mwenye dhambi ambaye hajapokea neema ya mungu anaweza asiamini kwamba anaweza kuishi maisha ya ushindi.

Tamaa za asili siyo ndiyo tatizo. Ni Mungu ndiye aliyeumba tamaa hizi za asili. Adam alikua na tamaa za asili na hakua mwenye dhambi mpaka alipofanya uchaguzi wa kutomtii Mungu. Hizi tamaa ni sehemu ya vile ambavyo Mungu alikusudia mwanadamu awe. Tamaa zenyewe siyo dhambi, lakini zinafanya uwezekano wa majaribu kufanyika.

► Mifano ya tamaa za asili ni nini?

Chati ifuatayo haijaweka kila kitu, lakini inatupa mifano ya tamaa za asili, baadhi ya kawaida na matumizi bora ya hizi tamaa na baadhi ya njia ambazo hizi tamaa zinaweza kufanya majaribu yafanyike.

Tukizitazama tutaona ya kwamba tamaa za asili sio lazima ziwe ni kama tamaa za mwili. Ni asili kwa sababu zinatoka katika asili ya mwanadamu, ingawa zote sio tamaa za kimwili.

Makundi ya Tamaa za asili	**Mfano wa utumiaji bora wa tamaa za asili**	**Uwezekano wa dhambi**
Kujihifadhi	Kuchukua tahadhari za usalama	Uwoga
Kukubalika mbele ya wengine	Kuvaa kwa ungalifu, kuonyesha heshima	Kiburi, wivu
Kuridhika kimwili	Kula chakula, kulala, na kuwa na tendo la ndoa kwenye ndoa	Kujifurahisha kwa dhambi
Kufurahia kijamii	Kuwa na ushirika na wengine	Usengenjaji, uzushi
Faraja ya kimwili	Kupendelea utulivu na amani	Uvivu, tamaa ya mali
Uthabiti wa kifedha	Kuweka akiba na kufanya uwekezaji	Ufisadi, udanganyifu

► Kuna tamaa yeyote ya asili ambayo unaweza kutii daima?

Hakuna tamaa yeyote ya asili inaruhusiwa kutuongoza bila kujiuliza maswali. Hakuna tamaa ya asili ambayo utafuatwa daima na kwa usalama kwa sababu tamaa haiweki ukomo wa yale yanayofaa kwako. Kwa mfano, hamu ya njaa haitofautishi kati ya chakula chako na cha mtu mwingine au uwezo wa mtu kununua chakula.

Kuna wakati ambapo kudhihirisha kihalali hisia hata kama ni nzuri ni lazima uzuiliwe. Sio kwa sababu mtu anahisi njaa ina maana kuwa anaweza chukua chakula cha mwenzake. Nikawaida kutamani kupumzika lakini wakati mwingine utafanya kazi hata ukiwa umechoka. Ni kawaida kwetu kuepuka hatari, lakini lazima mtu akabiliane na ushawishi wa kutaka kuepuka hatari anapotakiwa kuwajibika ili kumuokoa mwingine.

Hamu za kawaida zinaweza kuharibiwa na kufanywa kukosa mwelekeo hadi kuchukua mtindo ambao si wa kibinadamu na si wa asili. Hiyo ndiyo sababu watu hufanya mambo potovu na ya jeuri. Hamu ya asili huharibiwa na kukosa mwelekeo kwa sababu ya mafundisho potovu, kukuzwa kwa mtindo mbaya wa mawazo, kuwa katika mazingira ya dhambi, au matendo maovu ya mtu binafsi.

Kila muumini anatarajia kupata majaribu kwa sababu ya tamaa au hamu ya asili. Neema haiondoi tamaa za asili, lakini inampa mtu nguvu ya kudhibiti matendo yake na kuelekeza hamu yake kwenye mambo mazuri.

Hamu ya kawaida hufanya nidhamu ya kiroho kuwa ya muhimu ili upate ushindi wa kiroho. Neema haikuweki huru kutokana na hitaji la kutii maelekezo ya maandiko, kuhudhuria ibaada, kuutiisha mwili, maombi na kujifunza Biblia. Muumini anaye maanisha kupata ushindi wa kiroho anaweza akajiwekea mipaka ili alinde maeneo yake ya udhaifu.

Majaribu yataonekana ya kuvutia, lakini moyo ukiwa umethibitishwa katika mapenzi ya Mungu, mtu anaweza kataaa majaribu kutoka moyoni mwake (1 Yohana 5:3). Hataona kama amepoteza kile ambacho kingemfanya awe na furaha. Kwa imani atajua ya kwamba Mungu hawezi kuzuia kile ambacho hakina madhara, hata kama haoni madhara ya kile kitu ambacho kimekatazwa (Kumbukumbu La Torati 6:24). Kwa imani anajua kwamba hakuna kitu ambacho ni kinyume na mapenzi ya Mungu kitamtosheleza, kwa sababu utoshelevu wake unapatikana ndani ya Mungu (Zaburi 16:2, Zaburi 84:11).

Lishe Bora na Mazoezi

► Maandiko yasema nini kuhusu chakula?

Hakuna katazo mahususi katika Biblia kuhusiana na chakula. Katazo la kutokutumia baadhi ya vyakula katika Agano la Kale hayakuhitajika kwa Wakristo wa Agano Jipya. (1 Timotheo 4:4, Marko 7:19). Kulikuwa suala la chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu, lakini hiyo haikuwa kwa sababu chakula chenyewe kilikuwa kibaya, lakini ni kwa sababu watu walikula kile chakula kama sehemu ya kuiabudu sanamu (1 Wakorintho 8).

Lishe ni muhimu kwa afya ya mwili na nguvu. Kwa sababu sisi ni watumishi wa Mungu ni vizuri tuwe na afya njema. Tusijaribu kuharibu miili yetu au kuyafupisha maisha yetu kwa

sababu ya lishe mbaya. Watu wengi hawana chaguzi nyingi za lishe, kwa sababu ni lazima wale kile ambacho kinapatikana na wanaweza kumudu, lakini ni vizuri wafanaye mamuzi mazuri kwa kadri iwezekanavyo. Pia ni vizuri wawafundishe watoto wao kuhusu kuchagua lishe bora.

Watu wengi ambao wana fedha za kutumia kunua chakula hutumia kwa kununua chakula kingi sio kwa sababu ni lishe lakini kwa sababu ya ladha wanazozipenda. Pia kuna jaribu la kutumia fedha nyingi kwa kununua chakula ambacho hakina umuhimu mwilini. Watu wengine huona ni vigumu kununua kitabu cha huduma chenye mafundisho, lakini wanatumia fedha kiasi hicho kwa biskuti na soda.

Mazoezi ya mwili ni ya muhimu kwa mtu ambaye anataka kuishi maisha mazuri. Mtu yeyote hatakiwi kuruhusu ukosefu wa mazoezi kumsababishia ukosefu wa nguvu au kupata uzito uliozidi ambao unaweza kumzuia mtu kufanya yaliyo mazuri kwa Mungu. Kama ajira ya mtu inahitaji nguvu za mwili hahitaji mazoezi ya ziada; vinginevyo, anapaswa kuweka mwili wake ili uwe katika hali nzuri.

Mkristo anapaswa kufikiria lishe bora na mazoezi kwa maana yeye ni wa Mungu. Japokuwa maelekezo mahususi kuhusiana na lishe na mazoezi hayapo katika Biblia. Watu lazima watafute njia na kanuni za kujitoa kwa Mungu katika hali zinazo wakabili. Lazima tuepuke kuhukumu na kukejeli wengine. Mambo haya yasifanywe sheria ya maisha ya Kiroho ispokuwa kama kipo kikundi maalum cha watu ambao wameamua kufuata hiyo njia.

► Mwanafunzi asome Warumi 14:4 kwa niaba ya kikundi.

Ni lazima kila mmoja wetu kuzingatia kanuni za maandiko katika njia fulani, lakini tusiwahukumu wanaozitumia njia nyingine, wakati ambapo matumizi mahususi hayapo katika maandiko.

Uponyaji wa mwili wa ki-muujiza

► Mwanafunzi asome Warumi 8:18-23 kwa niaba ya kikundi.

Ugonjwa ni matokeo ya laana ambayo ilikuja kwenye uumbaji wote kwa sababu ya dhambi ya mtu wa kwanza. Mpango wa Mungu wa ukombozi utarejesha hali ya kwanza ya uumbaji na kumaliza mateso yote. Hata hivyo aya hizi zinasema urejesho hautafanyika kwa pamoja na mara moja. Japokuwa tumeokolewa tayari, miili yetu itaendelea kuzeeka na kuugua magonjwa hadi mpango wa Mungu wa ukombozi ukamilike.

Tayari Mungu hufanya miujiza katika dunia hii. Miujiza nyingi ya uponyaji imerekodiwa katika Biblia. Mungu ameahidi kuponya kupitia maombi ya imani itakayo fanywa na kanisa (Yakobo 5:14-15). Sio lazima mgonjwa awe na imani yake mwenyewe ili apate uponyaji; kanisa laweza kuwa na imani kwa niaba yake. Kwa hivyo mgonjwa asilaumiwe kwa kukosa imani.[39]

[39] Yesu aliponya aliyepooza kwa sababu ya imani ya marafiki wake (Marko 2:5).

Hatutarajii kwamba mtu mwenye imani hatapata ugonjwa. Mungu aliruhusu Ayubu ateseke mwili wake kwa muda japokuwa Ayubu alikuwa mwaminifu kwa Mungu (Ayubu 2:8).

Paulo anasema Mungu aliruhusu mwiba katika mwili yake ili kumfanya anyenyekee na amtegemee Mungu. Paulo aliomba mara tatu kwa ajili ya uponyaji lakini mwishowe aligundua ya kkwamba Mungu alitaka kumpa ustahimilivu na sio uponyaji (2 Wakorintho 12:7-9). Inaonekana kwamba kuna uwezekano mwiba katika mwili wake ulikuwa ni kuugua kwa mwili wake japokuwa hatuna uhakika kwa hilo.

Paulo aliteseka alipokuwa anahubiri injili kwa Wagalatia (Wagalatia 4:13-15). Inaonesha Paulo alikuwa na shida katika macho yake, kwa sababu anawambia Wagalatia kwamba walimpenda kiasi ya kwamba wangejitolea kumpa macho yao. Hatujui kama Paulo aliponywa badaye, lakini hakuponywa mara moja. Ni wazi ya kwamba Paulo hakuundisha kwamba ni lazima kila mwamini awe huru kutoka magonjwa, na Wagalatia hawakufikiri kwamba ugonjwa wake unahitilafiana na injili aliyo hubiri.

► Mwanafunzi asome Wafilipi 2:25-30 kwa niaba ya kikundi.

Epafrodito alikuwa mgonjwa na katika hatari ya kifo. Alikuwa mgonjwa kwa sababu alifanya kazi sana kumsaidia Paulo. Paulo anasema kwamba Epafrodito anastahili heshima kwa sababu alihatarisha maisha yake kwa ajili ya kazi ya Kristo.

Mfano wa Ayubu, Paulo na Epafrodito inatuonesha kwamba hatuwezi walaumu watu kwa kukosa imani wakiwa wagonjwa. Tusichukulie ya kwamba wanadhibiwa kwa sababu ya dhambi zao. Ni Mungu pekee anayejua kama kuna sababu ya kiroho inayosababisha mateso. Baadhi wa Wakristo mashuhuri katika historia, watu wa imani kubwa waliugua kwa muda mrefu.

Biblia haizuii matumizi ya dawa na kutembelea madaktari. Hata kama tunaomba afya njema na uponyaji siyo vibaya kutumia msaada uliyo karibu.

Ni makosa kutafuta uponyaji kutoka kwa watu wanaodai kutumia nguvu za uchawi au tumia roho ambazo hazitoki kwa Mungu. Hatumtumikii shetani na hatuwezi kutafuta faida kutoka kwake. Uaminfu wetu ni kwa Mungu na tunapaswa kuridhika na baraka zake. Akichagua kutoponya tunastahili kuomba neema zake na nguvu zake na tubaki kuwa waaminifu.

Dawa hatari

Watu wengine hutumia vitu ambayo inafanaya miili yao kuchangamka na vina matokeo mabaya.

Dawa za kulevya huharibu mwili, mawazo, na husababisha uraibu na ni kinyume cha sheria Sehemu nyingi duniani.

Isipokuwa kwa kiwango kidogo, pombe huathiri mtazamo wa binadamu na husababisha yeye kufanya na kutenda katika hali ambayo asingefanya kama asingekuwa ameathirika. Pombe inauraibu. Kwa viwango vikubwa inazorotesha afya. Inatumika zaidi katika Sehemu

za burudani za kidunia zisizofaa. Biblia haijakataza pombe waziwazi lakini makanisa mengi hukataa kwa sababu inaathiri tabia, maamuzi, na inauraibu na mara kwa mara husababisha na tabia mbaya. Wakristo wengi wana wasiwasi kwamba mtu akitumia pombe kwa uangalifu huku akizuia hatari zake, anaweza kuwadhuru wengine vibaya hasa vijana.

► Mwanafunzi asome Mithali 20:1 na 31:4-5 kwa niaba ya darasa.

Tumbaku, ikivutwa au ikitafunwa mara kwa mara ina uraibu na inafupisha maisha kwa asilimia fulani. Anayetumia yuko katika hatari kubwa ya kupata saratani.

Biblia haijakataza mihadarati, pombe au tumbaku moja kwa moja. Japokuwa, watu wengi wanaoelewa madhara yake wanaamimi ya kwamba mkristo hapaswi kutumia. Hiyo haijawahi kuwa sawa hivyo kila mahali, katika nyakati kabla watu hawajajua madhara kamili ya dutu (sabstance) hizi.

Hatari iliyo kuu ya dutu hizi ni uraibu. Uraibu huongoza maisha ya Mwanadamu. Hutumia rasilimali zake. Inaathiri mtazamo wake na maamuzi na hufanya yeye kuona ni vizuri. Yeye hufanya maamuzi ambayo yanaumiza familia yake na kazi. Uraibu huo unadai uaminifu unaofanana na wa dini, na unaopingana na uaminifu kwa Mungu.

Usafi na Mwonekano

Mkristo anapaswa kuwa na tabia za usafi wa kimwili ambazo ni nzuri angalau kama desturi za kawaida katika utamaduni wake. Hapaswi kuwa na sifa mbaya ya mwili kuwa na harufu mbaya, nywele ambazo haijashughulikiwa au nguo ambazo ni chafu au zilizo katika hali mabaya. Mtu aliye katika umaskini anaweza kupata ugumu kuwa katika mwonekano mzuri lakini afanye bidii kwa kadri awezavyo.

Lazima usikilize rafiki zako wanapokukosoa kuhusiana na mwonekano wako na usafi. Wazazi lazima wafundishe watoto wao tabia nzuri.

Wakristo hawapaswi kufuatisa namna ya ulimwengu huu kwa kutumia mavazi au mapambo ili kujionyesha kuwa wao ni bora kuliko wengine. Hata hivyo kuonekana kuwa asiyejali kunaweza kuonyesha ya kwamba mtu hana heshima kwa wale ambao anakutana nao. Kwa mfano kama haujali kuvaa kwako unapoenda kwenye kikao inaweza kumaanisha hauheshimu kikao wala watu waliopo katika kile kikao. Wakristo wanapaswa kuonyesha heshima kwa Mungu na kwa wengine kwa mwonekano wao mzuri.

Watu ambao hawana vipaumbele katika maisha ya kiroho na ya milele wanatumia miili yao na mavazi yao ili wapate kutambuliwa. Mwanaume angependa kuonyesha misuli yake. Mwanamke angependa kuonyesha urembo wake wa mwili kwa wanaume. Mkristo hastahili kuonyesha maringo na kupata mtazamo mbaya kupitia mavazi yake.

Kushiriki kwa vikundi

Watie moyo wanafunzi kufikiri jinsi ambavyo kujitoa kwa Mungu kunatakiwa kuleta mabadiliko katika maisha.

► Je, tabia zako zinaoneshaje ya kwamba mwili wako ni mali ya Mungu?

Epuka mijadala mirefu yeyote ambayo inalenga kuweka sheria za lishe au vikwazo sawa kama matakwa kwa wakristo.

► Utamwelezaje mtu juu ya kwa nini hutumii vitu fulani?

Maombi

Baba wa mbinguni,

Asante kwa mpango mzuri uliotupa sisi wa kuishi kwanza duniani na baadaye mbinguni.

Nisaidie niishi maisha makamilifu ya kujitoa kwako nikijua ya kwamba uliniumba na ukanikomboa mimi.

Nisaidie niishi kwa huru kutoka kwa chochote ambacho kinaweza kuzuia huduma yangu kwako na kukuabudu wewe.

Asante kwa heshima nzuri kwamba niwe hekalu la Roho Mtakatifu. Nataka kuishi kwa namna inayokuheshimu.

Amina

Zoezi la somo la 13

(1) Andika jibu kwa kila swali lifuatalo katika kitabu chako binafsi (Hii sio ya kumpa kiongozi wa darasa.)

- Je umejitoa kwa Mungu kikamilifu? Hii ina maanisha nini kwako?
- Ni tamaa gani za asili ambazo mara nyingi hukuongoza kwenye majaribu maishani mwako?
- Maandiko gani mawili au matatu ambayo itakubidi uyakariri ili yakusaidie kuyashinda majaribu haya?
- Mabadiliko gani ambayo Mungu amesema na wewe ubadilishe katika somo hili?

(2) Soma 1 Wakorintho 15. Kwanza gawa vifungu katika sehemu ndogo ndogo ukieleza ujumbe katika kila sehemu hizo. Andika mstari katika kila fungu. Ni hatua gani ya kuchukua ukizingatia somo hili?

Vyanzo Vinavyopendekezwa

Ili kujifunza zaidi kuhusu masomo yaliyodadavuliwa katika kozi hii, tafadhali angalia vyanzo vifuatavyo.

Somo la 1 - Uadilifu wa Mkristo

McDowell, Josh, and Bob Hostetler. *Right from Wrong.* Nashville: W Publishing Group, 1994.

Sider, Ron. *The Scandal of the Evangelical Conscience.* Grand Rapids: Baker Books, 2005.

Somo la 2 - Mazoezi ya utii kwa Mungu

Keep, Tim and Becky. *It's All about Obedience.* Shoals: Whispering Pines Publishing, 2016.

Spiritual Formation (course from Shepherds Global Classroom). Available online or in print at: https://www.shepherdsglobal.org/courses

Somo la 3 - Kazi

McQuilkin, Robertson. *An Introduction to Biblical Ethics.* (Second Edition). Wheaton: Tyndale House Publishers, Inc., 1995.

Somo la 4 - Mahusiano

Chapman, Gary. *The Five Love Languages.* Chicago: Northfield Publishing, 2015.

Carnegie, Dale. *How to Win Friends and Influence People*. New York: Pocket Books, 1936.

Somo la 5 - Kuongozwa na Mungu

Duewel, Wesley. *Let God Guide You Daily*. Greenwood, IN: One Mission Society, 1988.

Masomo 6-7 - Ndoa

Drescher, John. *For Better, For Worse.* Morgantown, PA: Masthof Press, 2012.

Eggerichs, Emerson. *Love and Respect*. Nashville: Thomas Nelson, 2004.

Thomas, Gary. *Sacred Marriage.* Grand Rapids: Zondervan, 2000.

Somo la 8 - Ekolojia ya Mkristo

Schaeffer, Francis, Udo W. Middelmann, Lynn White Jr., and Richard Means. *Pollution and the Death of Man*. Wheaton: Tyndale House, 1970.

Somo la 9 - Fedha

Ramsey Dave. *The Financial Peace Planner*. New York: Penguin Books, 1998.

Wesley, John. "The Use of Money" (a sermon). Available online at https://www.whdl.org/use-money-sermon-50 (as of January 14, 2021).

Somo la 10 - Uaminifu

Covey, Stephen M. R. *The Speed of Trust: The One Thing that Changes Everything.* New York: Free Press, 2006.

Somo la 11 - Thamani ya Binadamu

Lewis, C. S. *The Abolition of Man*.

Colson, Charles and Nancy Pearcey. *How Shall We Now Live?* Wheaton: Tyndale House Publishers, 1999.

Somo la 12 - Serikali

Schaeffer, Francis. *A Christian Manifesto*. Wheaton: Crossway Books, 1981.

Somo la 13 - Mwili wa Mkristo

Foster, Richard. *Celebration of Discipline*. New York: HarperCollins Publishers, 1978.

Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa

Jina la Mwanafunzi _____

Kwenye jedwali hapa chini, dhihirisha kwa alama za jina lako ukionesha ni lini ulikamilisha kazi za kufanya ulizopewa. Kazi zote ulizopewa kufanya ni lazima zikamilishwe kwa ukamilifu ili uweze kupatiwa cheti cha kuhitimu kutoka Shepherds Global Classroom.

Somo la	Kazi ya kufanya 1	Kazi ya kufanya 2	Kazi ya kufanya 3
1			
2			
3			
4			
5			
6			
7			
8			
9			
10			
11			
12			
13			

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kujazwa na kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).

Maelezo ya Kozi za Shepherds Global Classroom

Kuchambua Agano la Kale

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 39 vya Agano la Kale.

Kuchambua Agano Jipya

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 27 vya Agano Jipya.

Maisha na Huduma ya Yesu

Kozi hii inasoma maisha ya Yesu kama mfano kwa huduma na uongozi katika karne ya 21.

Warumi

Kozi hii inafundisha theolojia ya wokovu na dhamira kama inavyoelezewa katika vitabu ya Warumi, kujadili masuala kadhaa ambayo yamekuwa ya kutatanisha katika kanisa.

Kanuni za Tasfiri ya Kibiblia

Kozi hii inafundisha kanuni na njia za kutafsiri Biblia vizuri ili kuongoza maisha yetu na mahusiano na Mungu.

Imani za Kikristo

Hii ni kozi ya theolojia ya kimfumo, inayoelezea mafundisho ya Kikristo kuhusu Biblia, Mungu, Mwanadamu, Kristo, Wokovu, Roho Mtakatifu, Kanisa, na Vitu vya Mwisho.

Eskolojia

Kozi hii inafundisha vitabu vya kibiblia vya Danieli na Ufunuo pamoja na sehemu zingine za maandiko ya kinabii na inasisitiza mafundisho muhimu kama vile kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho, na ufalme wa Mungu wa milele.

Mafundisho na Mazoezi ya Maisha Matakatifu

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatarajia na uwezesho kwa Mkristo.

Mafundisho na Mazoezi ya Kanisa

Kozi hii inaelezea ubunifu na mpango wa Mungu kwa kanisa na masomo ya kibiblia kama vile uanachama wa kanisa, ubatizo, ushirika, zaka, na uongozi wa kiroho.

Historia ya Kanisa I

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyotimiza dhamira yake na kutunza mafundisho muhimu kuanzia kipindi cha kanisa la mwanzo mpaka Matengenezo.

Historia ya Kanisa II

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyopanuka na lilivyopitia changamoto kuanzia kipindi cha Matengenezo mpaka nyakati za kisasa.

Uundaji wa Kiroho

Katika kozi hii wanafunzi wanajifunza kuwa na mitazamo ya yesu, kuwa na Mungu kama Yesu alivyokwa na baba yake, kujinyenyekeza kama Yesu alivyofanya, kufanya nidhamu ya kiroho na binafsi ya yesu, kuvumilia mateso kama Yesu alivyofanya, na kushiriki katika jamii ya Kikristo (Kanisa) lililoundwa na Yesu.

Huduma ya Uongozi

Kozi hii inahimiza tabia ya Kikristo wakati inafundisha viongozi kuongoza mashirika kupitia mchakato wa kugundua maadili, kutambua kusudi, kushirikishana maono, kuweka malengo, kupanga mkakati, kuchukua hatua, na kupitia mafanikio.

Kanuni za Mawasiliano

Kozi hii inafundisha theolojia ya mawasiliano, njia za kuzungumza kwa ufanisi, na njia za kuandaa na kuwasilisha mahubiri ya kibiblia.

Uinjilisti wa Kibiblia na Uanafunzi

Kozi hii inatoa kanuni za kibiblia ambazo huongoza mbinu za uinjilisti. Inaelezea aina za uinjilisti na kutoa masomo ya kutumia kufundisha wapya waliobadilishwa.

Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani

Kozi hii inafundisha misingi ya kisayansi, kihistoria, na kifalsafa kwa mtazamo wa ulimwengu wa Kikristo, na inaonyesha jinsi gani imani ya Kikristo ni thabiti katika hoja na hali halisi.

Dini za Ulimwengu na Ibada

Kozi hii huumpa muumini wa kiinjili uelewa wa mafundisho na majibu sahihi kwa vikundi kumi na nane vya dini.

Utangulizi wa Kuabudu Kikristo

Kozi hii inaelezea jinsi gani kuabudu huathiri nyanja zote za maisha ya muumini na hutoa kanuni ambazo humuongoza mtu binafsi na mkutano wote mazoezi ya kuabudu.

Kuishi Kikristo kwa Vitendo

Kozi hii hutumia kanuni za kiroho kwa utumiaji wa fedha, mahusiano, mazingira, mahusiano na serikali, haki za binadamu, na maeneo mengine ya kuishi kwa vitendo.

Ndoa ya Kikristo na Familia

Kozi hii inatoa mtazamo wa Kikristo kuhusiana na maendeleo ya binadamu kupitia hatua mbalimbali za maisha na zinatumia kanuni za kimaandiko kwa ajili ya majukumu ya kifamilia na mahusiano.